ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/Jimbo la Donge
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura

10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z/Jimbo la Jang'ombe
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Uteuzi wa Rais
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake
21.Mhe. Iddi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali

22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole

34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile
41.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja
42.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
43.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani
44.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni
45.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe
46.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani
47.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe

48.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi
49.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
50.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni
51. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni
52.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba
55.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake
56.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe
57.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani
58.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka
64.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja
65.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani
67.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja

68.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini
71.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
74.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
75.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Zahra Ali Hamad	Nafasi za Wanawake
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nne – Tarehe 24 Juni, 2009

(*Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)*

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Watoto Zanzibar 2009.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 4

Uharibifu wa Mali

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Mvua za masika za mwaka huu 2009 zimeleta athari kubwa katika kisiwa cha Pemba kwa kuharibu nyumba zisizopungua Hamsini (50) Wilaya ya Micheweni na Thalalthini (30) Mtambwe; pamoja na kubomoka kwa jengo la kupumzikia abiria huko Bandari ya Wete ambako baadhi ya watu waliumia.

(a) Je, Mhe. Waziri, Serikali imetoa msaada gani katika maeneo hayo yaliopata maafa.

(b) Je, Mhe. Waziri, kimakisio maafa hayo yamesababisha hasara ya kiasi gani cha fedha.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, sio kila tatizo au ajali huwa ni Maafa ya Kitaifa, yapo matatizo au ajali yanashughulikiwa na mtu mwenyewe binafsi, familia, Shehia, na yapo yanayoweza kuitwa maafa yanayoshughulikiwa katika ngazi ya Wilaya, Mkoa

hadi Taifa. Vile vile zipo ajali au majanga yanayoshughulikiwa na Taasisi husika.
Baada ya maelezo haya, ninaomba kumjibu Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:-

(a) Tatizo lililojitokeza huko Mkoa wa Kaskazini Pemba la jengo la kupumzikia abiria lilishughulikiwa kwa ukamilifu na uongozi wa Shirika la Bandari.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Kamati ya Maafa ya Mkoa wa Kaskazini Pemba idadi ya nyumba zilizopata athari ya mvua za masika ni 38 na sio zaidi ya 50 kama alivyoeleza Mhe. Mjumbe. Kutokana na hali duni ya kipato cha Wananchi na Utamaduni uliopokewa wa ujenzi nyumba nyingi ni hafifu kimuundo, nyumba hizo zimejengwa kwa miti na udongo na kuezekewa makuti. Kwa hiyo wakati wa mvua kubwa kama zilizonyesha wakati huo, nyumba hizo zilipata athari ya kuroana na kurishai, jambo ambalo ni la kawaida kwa nyumba nyingi za aina hiyo.

Kwa ujumla matatizo hayo hayakufikia hatua ya kuwa Maafa ya Kitaifa kwa mujibu wa Sheria. Afisi yangu inawashauri wananchi wote kwa jumla kuacha kujenga mabondeni na kujenga nyumba imara zinazostahamili hali ya hewa ya nchi yetu.

(b) Kwa vile matatizo haya yote mawili hayakufikia kiwango cha maafa kama nilivyotangulia kusema Wizara yangu, haikufikia hatua ya kufanya makisio.

Mhe Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, athari hii ilipotokea ya kuharibikiwa na nyumba kwa mvua nyingi zilizonyesha serikali kwa kutumia mawakala wake kama Masheha na hata Afsa Tawala walikwenda katika baadhi ya watu waliopata athari hii wakaangalia na kupiga picha, na wakasema kwa vyovyote itakavyokuwa serikali itapeleka mkono wake wa msaada. Sasa ikiwa Mhe. Waziri amejibu hivyo, hivi viwango hasa au tuseme kwa hao masikini wa Mungu waliojenga nyumba hizi kwa kutumia udongo na makuti na ikatokea athari kama hii sio wa kusaidiwa, wakusaidiwa ni wale wenye nyumba za kudumu tu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny:Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi. Mhe. Spika, nilijibu katika jibu langu la

msingi ni kwamba kisheria hakikufikiwa kiwango cha maafa, sheria inasema maafa ni matokeo ya kimaumbile bila ya misaada au kupangwa na binaadam na inajumuisha matukio kama mitetemeko ya ardhi, tufani yaani kimbunga, mafuriko, ukame, moto au mripuko wa maradhi ya kuambukiza hayo ndio maafa katika tafsiri ya sheria.

Sasa haya yanatokea katika sehemu nyingi sana na ikiwa kila nyumba ikipata matatizo kama hayo tulipie na haijafikia kiwango kutakuwa kuna matatizo, sikusema kwamba wanaolipwa ni wale waliojenga nyumba za kudumu tu, nimesema tujitahidini na muhimu kujiunga katika mipango mbali mbali ya serikali inayoletwa kwa kuongeza kipato ili tujitahidi kujenga nyumba ambazo zitastahamili matatizo ya hali ya hewa kwa nchi yetu.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, huu mfuko wa maafa unatushughlisha sana na hatujui unaanza vipi na unamalizia vipi. Hivi karibuni katika jimbo langu Wilaya ya Kaskazini (A), Shehia ya Kikobweni kuna nyumba moja iliingia moto, bahati mbaya mtoto akafariki, mama nae akafariki na mume yuko hospitali. Lakini bado ukitafuta msaada wa maafa huujui uende wapi.

Hivyo Mhe. Waziri mfuko huu upo au upo kama hadithi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, ni vizuri na inafaa sana tukaribishe utamaduni wetu kwa kusaidiana katika maeneo yetu pamoja na kuwa kuna mfuko wa maafa, lakini vizuri tukarejesha utamaduni huo. Utamaduni mwenzetu anapopata tatizo basi huwa anasaidiwa na jamii iliyomzunguuka, sasa kama hatukufanya hivyo kweli tutajikuta kila kinachotokea katika maeneo serikali ndio ifidie. Nimesema katika jibu langu la msingi kwamba maafa yapo yanayoshughulikiwa na shehia, yapo yanayoshughulikiwa na Wilaya, yapo yanayoshughulikiwa na Mkoa kutokana na kile kiwango.

Sasa katika tatizo alilopata yeye mimi ninavyojua mtu akipata tatizo kama hilo wale wananchi waliomzunguuka kwanza humuonea huruma, halafu hufanya michango fulani kumsaidia. Ni mwendo mzuri kusaidiana katika maeneo yetu, na hata kama ikibidi kumjengea nyumba. Kuna watu wamepata matatizo kama hayo wamejengewa nyumba kwa kutwa moja tu na watu waliokuwepo pale katika maeneo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Kwa kuwa mfuko huu unaitwa wa maafa namwomba Mhe. Waziri aje atueleze maafa haya yafikie familia ngapi ili yaweze kutolewa kutoka Mfuko wa serikali, kwa kuwa maafa yanaweza kutokezea ikawa nyumba hamsini, lakini zikawa ziko maeneo mbali mbali.

b) Je, kuna sharti ya nyumba zile kuwa zimekusanyika pamoja au zinaweza kuwa mbali kupatwa na maafa hayo na zikaweza kupewa msaada.

c) Serikali ndio inayokusanya kodi tunategemea ni nani wa kusaidia wananchi wake kama sio serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi) Mhe. Spika, maafa hayasemi idadi ya familia maafa inasema ni matetemeko ya ardhi, tufani yaani kimbunga, mafuriko, ukame, moto au mripuko wa maradhi ya kuambukizwa. Sasa haya yanapotokea sio kama watu lazima wajikusanye pamoja yanaweza kutokea kama tulivyofanya hivi karibuni tu wenzetu pale kwa Kwahani walipata matatizo ya mafuriko na serikali ikatia mkono wake katika kuwasaidia hilo ni moja.

La pili kuhusu serikali ukweli serikali ndio inayokusanya kodi na ndio inayotakiwa kusaidia wananchi, lakini pia na sisi wananchi wenyewe tujenge utamaduni wa kusaidiana.

Nam. 93

Masomo Wanayofanya Vibaya Wanafunzi wa Zanzibar Katika Mitihani yao.

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Kuna masomo ambayo wanafunzi wetu hufanya vibaya sana katika mitihani yao.

a) Mhe. Waziri, Wizara yako ina mpango gani kuimarisha ufundishaji wa masomo hasa Kiingereza, Hisabati na masomo ya sayansi ili kusaidia wanafunzi wapate matokeo mazuri katika mitihani yao.

b) Ukitoa tatizo la walimu kuna sababu gani nyengine inayowafanya wanafunzi wetu kufanya vibaya masomo haya kwa mujibu wa utafiti wa Wizara.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 93 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Wizara imechukua hatua za kuimarisha ufundishaji wa masomo hayo, miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kuanzisha mafunzo maalum kazini kwa walimu wasio na sifa za kufundisha masomo ya Sayansi na Hesabati ili kuweza kuinua uwezo wao. Mafunzo hayo yanayojulikana kwa jina la *teacher Advacement Programme (TAP)* yamekuwa yakiendeshwa kwa ushirikiano na *Aga Khan Foundation.* Pia, kuanzishwa kwa kozi za stashahada ya Sayansi kwa walimu wa Sekondari katika Chuo cha Kiislamu. Pia, tumechapisha zaidi ya vitabu milioni moja vya Masomo ya Sayansi na Hisabati na kusambazwa katika skuli zote za sekondari. Aidha, Wizara imeandaa kambi za sayansi ambazo zimesaidia sana katika kuwapa wanafunzi mazoezi ya vitendo.

b) Mbali ya uhaba wa walimu wa masomo ya Kiingereza, Hisabati na Sayansi. Skuli zetu zilikuwa zinakabiliwa na uhaba wa vitabu vya kiada na vifaa vya maabara.

Pia, Wizara kupitia mradi wa elimu ya lazima inakusudia kuandaa mafunzo ya ualimu kazini kupitia vituo vya walimu kwa ajili ya kuimarisha ufundishaji wa masomo hayo. Vile vile kwa upande wa elimu ya msingi, kazi za kuandaa mitaala na silabasi mpya zinaendelea.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, nakubaliana na majibu ya Mhe. Waziri kwamba jitihada zinafanyika ili kuondoa adha hii au kilio hichi cha kukosa wanafunzi wetu kupasi vizuri katika kukosa nafasi za masomo ambayo nimeyataja hapa, lakini hivi sasa kuna malalamiko baadhi ya maskuli wanafunzi wa darasa la kumi katika skuli ambayo nimeletewa malalamiko kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii Skuli ya Kiwengwa, hivi leo kuna walimu hawazidi wawili wanakosa masomo ambayo ni lazima baada ya vipindi viwili tena wanakosa masomo ya vipindi vyote vya elimu wanayopata.

Je, Mhe. Waziri, hivyo tuseme Wizara katika jitihada hizo inazingatia vipi kupitia madarasa ambayo yanahusika na sekondari au elimu ya msingi kujua upungufu halisi wa walimu ili wapate elimu ambayo inastahiki na wafaulu vizuri wanafunzi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kwamba skuli ya Kiwengwa ni moja ya skuli ambazo zina matatizo makubwa ya ufundishaji na hili linasababishwa ama na kutokuwajibika, lakini vile vile inasababishwa na mgongano uliopo baina ya walimu pamoja na Kamati ya Skuli. Suala hili Wizara tayari imeshaliangalia na hatua tayari zimeshachukuliwa katika kurekebisha tatizo hilo, mimi mwenyewe nilifika katika skuli ya Kiwengwa na nikaiona hali hiyo na tayari wizara imeshachukua hatua ya kurekebisha hayo.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Naona tatizo lipo pale pale hajakosea kabisa katika somo la Kiingereza na Sekondari, kwa kweli shule za Sekondari hazina *dictionary* la *syllabus* wala *library*. Sasa sijui watatueleza vipi hapa jinsi gani walimu wataweza kusomesha bila ya kupata vitabu hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nilieleza kwenye jibu langu mama kwamba kweli bado tuna matatizo ya vitabu pamoja na mambo mengine mbali mbali ambayo yanapelekea uhaba au tatizo la kufundishwa vizuri. Tayari Wizara yangu imeshaliona tatizo hilo na hatua tumesema tumeshaanza kuchukua ikiwemo na kupitia upya mitaala na *syllabus* za masomo haya.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba baadhi ya maskuli yamekosa upungufu na kwa kuwa Skuli ya Mwambe ina upungufu wa zaidi walimu kumi na tano,

a) Je, anawapa ruhusa walimu wa Mwambe watafute walimu popote pale.

b) Kama hilo halikuwezekana atakuwa tayari skuli hiyo kuifunga.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, Wizara haikatazi kutafuta walimu ikiwa jamii itapata walimu ambao wana sifa ambazo zinafaa kufundisha katika masomo haya. Napenda nimuarifu tu Mhe. Waziri kama kweli anao walimu wenye sifa, basi Wizara itawapokea.

Kuhusu kuifunga skuli hiyo nadhani serikali pamoja na wizara haina nia ya kuifunga, lakini jitihada za kutafuta walimu bado zitakuwa zinaendelea na kuweza kuhakikisha kwamba masomo haya yanasomeshwa kama inavyohitajika.

Nam. 40

Ujenzi wa Hospitali Kubwa Nje ya Mji

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Kwa kuwa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa hospitali kubwa nje ya mji kimeshapatikana huko Binguni Wilaya ya kati. Na kwa kuwa suala la ujenzi wa hospitali hii ni muhimu sana kwa hivi sasa.

Mhe. Waziri, ni hatua zipi zaidi zilizokwisha kuchukuliwa ili kuona kwamba ujenzi huu unaanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 kama ifuatavyo. Mhe. Spika, ni kweli kuwa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa hospitali kubwa nje ya mji kimeshapatikana huko Binguni Wilaya ya Kati. Aidha, Wizara yangu inafahamu kuwa suala la ujenzi wa hospitali hii ni muhimu sana kwani kuweko kwake kutawasogezea wananchi huduma za Afya karibu na maeneo yao.

Mhe. Spika, hatua zilizokwisha kuchukuliwa hadi hivi sasa ni kuandaa michoro na kufanya makisio ambapo ujenzi wake umekisiwa kugharimu jumla ya dola za Kimarekani Millioni Thamanini (US$ 80,000,000). Kutokana na gharama kubwa ya ujenzi, Wizara yangu inaendelea kuwasiliana na washirika wetu mbali mbali wa maendeleo ili waweze kutusaidia, lakini hadi hivi sasa bado hatujafanikiwa.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Dhamira ya ujenzi huu iltokana na kauli kwamba katika ziara ya Makamo wa Rais wa Jamhuri za Falme za Kiarabu alipeleka ombi hilo la Zanzibar kupatiwa Hospitali, ndipo harakati za utafutaji wa eneo hilo ukaanza. Sasa Mhe. Waziri anatwambia sasa wanatafuta washirika wa kuchangia ujenzi huo.

a) Je, yule wa mwanzo ambae alitupa dhamiri hata ya kutafuta kiwanja ametoweka.

b) Mimi kama Mwakilishi suala hili katika kufuatilia kwa Mhe. Waziri niliambiwa linaratibwa na Mhe. Waziri Kiongozi. Je, hili ni sahihi hebu atutoe mashaka sisi wananchi wa Wilaya ya Kati.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, ni kweli ni sahihi yote aliyoyaeleza ni kwamba mradi huu ulikuwa umeombwa huko Abudhabi na sisi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tuliitwa tukalishughulikia jambo hili kwa kutayarisha michoro na kiwanda. Vile vile ni hakika kwamba hapa Unguja lilikuwa lipo chini ya Mhe. Waziri Kiongozi, lakini tulipokwenda huko kutokana na gharama kubwa hizo tulizozitaja bado suala hili halijapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa hii kutoa maelezo ya ziada. Nafikiri suala la Mhe. Haji Mkema mimi ndio mara yangu ya kwanza kulisikia kwamba hospitali hii ombi lake lilipelekwa kwa Makamo wa Rais kushughulikiwa. Mimi ndio mara yangu ya kwanza kusikia.

Lakini lililo kweli ni kwamba jambo hili lilianzia Afisi ya Waziri Kiongozi na mwaka juzi nilipata nafasi ya kuzungumza na balozi wa Falme za Kiarabu na nikamwambia kwamba kwenye eneo hilo la Binguni tunahitaji hospitali ya kisasa ambayo inaweza kuhudumia wananchi wa maeneo hayo na jirani.

Sasa kimsingi alikubali akanambia basi tayarisheni hilo ombi rasmi na tayarisheni mchoro kazi ambayo tuliifanya kwa ufanisi mkubwa. Sasa tulipokwenda kwake akanambia tumelipitia na serikali yangu bado inaendelea kulipitia na tumehisi kwamba gharama zake ni kubwa mno hatutaweza kuzitekeleza kwa haraka sana, kwa hivyo jambo hili tuachieni na tutizame namna na njia ambayo tunaweza kusaidia wakati mkifanya kazi hiyo endeleeni bado kutafuta wafadhili wengine.

Sasa ndio kazi hiyo ambayo ilisababisha tusikae tu na tunaifanya kwamba wao tumewaachia kwa upande wao, lakini hatukuwaachia wao tu tunaendelea kuzungumza na wafadhili wengine, ishaala kama atatokea mfadhili ambae yuko tayari kufanya hiyo kazi, basi tunaweza kumpa yeye badala ya hao wa awali walioonyesha nia ya kutusaidia. Kwa hivyo, narudia tena kusema hii ni mara yangu ya kwanza kusikia kwamba jambo hili lilitakiwa Afisi ya Makamo wa Rais, lakini nasema lililo kweli jambo hili limeanzia Afisi ya Waziri kiongozi kama hivyo ambavyo nimewaeleza waheshimiwa wajumbe.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Kwa kuwa hospitali ile inaelekea kama ni ya Wilaya ni kwa nini ikatayarishwa michoro ambayo ni ghali sana na tunajua katika ulimwengu watu wanaotoa fedha zaidi zilizokuwa hazina masharti makubwa ni hizi falme za kiarabu ikiwemo na Abudhabi.

c) Katika jibu lake lililopita Mhe. Waziri alijibu kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja ina msongamano mkubwa kwa sababu hakuna hospitali kati kati hapo, kwa nini wizara haianzishi jengo ili ikapunguza huo msongamano badala ya kusubiri wafadhili kila siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, nataka kusema hivi sisi wizara yetu nia hasa na madhumuni kuzijenga hospitali za Wilaya na hizo hospitali za Wilaya pamoja na vituo vyetu vya Afya vidogo vidogo vyote nia yetu kwanza ni kuviimarisha, tuimarishe vile vituo vidogo vidogo tuimarishe vile vituo cha sekondari halafu baadae tuimarishe *Cottage* ili huu msongamano wa Mnazi Mmoja hospitali uweze kupungua.

Sasa hii hata ikiwa inaonekana hospitali ya Wilaya, lakini ikiwa imepata ujengaji mzuri na ikapata vifaa vya kisasa na ikaweza kutoa huduma, huu msongamano wa Mnazi Mmoja hospitali unaweza kupungua, kwa hivyo nia yetu hasa ni kuboresha hizi huduma katika vijiji ili huu msongamano unaokuja katika hospitali yetu kubwa uweze kupungua hiyo ndio nia na madhumuni katika kuboresha afya katika Wizara yetu.

Mhe. Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo ya ziada kwa pale alipomalizia Mhe. Naibu Waziri. Namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa masuala yake mazuri sana.

Katika jambo ambalo halipendezi na hasa halipendezi kwa mtu aliye muungwana kama tulivyo sisi Wazanzibari, nafikiri hata dini yetu inakataza suala la kuwa omba omba si jambo zuri hata kidogo. Lakini wakati mwengine si kwa sababu tunapenda sana sisi kuomba, lakini wakati mwengine kuna mambo, mahitaji ya nchi yetu yanakuwa makubwa sana. Sasa tufanyeje, tuendelee tu kulalamika?

Mhe. Spika, kama kuna mtu yuko tayari kukusaidia basi si vibaya kuomba msaada huo. Sisi kama tulivyosema ni kweli hospitali hii inayotaka kujengwa ina gharama, lakini hayo ndio mahitaji ya kileo ya hospitali.

Hospitali hii inayojengwa leo inawezekana ikaonekana ni hospitali ya wilaya, lakini nchi yetu inakua, mahitaji yake yanakua kesho na keshokutwa, sasa ni lazima tunapofanya mambo yetu tufikirie leo, kesho na keshokutwa. Kwa sababu unaweza kuijenga hospitali ya leo kwa ajili ya hospitali ya wilaya, halafu baada ya miaka mitano ukaanza kufikiria ukaona mahitaji yake pengine yanahitajika yawe ya hospitali ya mkoa. Sasa kila wakati utakuwa kazi yako kujenga tu na kubomoa jambo ambalo lina gharama kubwa sana.

Nikirudia pale mwanzo ni kwamba hatupendi sana kuomba na kwa maana hiyo mimi ninaamini wako Wazanzibari ambao Mwenyezi Mungu kawajaalia sana ndani na nje ya nchi *Alhamdulillah* fedha wanazo. Sasa badala ya kukimbilia huko kwa wafadhili hawa ndugu zetu Wazanzibari basi tunawakaribisha wenye moyo wa kutaka kuisaidia nchi yao, tuko tayari kushirikiana nao kwa hali na mali.

Nam. 32

Ufungwaji wa Visima vya Maji, Kijitoupele

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Katika maeneo ya Kijitoupele, kulikuwa na visima vikubwa vya maji safi ambavyo vilisambaza maji safi kwa wananchi wa eneo hilo na maeneo ya jirani ikiwa ni pamoja na maeneo ya mjini.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa kuzingatia faida ya huduma ya maji safi iliyokuwa inapatikana kwa wananchi wetu, Je, kuna sababu zipi za msingi zilizopelekea kufungwa kwa visima hivi.

(b) Kwa kuvifunga visima hivyo, Wizara yako haioni kwamba ni hasara ukizingatia fedha nyingi zilizotumika katika kuvianzisha na kuvitengeneza.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake Nam. 32 lenye vifungu na(b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, visima vya maji vilivyochimbwa katika maeneo ya Kijitoupele ambavyo vilikuwa vikisaida maeneo ya jirani, Fuoni na Meli Nne vilisita kutoa huduma kutokana na kupunguwa kwa wingi wa maji.

(b) Wizara yangu bado ni mmiliki wa maeneo hayo ya visima na hasa kwa vile gharama kubwa zimetumika wakati wa kuchimba na kuvijengwa visima hivyo. Wizara imepanga kufunga *pump* ndogo itakayokidhi uwezo wa kisima ili kusaidia maeneo ya jirani yakiwemo ya Mkoroshoni.

Hata hivyo, kutokana na kupungua kwa maji katika Kituo cha Kijitoupele, Mamlaka ya Maji imechimba kisima chengine maeneo ya Kwarara ambacho hivi karibuni kitamalizika na kuanza kutoa huduma na kitasaidia sana kupunguza tatizo la maji katika maeneo hayo.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mara nyingi kwenye vianzio vya maji kama vile visima, huwa na upungufu wa maji kwa kuvamiwa maeneo hayo kwa kujengwa nyumba, kukatwa miti ovyo au kuharibu mazingira.

Je, Mhe. Waziri amejipanga vipi katika kusimamia kisima cha Chunga, Mwembe Mchomeke ili visima hivi visivamiwe kwa kujengwa majumba, kukata miti na kuharibu mazingira ili kuepusha kuja kutokea matatizo kama yaliyotokea Kijitoupele kufungwa visima hivi.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ni kweli maeneo mengi ya vyanzo vya maji hutokezea yakapungua kwa kuharibu mazingira ya maeneo hayo ikiwemo kukata miti na kujenga karibu na maeneo hayo kama ambavyo imetokezea hapo Kijitoupele.

Mhe. Spika, ni kweli kuna kila sababu na haja ya kuanzisha maeneo ya Chunga na Mwembe Mchomeke na mengine yote ambayo yana vianzio vya maji basi sote kwa pamoja Wawakilishi, Wabunge, Masheha na wananchi tushirikiane kuhakikisha kwamba hatujengi katika maeneo hayo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu a, b na c.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu ametueleza kwamba visima vilivyokuwepo Kijitoupele vimekuwa na upungufu wa maji na ndio maana visima vile vimekuwa havikushughulikiwa. Lakini Mhe. Waziri kuna kisima ambacho kina maji mengi na kimeharibika kwa muda mrefu sasa katika Shehia ya Kizimbani Jimbo la Dole.

(a) Je, suala hili wizara yako inalijua.
(b) Kama inalijua ni kwa nini wizara yako imekiacha kisima hiki kwa muda mrefu bila ya kukifanyia matengenezo na kuwaacha wananchi

wa Shehia ile wakitangatanga kuhangaika maji safi na salama. Kama jambo hili Mhe. Naibu Waziri hulijui ni kwa nini hulijui wakati maharibiko haya ni ya muda mrefu.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ni kweli Kizimbani kiko kisima hicho ambacho kwa sasa hivi hakifanyi kazi na ni kweli kuwa ni muda mrefu. Naomba niseme kwa pamoja kwamba hivi sasa tumo katika jitihada za kuchimba kisima chengine ambacho tayari kimeshachimbwa na tunategemea muda mfupi ujao tutaweka *pump* pale ili kupunguza tatizo hilo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wataalamu wanatwambia kwamba visima vinapokaa muda mrefu bila ya kutumika ndio sababu kubwa ya kupungua kwa maji. Je, Mhe. Naibu Waziri kiutaalamu analijua hilo.

Vile vile ni kwa nini inaruhusu basi *pump* ziharibike na visima kukaa muda mrefu na matokeo yake huwa visima vile haviwezi tena kuzalisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, inawezekana kwa visima vyetu hivi vya makalbi vinapokaa muda mrefu bila ya kutumika huwa vinafukilika, taka zinaingia, lakini kwa visima vyetu vya kileo ambavyo vinatumia ***submersible pump*** kwa kweli huwa haviathiriki kiasi hicho vinapokuwa havitumiki. Inapotokezea tu inapokuwa tayari kuja kukitumia ni kukifanyia *flashing* upya ili kiweze kutumika.

Nam. 45

Mahkama ya Kadhi

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza**:-**

Serikali imeanzisha Mahkama ya Kadhi kwa madhumuni ya kusikiliza na hatimae kutoa hukumu juu ya kesi mbali mbali zinazowasilishwa Mahkamani hapo kwa Waislamu.

(a) Je, Mhe. Waziri kunatofauti zipi za kimaslahi kati ya Kadhi wa Wilaya anayehukumu kesi za Waislamu, na yule Hakimu wa Wilaya anayehukumu kesi za kawaida.

(b) Ni utaratibu upi unatumika katika kusikiliza kesi ya rufaa baada ya mshitakiwa kutoridhika na hukumu iliyotolewa na Naibu Kadhi Mkuu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe, Spika, kabla ya kutoa majibu ya msingi, ninaomba kutoa maelezo mafupi kwamba Mahkama za Kadhi zilianzishwa rasmi kwa Sheria Nam. 3 ya mwaka 1985. Mahkama hizo zilianzishwa katika ngazi za Wilaya na Mahakama ya Kadhi Mkuu ambayo ni Rufaa. Kwa mujibu wa sheria hiyo Mahkama hizo zilikuwa na uwezo wa kusikilisha kesi kwa mambo yanayohusiana na
na ndoa, talaka, mirathi na uhalali wa mtoto.

Baadae sheria hiyo iliunda Mahkama za Kadhi iliyofanyiwa mapitio kwa Sheria Nam. 4 ya mwaka 2003 ambapo marekebisho kadhaa yalifanyika ikiwa pamoja na kuongeza mamlaka ya Mahkama za Kadhi katika kusikilisha kesi. Hivi sasa zina uwezo wa kusikiliza na kuamua mashauri yanayohusiana na uhalali wa mtoto, ndoa, talaka, haki ya kulea na kuishi na mtoto, kesi za wakf, masuala ya sadaka za kidini, hiba, mirathi na madai ya matunzo iwapo dai halizidi Shs. 500,000/= au Shs. 50,000/= kwa mwezi. Sharti kuu la kesi hizo ni kusikilizwa katika Mahkama za Kadhi ambapo wahusika wote watakuwa ni Waislamu.

Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe, Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Kulingana na muundo wa mishahara serikali hivi sasa tofauti iliyokuwepo ya kimaslahi kati ya Kadhi wa Wilaya na Hakimu wa Wilaya ni kwamba Hakimu wa Wilaya ambaye ndiye kwanza ameajiriwa anapata mshahara mkubwa kuliko Kadhi wa Wilaya. Hii inatokana na uzito wa kazi na majukumu yanayotofautiana kati yao kwa mujibu wa *scheme of service*, na wakati mwengine inatokana na tofauti ya kiwango cha taaluma *(Formal education)* kinachotakiwa kwa kazi hizo.

(b) Iwapo hukumu imetolewa na Naibu Kadhi Mkuu na kuna upande haukuridhika na hukumu hiyo, upande usioridhika una haki ya kukata rufaa Mahakama Kuu ya Zanzibar ambayo kwa mujibu wa sheria uamuzi wake ni wa mwisho na hauwezi kukatiwa rufaa Mahakama nyengine.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa mahakimu wa ngazi zote ndio tunaowategemea kutoa haki au hukumu za

haki kwa wananchi wetu, na kwa kuwa mishahara ya mahakimu ni midogo mno ukilinganisha na majukumu tuliowapa.

Je, Mhe. Waziri huoni kuwalipa mishahara midogo mahakimu kunaweza kuleta matatizo katika suala zima la utoaji wa haki ikiwa ni pamoja na kutofanya kazi zao kwa moyo mkunjufu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, nikubaliane kama ukitoa mshahara mdogo kwa hakimu anaweza akafanya varange za aina nyengine. Lakini nimpe taarifa tu kwamba mishahara ya mahakimu imerekebishwa hivi karibuni tu na hiyo nafikiri hana habari nayo.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali matatu ya nyongeza.

La kwanza naomba nimuulize Mhe. Waziri je, kuna vigezo vyovyote ambavyo vinatumika kati ya vile vinane vilioko katika sheria ya makadhi ili kuwapata hawa makadhi.

Pili ikiwa vipo inakuwaje mpaka kadhi akatoa maamuzi yakisikilikana na Waislamu anaonekana kama hana hata sifa moja miongoni mwa zaidi ya sifa nane.

Tatu kwa kuwa suala la kadhi ni suala linaloendana na misingi ya Dini Tukufu ya Kiislamu. Je, pale kadhi anapohukumu au kutoa maamuzi ambayo hayafanani na kadhi yanafanana na kazi sijui wizara inachukua hatua gani.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, vipo vigezo vinavyotumika kwa ajili ya mtu kuteuliwa kuwa kadhi. Kwanza awe ni Muislam, pili awe na elimu ya Sheria ya Kiislamu ambapo kwa maoni ya Tume ya Utumishi wa Mahkama itamfanya aweze kuchaguliwa kuwa kadhi.

Tatu awe amepata elimu ya Sheria ya Kiislamu katika vyuo ambavyo vitakubalika na Baraza la Maulamaa ambalo limeundwa kwa mujibu wa sheria ya Mufti ya mwaka 2001 na amepata sifa za kuwa na elimu hiyo kwa muda usiopungua miaka saba na uzoefu wa shughuli zenye kuhusu Sheria ya Kiislamu. Hivyo ndivyo vigezo vinavyotumika.

Suala la pili kwa nini huwa anatoa maamuzi ambayo Waislamu huwa wanalalamikia. Mhe. Spika, katika hoja za kidini watu wana tafsiri nyingi sana kila mtu na aliposoma. Kwa hivyo, kweli hata akitoa maamuzi wengine watalalamika hili wengine lile, ni mambo ya kawaida. Majibizano kwenye masuala haya yanaendelea kuwepo siku hadi siku. Lakini anaposema kwamba

maamuzi mbona yanakuwa yanafanana na kazi na hayafanani na kadhi. Sasa hilo ni suala jengine.

Suala hili lazima afisi yangu au Afisi ya Mahkama isaidiwe kutoka kwa wale wanaoathitika na masuala kama haya ili iweze kuwashughulikia makadhi hao. Tume ya Utumishi ya Mahkama ipo na inaweza kuwashughulikia watu wa namna hiyo.

Mhe. Haji Faki Shaali: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye (a), (b) na (c).

Kwa kuwa mfumo wa Mahkama ya Zanzibar ni *Parallel Court System* unaoitambua Mahkama ya Kadhi na Mahkama hizi za kidunia. Kwa kuwa Kadhi Mkuu huteuliwa chini ya kifungu cha 4 na *Senior* Kadhi huteuliwa chini ya kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Kadhi ya mwaka 1985.

(a) Je, hadhi ya Kadhi Mkuu na *Senior* Kadhi ni sawa na hadhi ya Mahakimu wa ngazi gani katika hizi Mahakama za kidunia.

(b) Mahkama ya Kadhi Mkuu kwa mujibu wa sheria chini ya kifungu cha 10 (1) haina *Original Jurisdiction* na *Original Jurisdiction* yote imewekwa katika Mahkama za Wilayani. Lakini kwa kuwa makosa yanapitana kuna makubwa na madogo. Je, huoni kwamba kuna upungufu wa kuinyima Mahkama Kuu *Original Jurisdiction* hasa ukizingatia kwamba kuna Mahkama Kuu yenye *Appellant Jurisdiction*.

(c) Je, ikitokea katika Mahkama Kuu Majaji wote waliopo si Waislamu na ndiko zinakosikilizwa rufaa zinazotoka kwa Kadhi Mkuu, ikiwa hukumu itayotoka pale haidhuru atashauriwa na washauri Waislam, lakini ikiwa hukumu itakayotolewa haiwafurahishi Waislamu. Je, huoni hapa itaonekana kuna kasoro katika hii *Parallel Court System* yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, Mhe. Haji Faki Shaali ananambia niende chuoni. (*Kicheko*)

Mhe. Spika, kwanza ameulizia habari ya Kadhi hadhi yao baina ya Kadhi Mkuu na Makadhi wa Wilaya na Mahakimu. Nimesema kwamba hii imo katika *Scheme of Service* yao ambao ndio inayoamua zile kazi zao, lakini Kadhi Mkuu anajulikana kuwa ni mtu ambaye anasikiliza rufaa na makadhi wa wilaya wanasikiliza kesi katika maeneo yale walioko katika wilaya zao na sehemu mbali mbali.

Halafu amezungumzia suala la *jurisdiction* kwamba Mahkama Kuu haina hiyo *jurisdiction.* Nafikiri hiyo ndio sababu wakawa wanawekwa washauri wa pale wawe Waislamu wote. Kwa sababu kama nilivyosema mwanzo hoja katika Sheria za Kiislamu zina matatizo yake.

Sasa ukisema iwekwe kama tulivyoweka katika sheria zetu za kidunia hizi utapata matatizo, ni vizuri washauriane huko, wajadiliane mpaka wamalizane na ikibidi wameshindwa wao tena watakuja kuingia Maulamaa kufanya maamuzi na kutoa fatwa kwa sababu kuna fatwa katika Uislamu. Kwa hivyo hiyo ndio hali halisi iliyopo.

Swali la tatu alisema kwamba ikitokea majaji wote si Waislamu, lakini ndio maana wanawekewa washauri Waislami watafuata ushauri ule. Kwa hivyo, hapa pamoja na kuwa jaji katoa ile hukumu, lakini dhima kubwa inaanguka kwenye jaji lakini wale washauri aliokuwanao ndio wanaohusika na matatizo yale kwa nini wakamshauri vibaya yule. Ahsante sana.

Nam. 25

Uzalishaji wa Viungo

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza**:-**

Zanzibar ni Nchi yenye utajiri wa uzalishaji wa viungo mbali mbali (Spices) ambayo vinasafirishwa nje ya Nchi. Viungo vyenyewe ni Karafuu, Mdalasini, Hiliki, Kungumanga, Bizari/Manjano, Pilipili manga, pilipili kali na vyenginevyo. Wafanyabiashara husafirisha bidhaa hizo baada ya kununua kwa wakulima wadogo wadogo wa Unguja na Pemba.

(a) Je, Mhe. Waziri viungo hivi nilivyovitaja aghalabu huuzwa katika Nchi gani duniani.

(b) Kwa kuwa hivi sasa vijana wengi wamejitokeza katika ukulima huu wa viungo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia na inatoa wito gani kwao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira –Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, viungo hivi huuzwa zaidi katika Soko la Afrika ya Mashariki hususan nchi za Kenya na Tanzania Bara. Aidha, kuna Kampuni ya *TZOP*

ambayo hununua bidhaa hizo na kusafirisha nje ya nchi ikiwemo Ujerumani, lakini kwa kiwango kidogo tu huongezea Tanzania Bara. Kwa upande wa soko la karafuu na pilipili kichaa bado linamilikiwa na *ZSTC*.

Kamisheni ya Utafiti kwa Wakulima ikishirikiana na Wizara ya Biashara, Utalii na Uwekezaji inaandaa mafunzo ya uzalishaji, usarifu, ufugaji mzuri wa bidhaa hizo pamoja na mbinu bora za uendelezaji wa sekta ya Utalii (*spice tour)* hapa nchini. Hivyo, vijana hawana budi kutumia mbinu bora za kilimo na kufuata ushauri wa kitaalamu ili kuongeza uzalishaji na kuimarisha ubora wa bidhaa hizo ili waingie katika ushindani katika masoko ya nje na kuimarisha Sekta ya Utalii nchini.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. hivi sasa vijana wengi hasa katika jimbo langu eneo la Kijichi, Mndo, Mkanyageni, Mbuzini na Kitundu wamejikusanya wanalima viungo na kuwauzia watalii. Je, kama wizara itatoa msaada gani kwa vijana kama hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza nakubaliana kwamba vijana wengi wa jimbo la Mfenesini na Dole wana *spice* nyingi. Moja katika msaada tunaotoa pale mara nyingi tunapopata wageni pamoja na watalii karibuni wote wanafika katika maeneo yale na kununua viungo vile. Lakini pia sasa hivi wizara inategemea sana kupata wafadhili kutoka Korea ambao watajenga kiwanda pale pale Kizimbani kwa ajili ya kusarifu mambo yafuatayo:-

Suala la samaki, maziwa na matunda mengine yote ambayo yatalimwa katika eneo hilo. Kwa hivyo, tunategemea kiwanda hiki mara tu kitapojengwa na kuanza kazi zake vijana wa jimbo lake na majimbo mengine yote pamoja na kule Pemba watafaidika sana na kiwanda hiki na tatizo hili la kusarifu mazao na kupeleka nje ya nchi litamalizika.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza linalohusiana na ulimaji wa viungo. Kwa sababu wananchi wa Jimbo la Gando wanalima sana viungo, lakini tatizo kubwa ni soko na bei. Je, wizara yake ina mpango gani wa kuona kwamba wakulima wa midalasini, pilipili manga na vyengine bei wanayouza inakidhi mahitaji yao. Kwa sababu karibuni kumeonekana kwamba watu wengi wamelima, lakini bei zao ni ndogo na wamevunjika moyo. Sasa wizara ina mpango gani wa kuona kwamba inaratibu na kuangalia kwamba bei wanayopata inalingana na jasho jingi wanalolitoa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, mimi namwomba Mheshimiwa awe na ustahamilivu kwanza mpaka pale wafadhili watapotupatia hiki kiwanda, kikipatikana kiwanda nafikiri tatizo hili litamalizika kwa sababu tutakuwa na masoko mengi ya nje.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika bajeti ya serikali ya mwaka huu kaulimbiu yake ni kupeleka miundombinu ya kilimo na utalii. Kwa kuwa katika kilimo ambacho kinasafirishwa nje kwa hapa Zanzibar ikiwemo pilipili kali.

Je, Mhe. Naibu Waziri atapeleka miundombinu gani kwa wakulima wa pilipili hasa akizingatia kwamba pilipili hizi zinalimwa katika ardhi ya maweni.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, moja katika jambo kubwa ambalo tutalichukua katika wizara yetu ni kuendeleza kutoa taaluma kwa wakulima hawa wa pilipili katika sehemu za maweni ikiwemo Matemwe, Jambiani na sehemu nyenginezo kama ilivyo kawaida yetu.

Nam. 42

Wizi wa Mishahara

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Kwa kuwa wafanyakazi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi wapatao 15 wameshukiwa katika wizi wa mishahara ya wafanyakazi na kwa kuwa wafanyakazi hao kwa muda mrefu wamesimamishwa kazi, na kwa kuwa uchunguzi wa Kipolisi hauonyeshi chochote juu ya kuhusika kwa wafanyakazi hao na wizi huo.

(a) Mhe. Waziri huoni kwamba kuendelea kuwasimamisha kazi wafanyakazi hawa ni kuwakosesha haki zao.
(b) Ikiwa wafanyakazi hawa hawahusiki na wizi huo ni nani hasa anayehusika.
(c) Nini hatma ya wafanyakazi waliokosa mishahara yao iliyoibiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimechukua hatua ya kuwasimamisha kazi wafanyakazi hao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi za Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, serikali inasubiri matokeo ya upelelezi na uamuzi wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka juu ya suala hili kwani hii ni kesi ya Jinai. Hivyo, kuwasimamisha kazi wafanyakazi hawa sio kuwakosesha haki zao bali ni utaratibu uliowekwa na sheria.

(b) Wizara yangu haitaweza kujuwa ni nani hasa wanaohusika na wizi huo mpaka hapo Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai kwa kushirikiana na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka itakapowasilisha kesi Mahkamani na kutolewa maamuzi.

(c) Mhe. Spika, kutokana na tatizo hili lilivyojitokeza, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kilichukua hatua za dharura kupitia miradi ya idara hiyo kuweza kuwalipa fedha za mishahara wafanyakazi ambao walikuwa hawajapokea mishahara yao kwa siku ya tukio la wizi huo.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria kesi yoyote inayoripotiwa Mahakamani inatakiwa polisi wamalize upelelezi wao ndani ya miezi minne. Sasa kwa kuwa miezi minne sasa imepita tangu lilipotokea tukio lile. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kuna haja ya kesi ile kuifuta na wale wafanyakazi akawarudisha.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, kwa kweli kazi hiyo inafanywa na Mahakama na sio Idara ya Zimamoto.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika jibu lake amesema kwamba yeye hawezi kufanya chochote kwa sababu ni masuala ya kisheria. Sasa ikiwa sheria hizo hizo baada ya kufanya kazi yake na ikagundua kwamba wafanyakazi hao hawakuhusika. Je, wamejipanga vipi kuwalipa fidia.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, kwa kweli maamuzi ya Mahakama ndio yatakayozingatiwa hapa zaidi kuliko maamuzi ya mtu mwengine. Kwa hivyo, ikiwa Mahakama imeamua kwa utaratibu wa Mahakama, kwa hiyo Idara ya Zimamoto itabidi iwajibike kufanya utatuzi huo kama ilivyotolewa na Mahakama.

Nam. 1

Kuanzishwa Maeneo Huru

Mhe. Ashura Abeid Faraji – Aliuliza:-

Kwa kuwa Micheweni Pemba kulianza kuchukuliwa hatua mbali mbali kwa lengo la kuifanya miongoni mwa maeneo huru ya kiuchumi.

Je, Mhe. Waziri suala hili limefikia wapi.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 1 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa katika eneo la Micheweni yametengwa maeneo kwa ajili ya uendelezaji wa Maeneo Huru ya Uchumi. Maeneo yenyewe yana ukubwa wa jumla ya hekta 808.8 ambapo kati ya hizo ni hekta 547.4 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya viwanda na maghala na hekta 261.4 zilizobaki ni kwa ajili ya ujenzi wa makaazi ya wafanyakazi wa miradi itakayoanzishwa.

Mhe. Spika, kwa kuwa uchumi sasa hivi una mwelekeo mwengine mpango huu huenda utabadilika. Hatua iliyofikiwa mpaka sasa ni kuyapima rasmi na kuyawekea mipaka (ya *beacons* na viguzo vya zege) ili yatambulike kirahisi. Vile vile yamefanywa makisio katika mwaka 2004 ya kupeleka huduma ya maji safi katika maeneo hayo na gharama ilikuwa ni Tsh. 967.0 Milioni kazi ambayo ilishindikana kutokana na ufinyu wa fedha. Hata hivyo, chini ya mradi wa *GP 5* eneo hili litapata maji kwenye mradi wa maji Micheweni ambayo itasaidiwa na *UNDP*.

Mhe. Spika, ni matumaini yetu kwamba kupatikana kwa umeme wa uhakika na kujengwa kwa mabarabara kisiwani Pemba ni hatua muhimu sana itakayowezesha kushajihisha wawekezaji kuanzisha miradi yao katika Maeneo Huru Micheweni.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna msemo wa wazee wanasema ‘sadaka huanza nyumbani’. Je, atakubaliana na mimi kama kuna haja ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanza kuwekeza yenyewe katika maeneo huru ya Micheweni. Wakaanza kujenga kiwanda cha kusindika samaki na kiwanda cha *tiles*.

(a) Je, anakubaliana na mimi baada ya kuanza kuwekeza wao na wawekezaji wengine watakuwa ni chachu ya kuja kuwekeza katika eneo lile la Micheweni.

(b) Je, anakubaliana na mimi kwamba kutokupeleka maji, umeme na barabara katika maeneo yale kunapunguza kutowawekeza wawekezaji katika maeneo yale.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, naomba nikubaliane nae na kama nilivyokubali katika jibu mama kwamba kutokuwepo kwa maji na umeme kisiwani Pemba hasa eneo la Micheweni ndiko kulikosababisha wawekezaji wasiwekeze kule.
Mhe. Spika, uwekezaji wa serikali kwa kiwanda cha *tiles* na samaki tutalifanyia kazi. Lakini nataka aelewe kwamba serikali haiwekezi yenyewe ila tutashajihisha wananchi wa Micheweni waje wasome kwa wenzao wananchi wa Bwejuu kuwekeza kiwanda cha *tiles*.

La pili tutajitahidi kama tulivyofanya kwa wenzao wa Nungwi kuweka mashine ndogo ya kukausha samaki ili wananchi wapate ajira pale.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Serikali ilitenga maeneo huru kwa makusudi kujikwamua kiuchumi, lakini inatimia mwaka wa 10 bado matunda yake hatujayaona dhahiri. Kwa sababu bajeti ya mwaka huu ni ya maendeleo ya utalii na miundo mbinu kwa kilimo. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba maeneo haya sasa tukayatumia kwa kilimo yakaandamana na bajeti hii.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi amependekeza kwamba maeneo haya yatumike kwa ajili ya kilimo. Kama ninavyoyajua maeneo haya kilimo kitakachoweza kulimika ni mahindi, mawele, mtama na mazao mengine kama hayo. Ikiwa serikali kwa pamoja au Baraza hili kwa pamoja litatoa kauli hiyo, basi mimi kama waziri wa wizara nitatekeleza maamuzi ya wengi.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, sababu kubwa ya maeneo huru nadhani ni kuzalisha kwa matumizi ya ndani na kupata ziada ya kusafirisha.

Kwa sababu eneo hili la Micheweni liko karibu kilomita 60 kutoka bandari ya Mkoani ambako ndio langu kuu la kusafirisha bidhaa kutoka Pemba. Je, uamuzi huu wa kuweka eneo huru umbali wa kiasi hicho ulikuwa sahihi. Mhe. Spika, Mhe. Waziri haoni kwamba ndio sababu inayofanya wawekezaji kuona kwamba itakuwa ni gharama kubwa ya kusafirisha bidhaa ya kisiwa cha Pemba kutokana na umbali wa lilipo eneo lenyewe.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ni kweli kwamba Micheweni iko mbali na Mkoani kilomita 60. Lakini kwenye barabara nzuri kilomita 60 sio kubwa. Kilomita 60 ni sawa na kutoka mjini kwenda Makunduchi na gari za abiria zinakwenda mara 3 kwa siku kwa hiyo sio mbali.

Lakini ukiangalia pia maumbile ya Pemba yalivyo, eneo pekee ambalo lilikuwa lina tambarare kubwa kwa eneo kubwa ni eneo la Micheweni. Kwa hivyo, nadhani serikali kwa wakati ule isingeweza kupata eneo jengine ambalo lina tambarare kubwa kwa pahali pamoja ukiangalia umbile la kisiwa chenyewe cha Pemba.

Nam. 15

Matengenezo kwa Gari za Serikali

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:-

Karakana Kuu ya Serikali, iliopo Chumbuni inafanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Pamoja na juhudi hizo matengenezo ya magari mengi ya serikali bado yanafanyika kwa mafundi binafsi.

Je, Mhe. Waziri, Wizara yako ina mkakati gani wa kuhakikisha magari yote ya serikali yanapelekwa katika karakana hii kwa matengenezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe Mwakilishi swali lake Nam. 15 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Ni kweli kwamba azma ya serikali ya kuanzisha Karakana Kuu ili kupunguza gharama za matengenezo ya magari ya serikali na pia kuangalia usalama wa magari hayo. Hata hivyo, kwa sababu mbali mbali kwa kipindi kirefu sasa magari mengi ya srikali yamekuwa yakitengenezwa katika gereji za watu binafsi hali ambayo inaleta hasara kubwa kwa serikali.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo :-

(a) Serikali kupitia Baraza la Mapinduzi limeshatoa waraka maalum kwa wizara zake zote kuzipeleka gari zao kutengenezwa katika Karakana Kuu iliyopo Chumbuni.

(b) Kwa kutambua umuhimu wa karakana hiyo serikali kupitia wizara yangu imepanga mikakati mipya ya kazi katika karakana hiyo ili kuinua viwango vya ujuzi wa mafundi, kuwapatia zana mpya za kisasa pamoja na uhifadhi wa eneo hilo kwa kujenga ukuta kazi ambayo imeanza.

(c) Kuunda kikosi kazi cha wizara ambacho kitapitia mahitaji halisi ya matengenezo hayo ya magari.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza niipongeze serikali kwa jitihada kubwa ya kununua magari mapya na tunaamini kwamba magari haya kama yatatunzwa vyema basi yatafika kwenye miaka 10 ili kuinusuru serikali kutoagizia gari nyengine.

Lakini kwa kuwa gari hizi huwa kila kikifika kipindi fulani au tarehe zilizopangiwa kufanyiwa service, ni wajibu kufanywa service ili ziishi kwa muda mrefu. Kwa kuwa kilio hicho kipo kwa baadhi ya madereva wanasema kwamba hizi gari toka kukabidhiwa baadhi ya madereva hazijafanyiwa service hadi hii leo. Je, wizara inatoa wito gani kwa wizara husika zilizopata magari hayo, kuanzia Waheshimiwa Mawaziri wenyewe mpaka maidara mbali mbali, ili kuhakikisha zinafanyiwa service kwa wakati na kuishi kwa muda mrefu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya kupatiwa gari mpya wamepewa maelekezo ya matumizi ya gari hizi. Kwa hivyo, ni matarajio yetu kwamba gari hizi na Makatibu Wakuu wanaelewa kwamba zinatakiwa zifanyiwe *service* kwa wakati na kama kuna kasoro badi tunatoa wito kwa wahusika gari hizo wazipeleke katika *service* kwa muda ambao upo ili kuzinusuru na maharibiko ambayo hayatarajiwi kutokea karibuni.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika maelezo yake ya mwanzo wakati wa kujibu swali mama alisema kuwa kwa sababu mbali mbali gari za serikali zilikuwa zinapelekwa kwa watu binafsi kutengenezwa. Je, ni sababu zipi hizo alizozikusudia zilizosababisha gari hizo zipelekwe kwa mafundi binafsi.

Swali (b) ikiwa sababu hizo ni uwezo mdogo wa karakana. Haioni serikali kuwa ilisababisha kwa makusudi gari hizi kupelekwa kwa mafundi binafsi.

Swali © ikiwa ni hivyo haionekani kuwa kuna uhusiano wa kimazungumzo na kimanufaa baina ya serikali na hawa mafundi binafsi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, Karakana Kuu ya Serikali ipo kwa muda mrefu kidogo lakini pia kuna na karakana nyengine za serikali kwa mfano Matrekta Mbweni na Chuo cha Karume Mbweni. Kwa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji walikuwa nayo *ZSTC* na Shirika la Magari. Lakini na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pia na wao walikuwa nayo karakana yao.

Sasa kuna ukweli ulio wazi kwamba vifaa ambavyo vipo karakana kuu kwa sasa havitoshelezi hili lazima tukiri. Lakini baada ya kuona serikali kwamba kuna umuhimu wa kuwa na karakana iliyo imara ndio ikaamua sasa kuifufua karakana yake na tayari tumeshaanza kufanya hatua za kuifufua. Baada ya kuanza hatua za kuifufua ndio tulipokubaliana kwamba sasa gari za serikali ziende pale Karakana Kuu.

Lakini kwa upande wa pili wa shilingi ni kwamba hata hizo gari za serikali zilikuwa zikienda pale wengi walikuwa wakishakutengenezewa wanachelewa kuyalipa madeni yao. Kwa hivyo, ukiwa hulipi ina maana unairudisha nyuma karakana ile kuendelea.

Mhe. Spika, lakini kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri pale suala la msingi ni kwamba sisi wizara tumeshajiandaa na tumeunda kamati yetu ya wataalam kupitia mahitaji halisi tutaimarisha karakana, tutapeleka mapendekezo yetu serikalini ili kazi zote ziende vizuri katika karakana ile.

Mhe. Spika, hili tatizo la watu kupeleka gari katika karakana za binafsi liondoke. Lakini kwa kipindi hiki cha mpito tumekubaliana sisi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba kama kutakuwa kuna ukosefu wa vifaa pale basi sisi tutawapa ruhusa waende katika karakana ya Chuo cha Karume kwa sababu na wao vifaa wanavyo.

Mhe. Spika, nafikiri kwa kipindi hiki tuko tayari kufanya kazi hizi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, kwa kuwa nchi yetu ya Zanzibar ina visiwa viwili Unguja na Pemba. Kwa kuwa Pemba Tibirinzi kuna karakana mfano kama iliyopo huku na kule kuna magari ya serikali.

Je, kuna mikakati ipi kwa magari ya serikali yaliyoko Pemba kupelekwa katika karakana ile ya Tibirinzi.

Je, kwa kuwa kuna vifaa ambavyo vimeshakufa kabisa kule Tibirinzi ambavyo vinahitaji matengenezo na huku mnafufua karakana. Je, kuna mpango upi wa makusudi kufufua na ile karakana iliyoko kule Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, karakana aliyosema Mhe. Subeit na hii ya Unguja zote ziko katika wizara yangu na zote ziko katika Idara ya Leseni. Kwa hivyo, tumelisikia ombi lake na kwamba tutaifufua nayo lakini kwanza tunaanza hii kuu ili tuweze kuwa na moja nzuri halafu tuendelee ya pili.

Mhe. Spika, nakumbuka kwa Pemba pia kuna karakana ya *ZSTC* Wete nafikiri bado iko hai tunaweza tukapeleka kwa muda gari zetu za serikali.

SHUGHULI ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Jana nilipanga nimalize wachangiaji wa kawaida ili leo tuwaite Waheshimiwa Mawaziri wawili watatu kusaidiana na Mhe. Waziri. Sasa nilibakisha kama wachangiaji wawili haraka haraka hebu tumalize.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa ni wa kijumla jumla hautokwenda kwa mafungu kama wengine walivyofanya. Unajua Mhe. Spika, duniani sasa hivi kuna mtikisiko wa kiuchumi. Nchi nyingi hasa kubwa zimekumbwa na mtikisiko huu wa kiuchumi ambapo sisi kwa wakati mwengine huwa ndio tunategemea kupata misaada kutoka kwao. Lakini nchi hizo hizo kubwa za dunia sasa hivi zimeanza nao kuwa na mtazamo wa kufuata mfumo mwengine labda wa kiuchumi. Mhe. Spika, nikisema hivi namaanisha kwamba hivi sasa duniani watu wanatazama kuanzisha mfumo wa mabenki ya kiislam. Hapa kwetu Zanzibar nimeshapata kuona au kusikia kwamba ziko benki hizi zinazoendana na mfumo wa kiislam.

Sasa kwa sababu chumi nyingi zinatetereka katika dunia pamoja na uchumi wetu. Hatuoni haja ya kwamba hivi sasa nchi yetu imeshafika wakati nao kuchungulia katika mfumo wa uchumi wa kiislam ili tuone unakwenda vipi. Huu utatusaidia kwa sababu ni uchumi ambao umeshapangwa na hauna matatizo. Kwa hivyo, tukifuata mfumo huu wa kiuchumi kama sasa hivi dunia

inavyoanza kutazama tazama na sisi tusiwe nyuma tutazame uchumi huu tuone utatupeleka wapi kiuchumi hasa kwa kipato cha wananchi wetu.

Mhe. Spika, wananchi wetu kipato chao ni kidogo, kwenda mabenki wakakopa wengi hawathubutu kwa sababu kuna mariba makali. Lakini tukiwa na mfumo huu wa chumi za kiislam na mabenki baadhi yao wakawa na vidirisha vyengine vya kutoa mikopo kwa mfumo wa kiislam, nadhani wananchi wataweza kukopa na wataweza kufaidika na mfumo huu wa kutokutozwa mariba makali makali.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nakuja katika biashara kwa ujumla. Mhe. Spika, biashara Zanzibar ni ini, ni kama chango la uzazi na mtoto, ni mwili na roho, ndio kitegemeo chetu toka asili. Lakini biashara Zanzibar sote tunajua kwamba imekufa. Imekufa si kama wafanyabiashara hawapo au si kama watu hawawezi kuja kuwekeza mambo makubwa makubwa hapa kwetu Zanzibar. Mhe. Spika, inakufa pengine kutokana na woga tulionao kama walivyosema wenzangu. Tuondoshe woga tulionao tufanye maamuzi ya kijasiri tuirudishe hali ya Zanzibar ilivyokuwa kibiashara ili nchi yetu iweze kuendelea. Haya mambo ya kumuogopa mtu naona yatatupeleka pabaya.

Mhe. Spika, sasa nizungumzie kilimo ambacho ndio huo uti mgongo unaosemwa. Lakini kama walivyosema wenzangu hatuwezi kwenda katika kilimo kama hiki tunachokwenda nacho sasa hivi ambacho ni kilimo cha kijembe kongoroka nitie mpini. Kilimo hiki hakiwezi kikatufikisha pahala inabidi tubadilike.

Mhe. Spika, kama bajeti hii imesema itaongeza fedha kwa ajili ya kilimo mimi bado naona hizi fedha ni ndogo zilizoongezwa hazitoshi. Kwa sababu wakulima wetu wengi sasa hivi wanalima vile vile kizamani, kizamani hatuwezi kupata mazao kama tunayoyategemea kwa kula sisi wenyewe na vile vile kututosheleza au kuuza baadae nchi za nje.
Mhe. Spika, jana katika televisheni nimeona Rais Jakaya Mrisho Kikwete alikuwa akizungumza na wakulima wakubwa wa mpunga walioko katika shamba fulani huko nimeshasahau wapi, wawekezaji wale wameingia pale katika nchi.

Sasa na sisi Zanzibar hatuna eneo kubwa. Lakini umefika wakati wa kuwashajihisha wafanyabiashara tulionao ndani ya nchi waje wawekeze katika masuala ya kilimo tena katika mambo mbali mbali, ikiwa chakula, ikiwa mazao ya kusafirisha. Hatuwezi kubakia hapa hapa lazima twende mbele.

Mhe. Spika, tukija katika uvuvi kwa sababu sisi ni watu wa bahari bado haujapewa nguvu kama tunavyotegemea. Kweli watu wamepewa vifaa vya

uvuvi lakini bado havijatosheleza na bado watu hawa hawawezi kwenda bahari kuu wakavua samaki ambao wameshaota ndevu hawajavuliwa hasa katika *Pemba channel. Pemba channel* kuna samaki wengi ambao bado hawajavuliwa kabisa toka siku waliyoumbwa wanakufa humo wanazaliwa wanapea lakini hawajavuliwa.

Sasa tuwashajihishe watu walioko nje walete meli za uvuvi ambazo zitasajiliwa Zanzibar ambapo tunategemea vijana wengi wa Kizanzibari watapata kazi. Vile vile itapelekea kujengwa viwanda vya kusindika samaki ambapo wanawake wengi humu watapata kazi na baadhi ya vijana wa kiume. Hii itapelekea uchumi wa wananchi kukua na uchumi wa serikali vile vile kukua tusibakie hapa hapa tulipo.

Lakini inasemekana hivi karibuni Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje alitia saini na Serikali ya Kenya juu a ulinzi wa Bahari Kuu kwa hizi meli zinazoingia na kuvua samaki katika bahari hizi. Mhe. Spika, mimi hapo kidogo napata wasi wasi kwa sababu Kenya najua imepakana na bahari yetu ya Zanzibar. Sijui suala hili sisi Zanzibar tunalijua kiasi gani kwa sababu hii pia na sisi ni bahari yetu, kweli ni mipaka ya Tanzania lakini kuna mipaka ya Zanzibar. Je, sisi katika utiaji huu wa saini wa ulinzi wa bahari kuu juu ya uvuvi wa samaki tunalijua vipi au tumeshirikishwa kiasi gani kuona kwamba na sisi hii rasilimali kwa sababu ni yetu nasi tunailinda.

Mhe. Spika, mimi niko hapa, kitu maadam ni chetu tusitake mwamvuli wa mtu, mwamvuli wa mtu ukitoboka turoe au tupigwe na jua. Ndio hivi tunavyopigwa na jua sasa na tunaroa kwa sababu ya kutegemea miamvuli ya watu. Mhe. Spika, naiomba Serikali ya Zanzibar iondokane na kukaa chini ya mwamvuli wa mtu ‘mtegemea cha ndugu hufa masikini’.

Mhe. Spika, wengi wamesema kwamba Zanzibar ni nchi iliyojaaliwa na mambo mazuri tu, ardhi yetu nzuri japo ndogo, bahari yetu nzuri na ina samaki wengi na haina madharuba mengi ya kukatisha tamaa, ikitokea ni Mwenyezi Mungu alivyopanga. Lakini bado hatujatumia rasilimali hizi kama inavyopasa. Mhe.Spika, mimi naomba kabla hatujenda huko nje kutafuta mambo mengine hizi rasilimali tulizonazo katika nchi za ardhi pamoja na uvuvi na hali ya hewa yetu nzuri tuitumie vizuri.

Mhe. Spika, ukija kwenye utalii naona unatuliza sasa. Kwa sababu mwanzo tulipoupokea utalii tulipokea tu lakini ulikuwa haujapangwa. Ingawa wizara inayohusika inajitahidi sana kutaka kupanga lakini bado kuna mapungufu ya hapa na pale yanataka kurekebishwa ili hawa wananchi basi wajihisi kwamba huu utalii nao ni wao.

Mhe. Spika, utalii kuchukua watu kutoka nje wakaja wakafanya kazi Zanzibar kama walivyosema wenzangu ya kuosha masufuria hii kwa kweli haipendezi wala haitusaidi. Mhe. Spika, bado tunasomesha watoto wetu wengi katika vyuo vya utalii lakini ukenda kwenye mahoteli mengi vijana wetu wao huwakuti na unakuta vijana wanaotoka nje ya Zanzibar. Sasa hii kiuchumi iwa ndani haitusaidii. Wakati fulani mimi niliuliza wale watalii wanaotoka nje *package tours* fedha zake tunazipata vipi sisi. Kwa hivyo, fedha hizi ni lazima zifuatiliwe na tujue tunazipata vipi na Zanzibar itafaidika lini kutokana na fedha hizi. Sasa kama watalii kila kitu wameshalipa kwao na hapa wanakuja kwa ajili ya kutembea tu na fedha hizi hazipatikani inavyotakiwa, basi bado haijatusaidia.

Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru kwa kunipa dakika 10. Isipokuwa namwomba Mhe. Waziri kuhusu miundombinu mibovu ya Pemba aitizame kwa jicho la huruma, kwa sababu na sisi tunahitaji kuichangia serikali kule Pemba. Lakini tunashindwa kuichangia kwa kiwango kikubwa kutokana na miundombinu mibovu ya Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Serikali. Kutokana na muda kuwa mdogo sana, nitajitahidi sana lakini kama nitatumia muda wako zaidi ya ulionipangia naomba univumilie.

Kwa kuanza mchango wangu moja kwa moja nizungumzie kuhusu nishati. Mhe. Spika, nadhani tunakumbuka katika Baraza lililopita suala hili la nishati lilizungumzwa kwa urefu sana, tena kwa pamoja Waheshimiwa Wawakilishi tuliomo humu tulipitisha kwa pamoja kwamba mafuta na gesi asilia pamoja na mambo mengine yanayotokana na hayo si ya Muungano.

Kwa bahati nzuri nimebahatika kukisoma kitabu hiki cha Mwelekeo wa Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa Mwaka 2009/2010. Katika ukurasa wa 26 kwenye Malengo kwa Mwaka 2009/2010 kwa Sekta hii ya Nishati kifungu 4 kimeeleza naomba kunukuu.

Ukurasa wa 26 kifungu cha 4 kinasema hivi:-

> "Kuratibu Ripoti ya Mshauri Mwelekezi kuhusu kugawana gharama za mapato yatokanayo na mafuta na gesi asilia"

Mhe. Spika, pengine sikufahamu hali halisi ilivyo, lakini kwa mujibu tulivyozungumza na tulivyopitisha kama ni maamuzi. Vile vile tulimtaka Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi atayarishe sera kwa haraka

inayohusiana na mambo haya na leo kukiona kifungu hiki cha maelezo. Hali hii inaonesha kuwa yale yote tuliyoyazungumza na kuyapitisha kama nilivyofahamu ndivyo, basi yalikuwa hayana maana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika kwa heshima kubwa na taadhima namwomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipe maelezo ya kutosha. Hivi ilikuwaje kikawepo kifungu hiki wakati Baraza lako tukufu tayari limeshapitisha maamuzi kinyume na utekelezaji wa shughuli za kifungu hiki, hilo ni moja.

La pili naomba nizungumzie kuhusu suala la Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, kama walivyozungumzia Waheshimiwa Wajumbe waliotangulia. Mhe. Spika, Kitambulicho hiki ni bora niseme kwamba ni kitu cha lazima tena ni haki ya kila raia wa nchi hii, baada ya kutimia umri pamoja na kukamilisha masharti mengine.

Wenzangu Waheshimiwa Wajumbe waliotangulia kuzungumza kila mmoja ametoa mfano katika jimbo lake. Mhe. Spika, kwa upande wangu naomba kusema kwamba ni kitu ambacho kimeshafanyika takriban katika majimbo yote 18 ya Kisiwa cha Pemba. Kutokana na hali hiyo hakuna jimbo hata moja ambalo wananchi waliotimia umri wa kupata vitambulisho na kupatiwa, isipokuwa wamekwenda kwa masheha na wananchi hao wakarejeshwa.

Pengine kuna mpango wa kufanywa ili mtu apate kipande cha kujiandikisha kupiga kura lazima awe na kitambulisho hicho. Lakini tukiachia hilo, kitambulicho hiki kinatumika kwa shughuli nyingi sana.

Kwa mfano, ukihitaji *Passport* ya kusafiria unaambiwa upeleke kitambulisho hiki, hata hawa wanafunzi waliomaliza masoma ya sekondari na wanataka kujiunga na masomo ya vyuo pamoja na mambo mengine yakiwemo vyeti vyao vya kuzaliwa, matokeo yao pia waliambiwa wapeleke Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Sasa ikiwa kuna njama yoyote iliyowekwa kwamba kukosekana kwa kitambulisho hiki kwa raia Mzanzibari mwenye sifa. Pengine kwa mtu anavyoona sijui ni vipi, yaani ungeliweza kufanikisha hivyo anavyofikiria, basi tujue kwamba kuna athari kubwa kabisa ya kuwakosesha watu haki zao.

Kwa sababu tunasema kwamba Zanzibar ni nchi yenye utawala bora na inapokosekana haki basi hakuna utawala bora. Mhe. Spika, imani yangu kwamba Masheha wasingekuwa na msimamo mmoja, lakini lazima kuna maelekezo au maagizo pamoja na kwamba watu wa juu hawajui kama

wanafanya hivyo. Kwa nini majimbo yote wafanye hivyo na wala hakuna jimbo hata moja ambalo wameandikishwa.

Kwa hivyo, wito wangu kwa serikali ni kwamba tunaishi kwa amani na usalama na *Alhamdullahi* tunafanyakazi vizuri. Hivi sasa tunaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010. Sasa raia wetu ambao wana vielelezo ambavyo havikamilishi katika sifa pengine ambayo itajitokeza ni pamoja na Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Kama kulikuwa na msimamo wowote, basi ni msimamo ambao utakaohatarisha amani ya Wazanzibari, kwa sababu hakuna mtu hata mmoja atakayekubali kukosesha haki yake.

Mhe. Spika, naomba kwa hili kama watapata nafasi ya kuzungumza, Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ watoe tamko rasmi, ili kama hapa katikati kulikuwa na mambo ambayo yamepangwa. Basi tuone kwa wananchi na watasikia kauli zao na kuona kuwa shughuli hii itafanyika kinyume na hivyo tulivyoiacha au tulipoondoka.

Vile vile hili ni suala la kutekelezwa kwa mapema kutokana na kuwa ndani ya mwezi huu pengine suala la la uandikishaji Pemba litaanza.

Jambo jengine Mhe. Spika, nimeona kwenye kitabu hiki kwenye Sera Mkakati katika Usafiri wa Baharini ni kwamba kuna matengenezo ya Bandari ya Wesha pamoja na Wete. Kwa kweli ni taarifa nzuri na Mwenyezi Mungu atujaalie hilo litekelezeke. Lakini Mhe. Spika, tusisahau kwamba Pemba tunayo Bandari ya Mkoani ndiyo kubwa kwa Kisiwa cha Pemba ambayo tunaitegemea.

Kwa kweli bandari hii tokea kipindi cha mwaka 2000/2005 tulikuwa tukipigia makelele kutokana na gati yake ilianza kudidimia karibu ya mwisho na kusababisha kutuwama kwa maji mengi sana sehemu ya katikati. Wataalamu waliopita walituambia kwamba haiwezekani kufanywa chochote mpaka gati ile iwe haididimii tena.

Lakini kila siku zikienda mbele athari inazidi kubwa sana na hivi sasa maji yaliyotuwama si ya kawaida, kwa sababu ya udogo wake na shughuli nyingi zilizopo na gari zinazokusanyika pale hata watu huwa hawana sehemu ya kupita.

Mhe. Spika, bandari ile kama tulivyosikia kwamba ilizungumzwa itakuwa ni Mlango wa Kimataifa. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwa vyovyote inatavyokuwa ile gati ishughulikiwe, ili wananchi waweze

kufanya shughuli za bandari ile katika hali ya kuridhisha. Vile vile itakuwa ni sehemu kubwa ya kuipatia mapato yatayokotokana na shughuli za bandari ile.

Suala jengine ambalo nataka kulizungumza ni kuhusu usafiri wa nchi kavu kwenye kitabu hiki alichokisoma Mhe. Waziri kwa ufasaha na kufahamika vizuri. Kwa kweli amezungumza barabara ambazo tayari zimeshatengenezwa, zinazotengenezwa pamoja na zile zinazofanyiwa marekebisho na kadhalika. Lakini kuna barabara tano za Mkoa wa Kaskazini Wilaya ya Wete ambazo hizi zimefadhiliwa na *Millennium Challenge Cooperation* humu hazikutajwa.

Mhe. Spika, kwenye kitabu cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo zimetajwa, lakini kwenye jadweli zimeandikwa tu hizi barabara kwa jumla, halafu *MCC* haikuoneshwa mchango au ruzuku ya serikali, mikopo wala wafadhili kama zilivyooneshwa kwenye sehemu nyengine. Kwa maana hiyo zipo, lakini hazina mpangilio maalum. Kwa hivyo, naomba kupata maelezo kuhusu barabara hizi, ambazo harakati zake za wanaohusika kuzipitia kila mara zimekuwa zikiendelea mpaka hivi karibuni. Lakini humu hazikuoneshwa namna gani zilivyotengenezwa.

Kwa bahati nzuri barabara hizi na barabara ya Mtambwe imo isije ikawa sababu ya kwamba imo barabara ya Mtambwe mle, ikawa tena mradi huu ukasahalika moja kwa moja *(Makofi)*.

Mhe. Spika, namwomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anipe kauli ya kuridhisha, ili wale watu waliokusanywa mara nyingi pamoja na watendaji wa *MCC* na kuwapa taarifa hizi na zile mpaka masuala ya kuajiriwa na kila kitu na leo hatuoni chochote kinachoendelea.

Mwisho mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Mtambwe tena kwa moyo na roho safi kabisa naiunga mkono Hotuba ya Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi) kama alivyoiwasilisha mbele yako *(Makofi)*.

Vile vile naishauri serikali kwa manufaa ya nchi yetu sehemu yake kubwa ichukuliwe, ili tuweze kukwamuka hapa tulipo *(Makofi)*.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nichukue fursa hii kwa kuchangia Bajeti ya Serikali ambayo imewasilisha na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi.

Awali ya yote na mimi nianze kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Chumbuni kuiunga mkono kwa asilimia mia moja bajeti hii. Kwa sababu Mhe. Mjumbe aliyetangulia alisema kwamba anaiunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri Kivuli. Sasa sijui matumizi yatakota kwenye bajeti ile aliyoiunga mkono, isipokuwa mimi naungako mkono hii yenye matumizi halisi *(Makofi)*.

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wa pande zote mbili tuunge mkono bajeti hii ambayo itatoa matumizi na wala tusiunge mkono bajeti ya Mhe. Waziri Kilivu ambayo itakuwa ndani ya kivuli haina matumzi. Sasa mimi kwa pamoja na wananchi wenzangu naona bora niunge mkono hii halisi.

Mhe. Spika, naunga mkono kwa sababu nyingi. Kwanza pamoja na hofu za baadhi ya Waehsimiwa pengine wa pande zote mbili kwamba bajeti hii ni tegemezi sana. Lakini kwa miaka karibu 9 ya Awamu ya Sita pamoja na Mawaziri mbali mbali wa Fedha ambao wameitumikia wizara hii, pamoja na kwamba tulikuwa tegemezi mambo yamekwenda vizuri hayajakwama.

Vile vile wamo Waheshimiwa Wajumbe wengine humu wametutangulia Barazani wanajua, kwamba hali ya uchumi inavyokwenda sivyo ilivyokuwa. Mhe. Spika, leo Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha ametudhihirishia kwamba hata wale wastaafu ambao wamekaa kwa muda mrefu, tayari wameshawamaliza, yaani wameshawalipa mafao yao *(Makofi)*.

Kwa hivyo, hivi sasa wanakwenda mwezi kwa mwezi baada ya ukakiki wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kuwalipa watu mafao yao. Kwa maana hiyo, hili ni moja la kulifurahia na kuiunga mkono serikali kwamba inafanya yale mambo inayowaahidi wananchi wake.

Mhe. Spika, kwa upande wa sisi Waheshimiwa Wajumbe kuna maendeleo makubwa majimboni mwetu katika Sekta za Umeme, Afya, Mawasiliano pamoja na Elimu, kwa hivyo haya nayo ni mafanikio. Kwa kweli nimefurahi kwamba Waheshimiwa Wajumbe wengi wameonesha kuridhika na utendaji wa serikali.

Kwa hivyo, nimatarajio yetu kwamba bajeti hii tutaipitisha, ili twende kama walivyosema wengi kuwa mwaka huu ni 2009 na mwakani ni 2010. Kwa hiyo lazima tutekeleze vizuri, ili mwakani 2010 twende kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo Waheshimiwa Wajumbe walilizungumza na mimi naliunga mkono na ninafikiri Mhe. Waziri ataliunga mkono. Kwa sababu Waheshimiwa wengi walizungumzia kuhusu mgawanyo sawa wa fedha za miradi midogo midogo. Kwa hivyo, suala hili ni zuri naona

kila jimbo wapate hata kama ni kidogo, lakini kila mmoja apate naye aonekane kwamba anafanyakazi.

Nikiondoka hapo nizungumzie kuhusu masuala ya barabara pamoja na mambo mengine yaliyoguswa katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Kwanza Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti) alizungumzia kuhusu barabara ya Pale Kiongele. Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba barabara hii imo kwenye mipango wa mwaka huu wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Vile vile barabara nyingi ambazo Waheshimiwa Wajumbe ambazo wamezitaja hapa, basi tutakaposoma Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano tutazieleza kwa kina.

Ninadhani si rahisi kwa Bajeti hii Kuu ya Serikali kwenda kwa kina kila wizara, kitabu cha Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi tusingeweza kukibeba, kwa sababu wizara ni nyingi pamoja na mambo yake.

Kwa hivyo, ameeleza kwa ufupi kuhusiana na wizara mbali mbali za serikali. Lakini kila sekta itakuja kueleza wenyewe na tutajibu maswali yanayotuhusu, ili kwenda mbele kama tulivyokusudia. Isipokuwa barabara ya Pale Kiongele tunatarajia kuijenga.

Vile vile Mhe. Haji Mkema Haji alisema kwamba bajeti haikutaja barabara ya Koani, Jumbi, Unguja Ukuu Uzi na Jendele Unguja Ukuu. Mhe. Spika, barabara ya Unguja Ukuu Uzi, hii ni barabara ni ndogo sana, lakini inahitaji utaalamu wa hali ya juu.

Kwa sababu kati ya Unguja Ukuu na Uzi kuna maji ya bahari, ili uweze kujenga unatakiwa utaalamu mpya au tunyanyue daraja ama *tunnel* za kupitia gari kama zilivyo nchi za wenzetu. Kwa kweli uwezo huu hatuna na wala hatujapata mfadhili wa kugharamia kipande kile cha kilomita karibu moja kwa gharama yake iliyokubwa.

Lakini kwa upande wa barabara ya Jumbi Koani na Jendele mpaka Unguja Ukuu tunafanya mazungumzo na *BADEA*, kwa ajili ya kuzichukua barabara hizi. Barabara hizi mwanzo zilikuwa zichukuliwe na MCC, baadaye MCC waliamua kwamba barabara watakazozishughulikia ni zile tano za Pemba tu.

Kwa hivyo, hizi za Unguja baada ya MCC kuziacha, Wizara ya Mawasiliano pamoja na serikali kwa ujumla tumeanza mazungumzo na *BADEA*, hata jana tulikuwa nao ili wazichukue hizi kwa ajili kutusaidia kwenye masuala ya matengenezo. Mhe. Spika, kama hatukufanikiwa huko basi tutatafuta wafadhili wengine au tutazijenga sisi wenyewe kwa kupitia fedha za serikali.

Vile vile Mhe. Said Khelef Ali pamoja na Mhe. Mkongwe Nassor Juma walizungumzia sana kuhusu barabara ya Bumbwini, lakini Mhe. Haji Mkema Haji alizungumzia kuhusu barabara ya Amani Dunga. Mhe. Spika pamoja na Waheshimiwa Wajumbe historia ya barabara hizi zilikuwa tatu, yaani kulikuwa na barabara ya Mfenesini Bumbwini, Amani Dunga, Mazizini Fumba pamoja na madaraja ya Donge Mkokotoni na Mwera.

Kazi hii ilitangazwa na alipewa mtu kujenga ninadhani mwaka 2006 au 2007. Kampuni ya *PRISMO* ndio iliyoshinda *tender* hii walianza ujenzi, lakini baadaye ikaonekana hawana uwezo wa kujenga, yaani mpaka kazi inakatishwa walikuwa wamefikia asilimia 16 ya ujenzi.

Sasa serikali ikaona kwamba ifanye juhudi kwa ajili ya kuzinusuru barabara hizi. Lakini barabara hizi lazima ifahamike kuwa ni ufadhili wake si *ADB*. Kwa hivyo, ulizungumza na *ADB* na walitukubalia kwamba barabara ambayo ilianza ya Mazizini Fumba SMZ iijenge, tena tulikubaliana kwamba tutaijenga kwa fedha zetu, lakini wao baadaye wagharamie Mfenesini na Amani.

Ninadhani hivi sasa sote tumeiona barabara ya Mazizini Fumba iko kwenye hatua nzuri, yaani karibu kilomita 13 kati ya 17 imeshawekwa kifusi na tunatajaria Mwenyezi Mungu akitujaalia mpaka mwezi wa 8 itakuwa imekwisha.

Mhe. Spika, kwa upande wa barabara ya Mfenesini Bumbwini na Amani Dunga tumeshatoa *tender* upya na kiasi ya kampuni kama 6 zimeomba *tender*, hivi sasa tayari tumeshafanya tathmini yake na tunatarajia kabla ya kusoma bajeti yetu tutakuwa tumeshamjua mjenzi ni nani. Kwa hivyo, tunatarajia sana tukipata mjenzi kipindi hiki basi tutawasiliana na *ADB*, tunategemea ndani ya miezi miwili mitatu ujenzi wa barabara utaanza.

Kwa awamu hii tumekubaliana kwamba barabara ya mwanzo ambayo tutaianza ni ya Mfenesini Bumbwini. Kwa hivyo, namwomba Mhe. Said Khelef Ali pamoja na Mhe. Mkongwe Nassor Juma wafahamu kwamba tutaanza, Mwenyezi Mungu akitujaalia bajeti ya mwaka huu barabara ya Bumbwini itaanza kujengwa kwa njia yoyote ile. Hapa ni Barazani na *hansard* zitakuwepo mtajua kwamba sisi tumekusidia kujenga barabara hizi *(Makofi)*.

Suala jengine ninadhani alizungumza Mhe. Haji Mkema Haji kama si yeye naomba radhi kuhusu matengenezo madogo madogo ni yepi. Kwa kweli matengenezo madogo madogo tumefanya Unguja na Pemba kama vile kutia viraka sehemu mbali mbali pamoja na *overlay*.

Matengenezo haya tumefanya katika maeneo tofauti kwa upande wa Unguja Mkoa wa Mji Magharibi, Mkoa wa Kaskazini, Mkoa wa Kusini na kwa upande wa Pemba tumefanya kwenye maeneo ya Mji wa Chake Chake. Kwa hivyo, haya yanaendelea na hizi ni kazi za kawaida za serikali.

Mhe. Rashid Seif Suleiman alizungumzia kuhusu mizani ya barabarani, kwamba lini Zanzibar itakuwa na mizani. Kwa kweli ni suala zuri la kuwa na mizani na ushauri wake kwa bahati nzuri wakati anauleta yeye na sisi tumeshauona. Hivi sasa tayari tumeshazungumza na wenzetu wa Mfuko wa Barabara na tunajiandaa kutafuta fedha za kununulia mizani. Inawezekana tusianze na mingi, lakini angalau moja tutatafuta eneo ambalo lazima gari ipite kwa ajili ya kupima uwezo wa gari ambazo zinaingia nchini.

Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii ya kumpongeza Mhe. Asha Moh'd Hilal kwa kupata ushindi wa kishindo na kuingia kwenye Baraza hili la Wawakilishi, kwa ajili ya kumalizia kazi aliyoiacha marehemu Mhe. Daud Hassan Daud. Namwomba Mwenyezi Mungu amjalie awe na uwezo wa kufanyakazi kwa bidii, ili awatumikie vyema wananchi wake wa Jimbo la Magogoni.

Mhe. Mjumbe alikuwa na mambo kama matatu au manne. Kwanza alizungumzia kuhusu uwanja wa ndege katika suala la *runway* ijengwe. Kwa hivyo, nataka nimhakikishie kwamba *runway* itajengwa mwaka huu na kampuni imeshaanza kuleta vifaa vyake ambayo ni Kampuni ya *Sogeya Satom* ya Ufaransa. Matarajio yetu ni kwamba kazi itakwenda vizuri na makubaliano yetu ilikuwa ni miezi 15, lakini tunawaomba ikiwezekana kabla ya miezi 15 itakuwa vizuri zaidi.

Katika makubaliano hayo ambapo mfadhili mkuu ni *World Bank*, tumekubaliana kwa upande wa uzio Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio. Kwa hiyo, watatusaidia *runway* na pia tutajenga uzio wa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar.

Vile vile alizungumzia kuhusu matengenezo ya barabara ya Amani Mtoni kwa awamu ya pili. Mhe. Spika pamoja na Waheshimiwa Wajumbe, ni kweli kwamba Rais Mstaafu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Benjamin William Mkapa, wakati wa ufunguzi wa barabara ile aliahidi kwamba ataendelea kusaidia kwa upande wa pili.

Kwa hivyo, serikali kupitia Afisi ya Waziri Kiongozi pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, tumefanya mawasiliano na wenzetu Bara. Kwa bahati nzuri kiasi miezi miwili iliyopita alikuja mtaalamu wa miundombinu alikuja kuiangalia mwenyewe ile barabara. Kwa maana hiyo, tunajua hatua zinaendelea kuchukuliwa, matarajio yetu ni kwamba barabara ile itajengwa upande wapili *(Makofi)*.

Mhe. Spika, pia Mhe. Mjumbe alizungumzia kuhusu barabara ya Kinuni kwa zile sehemu mbaya tukaweke kifusi na ikiwezekana kwa baadhi ya sehemu kutie lami. Ninamuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba tutashirikiana nae kazi hiyo tutaifanya, kwa sababu tumeshawahi kuifanya huko nyuma, lakini tutarudi tena kwa ajili ya kuangalia sehemu mbaya, ili kuweza kusaidia shughuli hiyo.
Vile vile Mhe. Said Khelef Ali alizungumzia katika barabara ya Bumbwini matengenezo ambayo tuliyokubaliana kuyafanya tumeanza Makoba mpaka Misufini. Lakini tumefanya hivi kwa makubaliano yao wenyewe na fedha zimemalizikia pale. Kwa hivyo, ni vyema kama tuje huku sasa, sisi tutaenedelea kuomba fedha na tukizipa hatuna tatizo la kutoka Misufini mpaka Mangapwani kweli ni sehemu mbaya sana.

Kwa maana hiyo, namwahidi Mhe. Mwakilishi tuendelee kushirikiana kama tulivyoshirikiana kwenye awamu ya kwanza, ili tuweze kuendelea mbele wakati tunakisubiri ujenzi wa barabara kuu. Kwa hiyo, asiwe na wasi wasi na tumekusudia kuwatengenezea wananchi wa Makoba, Bumbwini, Mangapwani, Fujoni wote wanufaike na barabara hizi.

Mhe. Haji Faki Shaali alikuwa na hoja kwamba mbona barabara ya Mshelishelini Pwani Mchangani inajengwa wakati kwenye kitabu imetengewe shilingi milioni 80. Kweli tulikuwa na shilingi milioni 80, lakini kwa mujibu wa utendaji wa serikali, kwa mfano sisi bajeti ya wizara nzima pengine haikufika hata asilimia 60.

Kwa hivyo, sisi kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi hatuzungumzi bajeti, yaani mamlaka ya mawaziri kuhaulisha kifungu kutoka sehemu moja kwenda nyengine. Sasa kulikuwa na miradi ya barabara ambayo haikuanza kwa mfano barabara tatu za Pemba hazikuanza mwaka jana na kifungu chake kilikuwa na karibu shilingi milioni 850, barabara ya Pale Kiongole, Mpendae meli mbili.

Kwa kutokana na hali hiyo, tulihaulisha kifungu na kupeleka Mshelishelini Pwani Mchangani na Mwenyezi Mungu ametujaalia ujenzi wa barabara unakwenda vizuri, tunategemea mpaka mwezi Agosti mapema itamalizika. Tukimaliza tuna jukumu kwa zile barabara ambazo tuliziahirisha mwaka jana,

basi zitakuwemo kwenye bajeti ya mwaka huu ambayo itakayoanza kesho kutwa na tutakapoisoma mtaiona.

Mhe. Spika, namwomba Mhe. Mjumbe asiwe na wasi wasi kwa hili na wala hakuna sababu ya kuleta *supplementary budget* hapa. Kwa sababu vifungu vyetu havijamalizika na tulikuwa na haki ya kuvihaulisha, kwa ajili ya kutumia matumizi ya serikali.

Kuhusu vifaa vya *MDR* Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshulikia Masuala ya Fedha na Uchumi atajibu yeye kwa ajili ya kulitoea ufafanuzi zaidi. Vile vile Mhe. Salmin Awadh Salmin amesema kwamba uwanja wa ndege uimarishe, kwa ajili ya kuongeza mapato. Suala hili tunalikubali kwa kweli ni jambo jema kwamba tukijenga uwanja wa ndege tutaongeza mapato pamoja na bandani.

Waheshimiwa Wajumbe Bandari ya Mpigaduri tunakwenda nayo, isipokuwa hatupendi kuitangaza haraka au mapema kwa sababu mambo mengine ukiyatangaza mapema yanaweza kukwama njiani, lakini tumefikia hatua kubwa kwa bandari hii. Kwa hivyo, ni vyema itoshe tu kwamba tunaendelea na mpango wa kujenga Bandari mpya ya Mpigaduri.

Mhe. Ali Denge Makame alizungumzia kuhusu *feeder roads* nazo ziangaliwe. Waheshimiwa Wajumbe ni jukumu lao kwa kushirikiana na Viongozi waliochaguliwa wa Majimbo kuzishughulikia *feeder roads*. Mhe. Spika, kwa hili naomba sana wakati mwengine tunazungumzia Mfuko wa Barabara kwamba fedha zake zinatumika vibaya.

Kwa kweli Mfuko wa Barabara fedha zake zinatumika vizuri sana na miongoni mwa watu waadilifu naweza kusema na wao wamo. Kwa sababu sisi wanapotupa fedha basi wanakuja kutukagua kwamba tumezitumia vipi.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe msiwe na hofu hata kidogo kwa watendaji wa Mfuko wa Barabara au Wizara yetu ya Mawasiliano na Uchukuzi, yaani wanatukagua tena sio kienyeji wanatuletea na *Auditors*, kwa ajili ya kukagua shughuli gani imefanyika.

Mhe. Spika, hili nataka nilichanganye na Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin, kweli barabara yake ya Mtambile/Pangani nilimwahidi kwamba tutakwenda kuvivunja kwanza vilima, kuweka kifusi, lakini tumeahirisha kwa sababu gani tunatarajia zile barabara tano za *NORAD* Pemba zitaanza karibuni sana, pengine mwezi wa Julai/Agosti utaanza ujenzi, na katika barabara za mwanzo kujengwa tutaanza na hiyo ya Mtambile/Kangani, Mtambile/Kengeja/Mwambe na barabara ya Wambaa tunategemea kwenda awamu mbili, lakini mwanzo hizo.

Sasa tumeona ndani ya miezi miwili ukachukue fedha zile halafu ukaziweke pale wakija *auditor* wa mfuko wa barabara watatwambia hatukuzitumia vizuri na fedha zile wametumia watu, kwa hivyo ndio maana zile tulikuwa tumeshaziomba na tumeshazipata hizo fedha tumezihamisha pale na tumezipeleka sehemu nyengine Pemba, ili kufanyia matengenezo ya barabara.

Mhe. Hamad Masoud Hamad alizungumzia barabara za MCC, yeye aliulizia vipi kasikia hazijengwi mpaka baada ya uchaguzi kwisha, hili nataka nilichange na la Mhe. Salim Abdalla Hamad alikuwa na hofu labda barabara ya Mtambwe ndio haijengwi. Sisi tunataka tuijenge kesho, ila kwa sababu tungepata kujisifia kwamba tumekujengeeni haraka haraka. Lakini tatizo haliko kwa SMZ, tatizo hao MCC wenyewe wao walitaka tujenge hizi barabara baada ya mwaka 2010, baada ya uchaguzi mwezi wa Novemba na nyengine zijengwe 2011 mpaka 2012, lakini sisi wizara tukapiga kelele tukasema huko ni mbali na mnatuumiza sana. Sasa baada ya mazungumzo ya kina sana wakakubali kwamba zitaanza kujengwa mwezi wa nane 2010 na ndio maana katika bajeti ya mwaka huu hakuna fedha zilizoombwa kwa upande wa barabara kupitia *MCC*, fedha zote zimepelekwa kwenye mradi wa umeme.

Waheshimiwa sio kwamba sisi tunataka tupozeshe mpaka uchaguzi, mimi ningelifurahi zaidi kama mpaka mwezi Disemba mwaka huu zitakuwa zimejengwa zote ningefurahi zaidi, lakini hali halisi ndio ilivyo na kwa bahati mbaya sasa katika shughuli za miradi zaidi za barabara na miradi mingine ukimwomba mtu akikukubalia, huwezi kutoka tena ukasema basi nakwenda huku kwanza, kwa sababu wao wenyewe wanazungumza kwamba mradi huu nimeshauchukua mimi na huu nimechukua mimi. Kwa hivyo, haiwezekani tena utoke nyumba hii leo ukaingie nyumba nyengine kesho utaonekana huna mipango madhubuti. Kwa hivyo, naomba waheshimiwa tuvute subra na tutaendelea kusaidiana nanyi ili miradi hii iweze kutekelezwa.

Halafu nizungumzie kwamba kwa barabara tatu za Pemba Kaskazini za *BADEA* na *SAUD FUND* tayari tumeshafunga mkataba na tayari vifaa baada ya wiki mbili vitafika Pemba, tutaanza na barabara ya Wete/Gando halafu Wete/Konde, tutajenga kwa awamu mbili, halafu baadae tutajenga Wete/Chake. Tumefanya hivi kwa sababu fedha ambazo tumezipata hazitoshi kwa barabara tatu zote kwa pamoja, lakini hizi tulizozipata tunaweza kujenga hizi mbili za mwanzo. Sasa tunaendelea na mazungumza na *SAUD FUND* na nafikiri DK. Mwinyi anajua na leo atatuongoza mchana saa saba tutakapozungumza na *SAUD FUND* ili watuongeze fedha kwa ajili ya hii barabara ya tatu.

Lakini pia kwa kupitia *OPEC* tumefanikiwa kupata fedha za ujenzi wa barabara ya Ole/Kengeja barabara hii mwanzo ilikuwa ijengwe na *MCC* wakakataa, lakini bahati nzuri *OPEC* hawakuwa na masharti magumu tunawasifu na kuwapongeza sana, sasa hivi tuko katika taratibu za kupata mjenzi baadae tutatangaza tenda ili kujengwa, barabara hii ina urefu wa kilomita 35 itawasaidia sana wananchi wa upande wa mashariki kisiwani Pemba. Lakini kule itasaidia kurahisisha mawasiliano na Mkoa wa Kaskazini na Mkoa wa Kusini Pemba, hili nalo mtaliona kwenye bajeti yetu ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Kuna barabara nyingi tu ambazo hapa hazikutajwa, lakini zimo barabara ya Mhe. Waziri Kivuli wa Mawasiliano na Uchukuzi ya kwendea Birikau imo kwenye Wizara yetu ataiona tutaijenga asiwe na wasi wasi.

Halafu Mhe. Hija Hassan kwanza nataka afahamu kwamba Mgagadu sisi tunaijenga na tumeshaanza kusafisha na tumekubaliana hatuondoki mpaka tumalize lami pale kuanzia Mgagadu mpaka Kiwani, kwa hivyo Mhe. Hija Hassan ukipata nafasi unaweza kuzungumza na wananchi wako ukawauliza kama kazi inaendelea au vipi.

Kuhusu barabara za *NORAD*, paliulizwa kwa nini watu wanaandikishwa halafu wanaulizwa vitambulisho, kwanza mradi huu kwa mujibu wa makubaliano yetu na *NORAD* kwamba wao wanatoa fedha halafu kuna kampuni ya *PORY* kutoka Uswiswi inatusimamia, lakini kazi itafanywa na UUB kwa mujibu wa makubaliano ya Mkataba. Sasa ili kuimarisha utendaji wa kazi au nguvu kazi za wizara mkataba huu umezungumzia kuwekezwa vifaa vya ukaazi, magari kununua spea na kuletewa vitu vingi tu ambavyo vitakwenda Pemba moja kwa moja na bahati nzuri tayari hatua za manunuzi tayari zimeshafanywa tunatarajia vifaa hivi kuwasili kati ya Julai na Agost.

Lakini kuna kazi *NORAD* wamesema katika kufanya kazi hii lazima wananchi wawezeshwe ili kupunguza umasikini, kwa hivyo kuna kazi zitafanywa na wananchi wa kawaida, sasa hao ndio watu ambao wanaangaliwa kuajiriwa na bahati nzuri hao hatuajiri sisi Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, hao watu wanaandikishwa, lakini atakayewafanyia *interview* ni mshauri hiyo kampuni ya *PORY*.

Sasa mtu hata kama utaniletea mie lakini anaweza kufeli akawa hawezi. Lakini sasa kwa ubinaadamu wetu na sio kwetu duniani kote ukitembea ukitaka chochote kile, lazima uwe na kitambulisho chochote na kule hawakuambiwa kwamba lazima kitambulisho cha ukaazi nafikiri hata *passport* unaweza kwenda nayo na ukajulikana, ama ukapata barua ya sheha kwamba huyu ndio fulani alimradi ujulikane kwa sababu tumekusudia wanufaike wale wananchi

ambao zinapita barabara katika maeneo yao. Kama wananchi wako wewe wa Kengeja, Mahaduthi wote watakwenda huko, usiwe na wasi wasi Mheshimiwa hili linawezekana.

Mhe. Spika, barabara ya Wambaa kama alivyosema mwenyewe Mhe. Moh'd Ali Sallim tumejitahidi sana kuifanyia ukarabati Dk. Mwinyi alikwenda juzi na mimi nimekwenda juzi katoka yeye nimeingia mimi, sehemu moja tu ndio mbaya kwa sasa hivi kwenye maungano ya barabara kuelekea Mgelema Kipapo kwa kuelekea huku Wambaa chini pale kabla ya kufika kwa Azani, pale kweli pabaya.

Sehemu nyengine zote unapita tena kwa muda mdogo mimi nilipopita pale niliona kumbe barabara ya Wambaa sasa hivi ni nzuri kuliko hata ya Gando wakati mwengine, saa hili ni kwamba tumeishughulikia sana na Gando tumekwenda kushughulikia, lakini bahati mbaya hatukuimaliza kwenye kilima cha mlima wa juu kwa sababu ndio yale tuliyopata maharibiko, lakini tumeagiza vifaa ndio vimeshafika kwa hivyo pale Kilimajuu tutatengeneza ile njia ya kupita pembeni na kutokezea uwanja wa mpira tuiwache na tupite moja kwa moja pale. Kwa hivyo Mhe. Said Ali Mbarouk kabla ya kukutengenezea barabara yako nayo itakuwa iko vizuri.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin nahakikisha kwamba hakuna upendeleo na wenyewe mmeona kama mtu anataka kusema atasema, lakini hakuna upendeleo, hii miradi ya muda mrefu mmeona ya Unguja tumefanya na Pemba tunaifanya na mwaka huu kama nilivosema mwanzo tutahamia sana Pemba ili kutekeleza miradi ya barabara na muda mwingi sisi tutakuwa Pemba ili kuhakikisha kwamba kazi hizi zinakwenda, hatumzuii mtu kusema.

Lakini tukimaliza kufanya yule mtu aje aseme kwamba kimefanywa, yule aliyesema basi aje aseme hapa kwamba kimefanywa ndio jambo liwe zuri, lakini tukimaliza kusema aje aseme mmeweza na mmefanya hongereni. Sasa nasema tukae, lakini ikifika muda mje kusema kweli mmefanya. Kwa hivyo, kama Mhe. Moh'd Ali Salim kama angekuwepo ningemwomba atuambie Makombeni waheshimiwa mmeshafanya vizuri kwa hivyo tuko pamoja.

Mhe. Suleiman Hamad kuhusu fedha za mfuko nimeshazisema kwamba kuna tatizo, maeneo ya bandari kwamba yanaingia maji ya mvua kwanza waheshimiwa hatujaona *terminal building* hapa ile ni dharura tu mpaka sasa hivi, lakini tutakuja kujenga jengo la abiria wa kuingia na wa kutoka, kwa hivyo hili lisimtie wasi wasi tutajenga kwa hivyo wazo lako lipo na tutaweka *parking* pale ndani sio nje. Kwa hivyo hili lisiwasumbue sana.

Kule ndani hatujengi kwa meli kubwa kwa sababu kule hatutaki abiria watumie tunataka abiria watumie huku tu, sasa tukijenga kule tutakuwa tunaingiza watu ndani ambao hawana shughuli maalum kwa hivyo kule hatujengi banda la kukaa abiria.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak nafikiri barabara yako nimeshaizungumzia ya Ndijani na hizi nyengine zitajengwa na SMZ japo kwa kifusi kama alivyosema Mhe. Rais, sisi Mhe. Rais akiahidi huwa tunafurahi kwa sababu kama hakuahidi hatuendi, hata kama wewe mwakilishi huwaahidi wananchi wako basi utakuwa huna jambo la kufanya, lakini lazima uwaahidi ili ukumbuke kwamba ninalo hili, sasa Mhe. Rais kaahidi barabara nyingi na tunazijenga. Kwa hivyo, mtu asiseme mbona huku kaahidi lakini hajafanya zile ni *challenge* zake za kiuongozi na anafanya na nafikiri mmeona ahadi zake nyingi tunazifanya, aliahidi kwamba barabara kuu zitamalizika kabla ya 2010 na tunatarajia hivyo kwamba zote zitakuwa zimemalizika kama tulivyopanga.
Mhe. Abass Juma Muhunzi alizungumzia barabara ya ukanda wa mashariki ambayo nimeizungumza bahati nzuri hayupo, lakini ni kwamba ukanda ule utazunguushwa kwa barabara ya Ole/Kengeja ambayo itapita Pujini, Chambani na sehemu nyengine.

Mhe. Spika, mimi nadhani kwa upande wangu mambo ambayo yamezungumzwa ya Wizara yetu ni hayo zaidi tutaonana tarehe 24/07/2009 siku ya bajeti yetu nafikiri mtatuunga mkono kwa bidii ili tuweze kutekeleza kazi zetu. Nashukuru sana.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kama walivyotangulia wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu na mimi pia nafanya hivyo kwa kutuwezesha sote kuwepo hapa hii leo, mimi nimesimama hapa kuichangia bajeti ya serikali na naichangia katika maeneo yale ambayo yamezungumzwa kwenye bajeti yenyewe, sitaki niende nje ya yale ambayo hayakuzungumzwa kwenye bajeti hii kwa sababu najua mengine yatakuwemo kwenye zile bajeti za wizara husika.

Mhe. Spika, kwanza pia nataka nimpongeze rafiki yangu profesa Ibrahim Lipumba mwenyekiti wa Taifa wa chama cha CUF kwa muono wake wa bajeti hii hasa ya mwaka huu ambayo amesema hii bajeti ni nzuri na imekidhi haja, nimesoma kwenye gazeti, lakini nilipokutana nae wakati wa chai alinambia hivyo hivyo, sasa kama Mwenyekiti wa CUF ameunga mkono viongozi wa CUF hawaungi mkono ama itakuwa ni misimamo au itakuwa hakuifahamu vizuri hii bajeti yenyewe. Kwa sababu Profesa Ibrahim Lipumba yeye ni mtaalam aliyebobea kwenye masuala ya uchumi, kwa hivyo ilikuwa ni haki

yangu na ningestaajabu sana kwa bajeti hii ilivyopangwa na kuandikika ningestaajabu sana kama asingeunga mkono na kuisifu.

Lakini la pili nataka nichangia kwenye vile vifungu ambavyo vimetajwa kwenye bajeti hii ili kuviweka sawa na kutoa maelezo ya ziada ambayo mwenyewe Mhe. Waziri atakapokuja na nadhani atakuwa amepata msaada kutoka kwangu kama alivyopata msaada kutoka kwa Mhe. Machano hivi sasa.

Mhe. Spika, wajumbe walizungumzia habari ya *inftation* na swahibu wangu Mhe. Haji Faki Shaali alikuwa anastaajabu kwa nini kilimo kimechangia au kimeengezeka mchango wake katika pato la serikali, lakini mbona bado kuna *inflation* na wapo wengine waliochangia namna hiyo au waliokuwa na dhana ya namna hiyo, kwa upande mmoja suala lake ni sahihi kama kilimo kimepanda maana yake chakula tumezalisha na kwa hivyo bei ya bidhaa hizo za chakula imepungua na *inftation* nayo lazima ipungue. Lakini, tukubali kwamba idadi kubwa ya matumizi tunaagizia kutoka nje idadi kubwa sana pamoja na hicho chakula pamoja na huo mchele, kama wengi walivyosema ulimwenguni sasa hivi bei za bidhaa zimepanda kwa sababu ya matatizo ya uchumi iliyoikumba dunia nzima. Sasa kama tutaendelea kuagizia mchele badala ya kula muhogo tunaolima wenyewe tutaendelea kuagizia pishori badala ya kula ndizi tunazolima wenyewe kwa kilimo peke yake hakiwezi kuondosha *inftation.*

Mhe. Spika, kilimo chetu sisi kitasaidia katika kuleta *food security* na kupunguza hiyo gap ya *inftation*, lakini kilimo cha Zanzibar hakiwezi kabisa kuondosha *inftation*. Sitaki nizame sana kwa hili kwa sababu nitajinyima nafasi katika maeneo mengine. Lakini kuna sekta zinazoleta *inftation* kutoka nje ambazo hatuna uwezo nazo ka mfano mchangiaji mmoja alichangia hapa, anasema watu baada ya kusikia kuna nyongeza ya mshahara bei ya chakula kidogo imepanda tumeongeza mshahara kupunguza makali ya umasikini ili wananchi wenye kipato cha chini sana hata kama kilichoongezwa hakitoshi, lakini haba na haba hujaza kibaba, lakini ile *effect* ya mshahara tuliyoongeza inaanza kuonekana hivi sasa kwa maana baada ya kuongezeka tu hizo shilingi elfu ishirini zinazoambiwa ni kidogo, basi tayari bei zitapanda karibu shilingi ishirini na tano. Kwa hivyo hizi ni sekta ambazo zinasababisha *inflation* hata kama serikali imejitahidi kwa njia moja au nyengine kuondosha *intlation* hasa kwenye bei za bidhaa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nataka nije kwenye suala la kilimo kama nilivyokwisha kuligusia, kilimo ni kupunguza *inflation* kwa kiasi fulani, lakini kilimo zaidi ni kwa ajili ya *food security.* Wengi wamezungumza kilimo chenyewe hakibadiliki kijembe kongoroka na kadhalika, hatutaki kukubali kwamba tumepiga hatua kubwa na kwa wale wanaobahatika kwenda

mabondeni na hasa Mwenyezi Mungu alivyotubariki safari hii hali ya hewa ni nzuri, atakuta mazao yalivyoshamiri, atakuta kilimo cha mpunga kilivyoshamiri kwa kasi kubwa kutokana na matrekta ishirini na nne tu yaliyoletwa.

Serikali itaagiza matrekta mengine ishirini na nne au zaidi inategemea na hali ilivyo na ndio maana bajeti ya wizara ya kilimo au sekta ya kilimo ikapewa kipaumbele kikubwa kwa sababu ya umuhimu huo, kwamba tunataka kubadilika, na wale ambao wataendelea kusema tu bila ya kufanya kazi huko tunakokwenda bado hali haijawa nzuri, wakubwa wanasema matatizo yaliyokuwepo hayawezi kuondoka chini ya miaka miwili.

Lakini nina hakika *recession* iliyotokea mwaka 1933 ilidumu kwa miaka mitano, sasa sisi kama tutabahatika kuiondosha kabla ya miaka miwili, basi nasema tutajipongeza, lakini lazima tufunge mikaja, tukalime na tusilalamike papai limepanda bei, nazi imepanda bei, ukifika wakati wa mvua huendi kupanda mche wa mnazi, hupandi papai, hulimi wewe kazi yako ni kulaumu tu na kuitaka serikali ifanye kila kitu, serikali katika mambo mengine imeshajiondoa iko kwenye utaalam na pembejeo shughuli za kulima ni za wananchi wenyewe. Serikali imekusudia kuwarahisishia shughuli zao za kulima kwa ajili ya kuongeza idadi za matrekta, hata Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amezungumza kipindi hiki tukiongeza idadi ya matrekta na yeye ataongeza idadi sawa na hiyo ili shughuli za chakula cha matrekta zipate ziende vizuri zaidi.

Mhe. Spika, wengi wamezungumza bajeti tegemezi wameilaumu bajeti hii kwamba bado inaendelea kuwa bajeti tegemezi, nataka niwahakikishie kwamba bado itaendelea kuwa bajeti tegemezi na hawa tunaoita washairiki wa maendeleo tumejenga *partnership* katika kuendeleza uchumi wetu na mambo mengine. Sisi hata tukikubali bado tunaendelea kutegemea *development partnership* hawa wamegawika sehemu mbili, kuna wale walioko katika mkono wa *multilateral* na wale walioko kwenye mkono wa *bilateral* hawa wa *multilateral* wanatupa msaada kutokana na uanachama wetu katika *association* hizo kwa mfano, *World Bank, IMF, IFAD* n.k.

Tanzania sisi ni *member* wa mashirika hayo ya kimataifa kama ni *member* tumeridhia na kama tumeridhia na wao wameridhia. Kwa sababu hiyo sisi tunalipa michango yetu kikamilifu, kwa hivyo tunachokipata kutoka kwao ni sehemu ya kile ambacho sisi tuna *contribute* kama sisi ni memba wa hizo taasisi.

Kwa hivyo, *World Bank* wakikubali kutusaidia maana yake wametusaidia kwa sababu sisi ni wanachama na tuki-*default payment* ama wakatufukuza au watapunguzia misaada ile ambayo tunastahiki kupata, mimi nasema kwa lugha

ya kisiasa ni sawa tuseme kwamba mpaka lini hatutajitegemea wenyewe, tutaendelea kutegemea wahisani, hawa sio wahisani tumewabadilisha jina tunawaita *development patner* ni washiriki wa shughuli zetu za maendeleo kwa sababu sisi ni wanachama wao.

Lakini tukiingia kwenye urafiki wa nchi na nchi kama ameridhika kwamba wewe ni rafiki yangu na kuna mapungufu fulani nikikusaidia wewe utaondokana nayo, basi kuna ubaya gani, mimi nasema wategemezi wa bajeti kuna nchi kwa mfano Mayote, Misri, Reunion na nyenginezo hawa bajeti zao zinakuwa *total* katika sehemu kubwa sana na wengine wamekataa kupewa uhuru, wanabaki kwenye mahamia ya zile zilizokuwa zimewatawala kwa kuendelea kupata faida kama hizi, sisi tuko huru tumejitawala na hatutegemei moja kwa moja, bajeti zetu zisimamiwe, zipangwe na zitekelezwe na hawa hapana. Tunasimama wenyewe, tunapanga wenyewe na tunatekeleza wenyewe na *patner* anakuja kuturidhia.

Mhe. Spika, kutokana na utaratibu huu imekuja hivi karibuni utaratibu wa kusamehe madeni na chini ya huu mradi maarufu unaitwa *MDRI*, sisi katika msamaha unaotoka tuna 4.5 yetu hii ni haki yetu hatutegemei sio utegemezi ni haki yetu tumepewa hizi pesa na tumenunua matrekta, tumenunua magari na zile tumenunua Wizara ya Afya sasa hivi imekuwa *highly modernized* kutokana na vifaa vilioko pale vya *CT scan*, kuna vifaa vya darubini ya kupimia presha ya macho, mimi ndio kwanza nimesikia juzi, najua binadamu anapimwa presha ya damu, lakini sasa kuna ya macho unapimwa baada ya saa moja unapata matokeo tena ya kileo kabisa. Tumenunua vitu vingi sana nimekwenda kutizama *X-ray*, unageuzwa kama *toys*, unageuzwa huku mara huku ukitakiwa ubavu huambiwa inuka tu ukae hivi ya kileo kabisa, sasa pesa hizo utasema ni utegemezi.

Kwa kweli sisi wenyewe tusingekuwa na fedha hizo katika bajeti yetu, lakini kwa sababu ni haki yetu tumesamehewa madeni, kama Tanzania imesamehewa na Zanzibar imo, sasa tumepata haki yetu na keshokutwa nitakuja kulizungumza hili nitakapotoa bajeti yangu ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kuwa tunanunua vifaa vya kileo vya *digital* kuibadilisha studio yetu *more than hundred and sixty million shillings* tayari zimeshakuwa *committed* katika huu mradi wa *MDR*, huo sio utegemezi ni haki yetu. Kwa hivyo nilitaka kidogo nitumie muda katika sehemu hii kuondosha ile dhana ya kwamba bajeti tegemezi.

Lakini labda nizungumze kitu kidogo tu unapofaulu kupewa msaada au kupewa mkopo na mambo mengine, kuna sifa lazima uzitimize kwa mfano wewe nchi yako inayo sifa ya kukopeshwa na ulipokopeshwa pesa ulizitumia vzuri,

credibility ya pesa zako iko vipi n.k. hukopeshwi tu kama sadaka wala hupewi kama sadaka.

Lakini la pili bajeti yetu ukiitizama ya mwaka huu ile *breakdown* inaonyesha mikopo ni mikubwa kuliko misaada tafsiri yake nini? Mkopo maana yake ni pesa yako unakopeshwa, hudaiwi, utalipa sasa. Ile kukopeshwa inatakiwa kuna vitu ndio ukopeshwe. Kwa hivyo shilingi milioni 102,309 mkopo na shilingi 96,000,000/= ndio msaada sasa hata huo msaada ni mdogo kuliko mkopo, huo msaada unapata kwa sababu unafaa na huo mkopo unakopeshwa kwa sababu unafaa.

Mhe. Spika, watu wengi wamezungumzia suala la kutetereka kwa uchumi duniani Mhe. Abass Juma Muhunzi alizungumza kama kutukumbusha sote tunaelewa hali ya uchumi ilivyo sasa hivi ni kwamba uchumi umefungamana. Hakuna nchi peke yake inayoweza kujiendesha kupanga mipango yake peke yake kiuchumi bila ya kushirikiana na mwenzake. Kuna Muungano wa kidunia nzima na kuna Muungano wa Kikanda.
Mhe. Spika, uchumi ulipotetereka kwa Wakubwa na sisi tumepata mtetereko mkubwa, wale wanaosema hatukutetereka hawajaenda mbali sana na wala tusijipe moyo tukasema sisi uchumi ulivyotetereka ulimwenguni sisi haujatugusa na hautugusi, aa. Mfano mmoja tu umetolewa hapa kwenye utalii na utalii ni sekta ambayo tunaiona sasa hivi, sio ita-*take over* kwenye biashara za karafuu na kadhalika lakini ita *supplement* kwa sehemu kubwa sana kipato chetu cha fedha za kigeni. Utalii umeanza kutetereka kwa sababu ulimwengu umetetereka.

Wale waliokuwa wanakuja kutalii kwa sababu walikopa pesa kule ambazo wanakopeshwa makusudi ili waje watalii, basi kutetereka kwa uchumi wa ulimwengu *credit grant* imetetereka. Kwa hivyo, wale waliokuwa wanategemea kupata hiyo *credit* ili watalii wameacha na wale wachache wanaojimudu ndio wanaotumia pesa zao sasa kwa sababu ile *credit* haipo tena huja katika kutalii. Kwa hivyo, *definitely* hiyo imetetereka, tumwachie mwenyewe waziri atapokuja atakuja kutuambia *rescue package* yake ya utalii iko vipi, lazima kuna mambo mwenyewe ameshajitayarisha na watu wake.

Hivi karibuni alifanya ziara kubwa sana kwenda kuangalia hali halisi ya utalii ulivyo na vipi ata *incorporate* hiyo hali halisi na utalii wetu wa Zanzibar. Kwa hivyo, hakuna hata mmoja aliyekaa kusema tu kakamata kichwa analia mama, mama, ni kuhakikisha pale tulipo tunaondoka hata kama si kwa kasi kubwa lakini tunaondoka na *Inshaallah* tutaondoka.

Mhe. Spika, ninazo *figure* za hivi karibuni kiasi miezi mitatu iliyopita, kutetereka kwa utalii katika mataifa makubwa. Kwa mfano Ujerumani

kutetereka kwa uchumi, Ujerumani uchumi wake umeshuka kwa asilimia 3.2, uchumi wa Ufaransa umeshuka kwa asilimia 1.6, uchumi wa Uingereza asilimia 2.1 na uchumi wa Marekani asilimia 1.2. hizi ni *figure* kama za miezi minne iliyopita sijui hali sasa hivi iko vipi. Kwa hivyo, hawa ni wakubwa wamekwenda chafya sisi wadogo lazima tutapata *flu*. Sasa uzito wa ile *flu* yenyewe inategemea tumejitayarisha vipi kupambana na *flu* hiyo. Mtu mmoja ananimbia *flu* ya nguruwe Mwenyezi Mungu atuepushie.

Sasa tukubali na mimi nakubali na pengine nisije nikasahau naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja kwa sababu imejitayarisha vizuri sana kukabili hali ya mtikisiko wa uchumi kwa dunia.

Mhe. Spika, kuna suala limezungumzwa la ajali ya meli, wala nisingependa kulizungumza hili kwa sababu halimo kwenye bajeti yetu. Lakini imetolewa shutuma nzito sana zidi ya serikali na kwa kweli tamko hilo ambalo tayari limesharikodiwa kwenye *hansard* mimi nadhani linahitaji kutolewa ufafanuzi ili *hansard* iweze kurikodi yote mawili.
Mhe. Spika, ilitajwa meli iliyoungua njiani, imetajwa meli iliyozama Malindi na ikasemwa serikali inahusika na ajali zote zilizotokea. Mimi nakataa serikali haihusiki, kama tunajua utaratibu wa meli basi tumuoneshe kidole nahodha wa meli, alitimiza masharti yote ya kuendesha meli yake?

Kwa mfano, nina *cutting* hapa ya gazeti la *The Guardian* la tarehe 12 Juni, 2009 na *cutting* hii nimeitoa katika ukurasa wa nne. Linasema "***SUMATRA Seizes Boat Bound for Zanzibar for Over Loading***". Meli ya MV Sepideh ilizuiliwa bandarini juzi tarehe 4 Juni, 2009, inatoka Dar es Salaam inakuja Zanzibar. Meli hii ina *capacity* ya kubeba abiria 325 lakini ilibeba abiria 400, kwa hivyo ilikuwa na *axes* ya abiria 75. Watu wa *SUMATRA* na watu wa Bandari walipokwenda kuikamata meli ile wakamuhoji nahodha, wakatizama *manifesto* yake nahodha, kuna majina hayo 75 hayamo katika *manifesto*. Nahodha alipoulizwa akasema hawa ni ziada kwa sababu ni watoto waliofuatana na wazazi wao, kwa sababu mtoto hana roho, mtoto akifa si tatizo maana yake ni mtoto tu.

Kwenye meli ile iliyoungua moto hapa nataka nifute ile shutuma ya rafiki yangu Mhe. Hija Hassan Hija kwamba serikali haikushughulika na chochote, sana sana kaenda Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi kule Mombasa. Lakini aliyekwenda ni Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, lakini sio Mhe. Waziri kama binadamu Mhe. Hamza hapana, aliyekwenda ni Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi na ninajua kafuatana na maafisa wake wa shughuli za maafa. Lakini Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii alikuwemo pamoja na Mhe. Hamza katika msafara huo.

Mhe. Spika, mimi kwa niaba yangu binafsi, kwa niaba ya serikali na kwa niaba ya chama changu cha CCM, nilikwenda Kiwani jimbo ambalo Mheshimiwa ndiko anakotoka, nilikwenda kutoa mkono wa rambirambi kwa wafiwa, nikatoa mkono wa rambirambi, nikatoa ubani, bahati nzuri katika waliokuwepo katika familia ile ni mtoto mmoja ambaye alizama lakini akaokolewa. Sikutaka kumdadisi sana lakini nilimdadisi kidogo na kupata *some of caution information* ambazo sitaki nizieleze hapa kwa sababu uchunguzi bado unaendelea.

Mhe. Spika, meli haikufuata utaratibu unaotakiwa, imeondoka saa nne za usiku badala ya saa 11 iliyopangiwa na kadhalika na kadhalika kwa nini ilifanya hivyo. Lazima kuna vitu vimefichwa na hivyo vitu ndivyo vilivyosababisha meli iungue. Kama meli iliondoka Tanga au Mombasa nafikiri ile *port* ya pale meli ilipoondokea na yule mhusika (nahodha) ndio wanaowajibika kuangalia *manifesto,* idadi ya mizigo, uzito wa mizigo na aina ya mizigo na abiria na kadhalika, sio njiani wala sio pale ilipofikia ile meli.

Kwa hivyo, meli iliyozama Malindi nayo ilitokea Dar es Salaam Mhe. Waziri hakuwepo pale, Mhe. Mkuu wa Bandari hajakuwepo pale Dar es Salaam na meli ile ilipewa ruhusa pale baada ya kuangaliwa bila shaka, sasa imefika kwenye *port* ikapata ajali, lakini tunaambiwa serikali ilihusika ndio maana nikataka nichangie japo kidogo kwa hili kuweka sawa kwamba serikali siyo iliyohusika.

Bajeti yetu kama ilivyoandikwa imegusa vitu vitatu vya jumla, imeheshimu dira ya 2020 ambayo sasa hivi inatekelezwa kwa miaka mitatu mitatu chini ya mradi wa MKUZA kwa kuondosha umasikini na balaa la njaa. Lakini pia inatekeleza ilani ya uchaguzi wa CCM. Watu huuliza tena kwa ukali sana, hivyo hii bejeti ya serikali ina uhusiano gani na ilani ya uchaguzi wa CCM?

Hii ni Bajeti ya Serikali ya CCM kwa maana imeletwa hapa kwa sababu CCM ilishinda, na ilishinda kwa sababu ilikuwa na ilani, ilani hii ilitangazwa kwa wananchi na ikauzwa na wananchi wakainunua kwa kuipigia kura. Sasa ilani ni ahadi ya utekelezaji kati ya mpiga kura na serikali yenyewe. Kwa hivyo, kutekeleza bajeti kwa sera ya ilani ya uchaguzi wa CCM ni sahihi kabisa, kwa hivyo, bajeti hii imezingatia mambo haya matatu ya dira, MKUZA na Ilani ya CCM na ndio maana ikajengeka namna hii kwa kujali mahitaji ya wananchi.

Namalizia kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri, bajeti yetu kwenye mipango ni asilimia 58.1, bajeti yetu kwenye *recurrent* ni asilimia 41.9, sidhani kama tungeweza kufanya jambo la maana na kuyaangalia mahitaji ya wananchi ya kujali na kujitayarisha hali mbaya ya uchumi iliyotukabili kama tusingekuwa na bajeti ya namna hii. Tunajenga barabara na huko ndiko ilikojikita zaidi,

maji, umeme na kadhalika, miundombinu. Miundombinu maana yake ni vichocheo vya kudumu vya ukuaji wa uchumi, kama tume-*invest* pesa zetu nyingi katika suala hilo na pesa kidogo tume-*invest* katika matumizi ya kuendesha serikali kusingekuwa na bajeti nzuri katika kipindi hiki tulichoandamwa na kuanguka kwa uchumi kwa nchi ndogo kama Zanzibar kuliko hii.

Mwisho watu wengi wamezungumza *stimulus package*. Wakubwa waliokwamba huko wanaita kila lugha *rescue package, stimulus package* na kadhalika. Sina haja ya kwenda mbali kwa sababu ya muda kusema aliyesababisha hali hii ni nani hata sasa tukawa tuko katika kutayarisha *package* kama hizi, lakini kwa sababu sisi limeshatufika kama tulivyosema mwanzo lazima tujitayarishe.

Stimulus package ya Zanzibar ni aina yake, kwa sababu sisi Zanzibar kama Zanzibar peke yetu hatuwezi ku-*manoeuvre* sana katika *monetary policies*. Labda tuka-*print* pesa ambayo kwa utaalamu wa uchumi wa siku hizi watu hawafanyi hivyo, tukazigawa pesa katika mabenki ili benki ziweze kukopesha, hatuwezi kufanya hivyo lakini sisi tumefanya nini?

Mhe. Spika, tumefanya mambo manne, katika bajeti hii *stimulus package* yake inahusu mambo manne kwa nilivyoyatafsiri mimi kwenye hii bajeti.

La kwanza, Mhe. Hamad Masuod alizungumza vizuri sana kuhusu kupunguza kodi ya *VAT*. Wengine wanakubali kwamba hatua ya kupunguza ni nzuri, lakini kwa vyovyote vile watoe kosa, watoe *alternative suggestion* na kadhalika wanasema kwa nini imepunguzwa kutoka asilimia 20 mpaka asilimia 18 isingekwenda kwenye asilimia 16 au 15, ingepunguzwa kwenye asilimia 16 basi wangesema kwa nini isingekwenda kwenye asilimia 10 na kadhalika.

La msingi tumepunguza kodi ya *VAT*, kwa nini? Kwa sababu gharama za *importation* ziwe ndogo, gharama za uzalishaji wa ndani wa bidhaa zipungue, zikipungua zitamsaidia mlaji. Kwa mfano, gharama kutoka nje za vipuri na kadhalika zitapunguza gharama za *industry* na kwa hivyo kitakachoanzishwa katika *industry* gharama yake itapungua, yote inalenga kum-*rescuer* mlaji ndio maana tukaita *rescuer package*.

Mhe. Spika, lakini huku tunapunguza kodi huku tunapandisha mishahara ya kima cha chini, *again* kama kawaida wanasema kutoka sh. 80,000 kwenda sh. 100,000 ni ndogo sana, tungeweka sh. 150,000 basi watu wangesema kwa nini isiwe sh. 200,000. Kwa sababu mawazo yanatofautiana na hiyo ni sifa ya mwanadamu na wala si kosa hata kidogo. Kwa sababu tumeambiwa hitilafu za maulamaa ni rehma, sasa tukihitilafiana katika mawazo ni baraka, lakini tukija

katika *reality VAT* tumeipunguza, mishahara tumepandisha. Hiyo ndio *rescuer package*, wakati tunampunguzia gharama mlaji lakini pia tunampa uwezo ale vizuri, lakini sasa hawa wabaya ndio wanaanza na wao kumvuruga huyu mlaji wenyewe.

Kama kwamba hayo hayakutosha, *rescuer package* imesema bajeti ya maendeleo tunaipandisha ili tupate infrastructure zijengwe vizuri kwa haraka. *Priority*, *rescuer package* yetu imeweka *priority* kwenye kilimo, elimu, afya na mawasiliano haina maana kwengine tumedharau lakini hiyo ndio *rescuer package* yetu.

Mhe. Spika, naipongeza sana bajeti hii, nampongeza sana Mhe. Waziri na naomba sana tuiunge mkono pamoja na Mhe. Abass Juma Muhunzi ambaye sasa hivi hayupo na Mheshimiwa mmoja aliyesema kwamba yeye ataunga mkono ile bajeti ya Waziri Kivuli hatounga mkono bajeti hii. Mimi namsihi aunge mkono ya waziri kivuli lakini na hii aiunge mkono kwa sababu hii ndio yenye matumizi na mapato na utekelezaji.
Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii narejea tena kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Donge, kwa niaba yangu binafsi naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena ninakushukuru sana kunipa fursa hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kufanya majumuisho ya michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe katika hotuba yangu ya hali ya uchumi na mpango wa maendeleo pamoja na makadirio ya bajeti na mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mhe. Spika, naomba nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Waheshimiwa wote, wale waliopata nafasi ya kuchangia hotuba hii kwa sababu ya muda wengine hawakupata, lakini walikuwepo Barazani hapa wakasikiliza kwa utulivu na wengine tukabadilishana mawazo nje ya ukumbi, kwa kweli wote tunawashukuru sana.

Mhe. Spika, niseme tu kwa uongozi wako wa busara basi hata vionjo mwaka huu kwenye bajeti ya speech naona vilikuwa vidogo vidogo tu au kwachati kwachati tu hivi. Hata mheshimiwa rafiki yangu safari hii kwa sababu labda kapata uwaziri kivuli kidogo kapumua Mhe. Said Ali Mbarouk.

Kwa kweli tunashukuru sana hali ya utulivu na michango Mhe. Spika, ni mingi mno na yote sisi tumeipokea. Sasa kwa muhtasari tu naomba nizitaje zile dondoo za hoja zilizozungumzwa na Wajumbe takriban wengi sana kwa njia moja au nyengine umezigusia.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wengi sana wamezungumzia:-

1. Suala la ongezeko la idadi ya watu.
2. Matatizo ya wadudu waharibifu wa mazao na matunda.
3. Bei ya mwani na kilimo chake kwa jumla.
4. Suala zima la karafuu, tokea kilimo chake mpaka uuzaji wake.
5. Biashara na Tanzania Bara hasa viwango vya kodi vinavyotozwa na *TRA*.
6. Ujenzi wa Barabara hasa Pemba.
7. Miradi midogo midigo ya wananchi.
8. Utalii na mapato tunayoyapata.
9. Kadi za vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.
10. Nyongeza ya mishahara ndogo.
11. Nyongeza ya mishahara iliyofanywa basi ifanywe kwa mpigo, yaani kwa mara moja sio kwa mara mbili kama tulivyoshauri.
12. Penchni tumeambiwa nayo tutizame kwa jicho la huruma kuwa ni ndogo.
13. Huu mpango wa kujinusuru kutokana na mtikiso wa uchumi.
14. Mapato ya ndani *vis-visa* kupimwa bajeti ya kawaida na ya maendeleo.
15. Ni *co-operate tax* kwa kodi za muungano kulipwa Zanzibar
16. *VAT* ipunguzwe zaidi
17. Kodi ya Majengo
18. Kodi ya ardhi
19. Tumeambiwa au tumeshauri tusiwe waoga, tusiogope watu, tuwe wakakamavu
20. Kodi za Halmashauri za Wilaya kuchukuliwa na kuhamishiwa *ZRB*
21. Suala la mafuta hatukuligusa kabisa tumemuachia Mhe. Mansour?
22. Suala la maafa
23. *JFC*

Sasa tumejaribu kuyaoresha haya masuala takriban Waheshimiwa wengi wamezungmza. Kwa kweli Mhe. Spika, haya mambo ni mengi lakini kama nilivyosema sisi tumeyaweka kama kwanza ni ushauri, pili ni ufafanuzi uliotolewa na tatu kuna maswali yanataka kujibiwa.

Sasa nitawaomba sana Waheshimiwa waliochangia nje ya haya kama hatukuyagusa basi ninawaomba radhi ni kwa sababu ya muda tu Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa kunieleza kwamba nijaribu sasa hivi na nina fursa na kuendelea tukirudi jioni. Kwa kweli itakuwa vizuri sana kwa sababu naona mambo ni mengi na haitokuwa vyema kumuachia au kuacha rafiki yangu Mhe.

Hijja nisimguse, halafu ninataka mwaka huu kidogo aikubali bajeti hii, aoneshe mageuzi kwa kweli. (*Makofi*).

Mhe. Spika, Waheshimiwa waliochangia kwa jumla wote ni 35, ukumbini hapa wamepata fursa Waheshimiwa 34 na mheshimiwa mmoja kachangia kimaandishi. Sasa niwatambue kwa ruhusa yako mmoja mmoja:-

1. Mhe. Haji Omar Kheir
2. Mhe. Said Ali Mbarouk
3. Mhe. Ali Suleiman Ali
4. Mhe. Haji Mkema Haji
5. Mhe. Rashid Seif Suleiman
6. Mhe. Asha Moh'd Hilal
7. Mhe. Said Khelef Ali
8. Mhe. Haji Faki Shaali
9. Mhe. Ali Abdulla Ali
10. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
11. Mhe. Abubakar Khamis Bakary
12. Mhe. Salmin Awadh Salim
13. Mhe. Mkongwe Nassor Juma
14. Mhe. Zakiya Omar Juma
15. Mhe. Ali Denge Makame
16. Mhe. Hamad Masoud Hamad
17. Mhe. Mohamed Ali Salim
18. Mhe. Bihind Omar
19. Mhe. Hijja Hassan Hijja
20. Mhe. Assaa Othman Hamad
21. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu
22. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin
23. Mhe. Omar Ali Shehe
24. Mhe. Ame Mati Wadi
25. Mhe. Ali Moh'd Bakari
26. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
27. Mhe. Ali Haji Ali
28. Mhe. Mtumwa Mbarouk
29. Mhe. Abass Juma Muhunzi
30. Mhe. Zainab Omar Moh'd
31. Mhe. Najma Khalfan
32. Mhe. Salim Abdulla Hamad
33. Mhe. Machano Othman Said
34. Mhe. Ali Juma Shamuhuna
35. Mhe. Fatma Tamim (amechangia kimaandishi)

Mhe. Spika, wote tunawashukuru na kusema ahsanteni sana kwa michango yenu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwa kweli bajeti yetu mwaka huu ilikuwa na mafanikio sana kwa vile Waheshimiwa hatukuwa na jazba ya kuchangia bali ilikuwa na vionjo, najua wawili kidogo na hasa nimnukuu Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin alikasirika kidogo Mhe. Mohamed Ali Salim alipozungumza suala la mikarafuu Pemba watu wakafyonya. Alipozungumza kidogo haikufurahisha ndio maana watu wakafyonya pale kwa sababu mambo haya tumeyasahau tena kuzungumza Upemba, Uunguja, Utumbatu, sote hapa baba mmoja mama mmoja, Unguja na Pemba tunapendana, tunashirikiana, tunaoana, tunatembeleana.

Mhe. Spika, mimi leo Mkanyageni nakwenda Mhe. Haji Faki Shaali ananipokea. Mimi siku zote namkuta anatoka Jang'ombe kwa miguu wala haulizwi yuko huru. Sasa tukirudisha mambo haya si vizuri ndio maana watu wakawa wanafyonya. Mhe. Spika, hivi sasa sote tumeshikana, masuala ya mafuta tumezungumza vizuri na masuala mengine, tena turudi tu kuzungumzia lugha hiyo.

Mhe. Spika, nimeipenda sana lugha ya Mhe. Ame Mati Wadi alivyozungumza nampa hongera sana, huyu ni *philosopher* mwengine wa Barazani hapa.

Halafu Mhe. Spika, kuna mtu tunamwita Paul Kagame hapa, Mhe. Ali Moh'd Bakari. Mhe. Spika, mimi namsifu sana Mhe. Ali kwa *philosophy* yake, maana yake kaja katutuliza, katwambia na kaonesha mwelekeo na hivi ndio tunavyotaka. Kijana mdogo anatulia shababi anaonesha ana damu ya kuchemka hasa na anatuonesha njia nzuri twende. Mhe. Spika, nampa hongera sana hayupo hapa na kweli anafuata nyayo za Kagame anavyoijenga Rwanda huko. Tunampa sifa sana.

Mhe. Spika, kwa kweli nimeona nizungumze haya na kutoa shukrani kwa Baraza zima hasa kwa michango yao. Michango kama nilivyosema ilikuwa ya kusisimua, mizuri na ya kutuelekeza.

Mhe. Spika, sasa naomba nianze kuchambua hapa na pale kama mjadala ulivyokwenda. Mhe. Spika, nianze kwa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti tunamshukuru sana. Kwa sababu yeye ni Mwenyekiti wa Wenyeviti kwa hivyo mawazo aliyotuwakilishia ni mawazo ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza. Sasa mchango wake kwa kweli ulikuwa mkubwa na maelekezo aliyoyatoa mengi ni ya kutusaidia na niseme tumeyapokea.

Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti alianza kwa kuzungumzia vipi tutaweza kushajihisha vyanzo visivyokuwa na kodi. Mhe. Spika, serikali imeupokea ushauri wake na niseme kwamba tutaufanyia kazi juu ya vyanzo mbali mbali visivyokuwa vya kodi vilivyopendekezwa. Aidha, serikali itafanya mapitio ya vyanzo vyote vya mapato kwa lengo la kupunguza utitiri wa kodi ili kuleta ufanisi katika mfumo mzima wa ukusanyaji wa mapato nchini.

Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti pia alizungumzia suala la kuimarisha sekta ya viwanda. Mhe. Spika, kwa kweli kuna haja ya kuimarisha sekta ya viwanda. Lakini ndio pale walipozungumza Mhe. Ali Juma Shamuhuna na wengine kwamba serikali kazi yake ni kutandika sera na kutoa *policies* nyengine kuwakaribisha hao wawekezaji wa viwanda. Sisi kama serikali hatufanyi viwanda tena, haturudi kwenye hali ile ya zamani tuliyokuwa nayo.

Serikali kupitia Idara ya Viwanda inawasaidia wenye viwanda kwa kuwapa ushauri juu ya namna ya uzalishaji bidhaa kwa unafuu, kuongeza ubora wa bidhaa *(value addition)*, kuongeza uzalishaji wa bidhaa ili kutosheleza mahitaji ya soko la ndani na kuuza nje. Aidha, wenye viwanda hupatiwa mafunzo juu ya utafutaji wa masoko pamoja na kushiriki katika maonesho ya biashara.

Mhe. Spika, jengine alilotushauri Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti ni suala la marekebisho ya viwango vya kodi ya ardhi. Mhe. Spika, serikali kupitia Bodi ya Mapato Zanzibar inafanya mapitio ya viwango vya kodi na hatimae kuweza kuishauri serikali juu ya viwango, vigezo na utaratibu bora wa utozwaji wa kodi za ardhi.

Halafu pia alitushauri suala la mapato yanayokusanywa na *ZRB* yakusanywe na Idara ya Uhamiaji. Huu ni ushauri mzuri na hili tutalizingatia kwa sababu kidogo kuna taratibu za kisheria na kikatiba, sasa inabidi tuziangalie vipi tunaweza tukalifanikisha suala hili.

Mhe. Spika, ushauri mwengine alioutoa Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti ni fedha za kukabiliana na maafa kwamba kwa nini zisitolewe kwenye mfuko wa hazina na badala yake zinatolewa kwenye fungu la idara ya kukabiliana na maafa. Mhe. Spika, nikiri kwamba hilo tumeliona, tumelipokea na tutalifanyia kazi. Kama alivyosema kwa kweli kama walivyosafiri mawaziri na hata maafa mengine yaliyotokea imebidi mfuko mkuu wa serikali utumike. Lakini kama vimetumika vifungu kwa bahati mbaya tu tutalirekebisha hili.

Mhe. Spika, ametushauri Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kwamba vitabu vya mahesabu kidogo vilikuwa na matatizo ilibidi tuvichapishe tena. Hilo tunalikubali na zaidi yeye anatokana na *ceilings* walizowekewa mawizara na hasa pia vile vianzio vyengine vya wafadhili vinavyokuja dakika ya mwisho.

Kwa hivyo, inabidi kwa kweli hakuna uhakika maana yake zile kauli zao zinakuja mwezi wa Mei mpaka mwanzoni mwa Juni, sasa kidogo inatupa matatizo inabidi tuwafuate tuzungumze nao. Sasa yale yote sisi tunaogopa tusichelewe kwa sababu tunaratibu tunaanza kwenye kamati, tunakuja Kamati ya Mwenyekiti wa Wenyeviti, sasa tunaogopa tusije tukachelewa kile tulichonacho tunaanza kumpa *lecture*. Lakini *concern* tumeisikia kwa kweli si vizuri kulifanya buku halafu ukalifumua.

Mhe. Spika, uvujaji wa mapato yanayotokana na sekta ya utalii ushauri wake tumeuchukua na naomba nimfahamishe yeye pamoja na waheshimiwa wengine kwamba kupitia mradi wa kuimarisha ukusanyaji wa kodi *(TMP)* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na wadau wengine imemtafuta mshauri mwelekezi kuangalia ukubwa wa mapato yanayotokana na kianzio hiki pamoja na kujenga uwezo kwa wafanyakazi wa *ZRB* katika uendeshaji na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vianzio vya sekta ya utalii hapa nchini. Kazi ambayo itafanyika mwaka huu wa fedha 2009/2010.
Marekebisho ya kiwango cha kodi ya pango la ardhi. Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti pia alitushauri kuangalia suala la kiwango cha kodi ya pango la ardhi. Kuhusu viwango vya kodi ya ardhi tayari serikali inalifanyia kazi suala hili ambapo Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ameshaiagiza *ZRB* kuvipitia upya viwango vya sasa na kupendekeza viwango vipya vitakavyoendana na thamani halisi ya ardhi kwa hivi sasa. Kwa hivyo, mchango wake tumeusikia, tumeupokea na tayari tumeshaanza kuufanyia kazi.

Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti alitushauri suala la wastaafu kurejeshwa kazini kwa njia ya mkataba. Ushauri wake ni mzuri ni kweli kwamba ikiwa ajira hizi zitakuwa nyingi zitapunguza nafasi kwa vijana. Hilo tunakubali tutazidi kuliangalia.

Lakini Mhe. Spika, naomba kulijulisha Baraza lako tukufu kwamba kuna kada *discipline* kidogo ni ngumu sana lazima tuwe waangalifu na tunazihitajia. Nitatoa mfano madaktari wa binadamu. Kumsomesha daktari peke yake ni miaka 7, aende *internship* mwaka mmoja, apate uzoefu halafu ndio anakwenda *specialization* miaka 2. Sasa yule hata kama kastaafu lakini unamwona bado ana nguvu hatetereki kwenye prescription basi inafaa umchukue. Unajua lazima ufikirie uzoefu ni kitu muhimu sana. Mahakimu, ma-*engineer* lazima tujali ule uzoefu wa exposure wanayoipata kazini ni kitu cha msingi sana. Kwa hivyo, ushauri tumeuhukua kwa baadhi ya kada lakini kada nyengine inabidi tuendelee na watu kama hawa kwa sababu bado tunawahisi wana nguvu na wanaweza kutusaidia.

Mhe. Spika, jengine ni marekebisho ya maslahi ya watendaji wa serikali yamefanywa bila ya kuwepo kwa sera madhubuti. Mhe. Spika, niseme tu

kwamba marekebisho ya mishahara iliyofanywa na serikali yalifanywa kwa makusudi ili kupunguza ukali wa maisha kwa wafanyakazi, huku serikali ikiendelea na taratibu za ufanyaji wa tafiti na kufanya mapitio ya muundo na utumishi serikalini ambao unatarajiwa kukamilika mwezi wa Disemba, 2009. Tulihisi tukingoja tu zikamilike hizi tafiti ukali wa maisha kidogo mkali na watu wanasikitika kwa hiyo twende kidogo kidogo tu. Mhe. Spika, tunaukubali ushauri wake wa tafiti na tutashirikiana kwa pamoja katika kazi zetu.

Mhe. Spika, kiwango cha asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti kinachotokana na mikopo ya *GBS* ni kidogo sana. Mhe. Spika, ni kweli tunakiri na sisi tunahisi hasa hazitutoshi lakini lazima tukubali kwamba kuna mchakato uliowekwa kupitia Tume ya Fedha ya Pamoja juu ya kiwango stahiki kwa mgao na misaada kutoka nje bado hiki ndio kilichowekwa kwa hiyo tunaendelea nacho. Hii ni ya mpito tu. Tunajua kwamba mpito siku zote hautakiwi wende muda mrefu sasa tunalifanyia kazi suala hili la *JFC* kwa pamoja na naamini tutafikia hatima yake si mbali.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kwa kutuhimiza Waheshimiwa Wawakilishi sote na wananchi kwa ujumla kuhusu kudai risiti tunapofanya manunuzi. Kwa kweli hili bado niseme kwamba ni zoezi ambalo tunapata tabu kwa sababu kuna wafanyabiashara wengine anakuuliza hasa, unataka risiti hutaki risiti, kama unataka risiti bei mbali na ukikataa risiti bei mbali. Sasa kwa kweli sote tuwe kitu kimoja kuisaidia nchi yetu kupata mapato basi tudai risiti. Yeye anajua tatizo kwamba akitoa risiti itabidi akaunti kule ichekiwe na itaonekana kauza basi itabidi atozwe kodi zaidi.

Kwa hivyo, tunakubali ushauri wake na huu ni wito maalum kwetu sote, naamini hakutwambia wizara tu, sisi wizara kazi yetu kusimamia lakini kama wawakilishi naomba mtusaidie wenye biashara wote tunao kwenye majimbo yetu.

Mhe. Spika, kwa ufupi hiyo ndio michango ya Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti. Kama nilivyosema kwa kweli tunamshukuru sana kwa sababu yeye amewakilisha wenyeviti wengine wa Kamati za Kudumu za Baraza na haya ni mawazo yao kwa jumla, ingawa tukija kwenye wizara wenyeviti hawa watapata fursa tena ya kuchangia.

Mhe. Spika, naomba sasa nimguse msemaji wa kambi ya upinzani Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi, Mhe. Said Ali Mbarouk. Mhe. Spika, mimi nampongeza kwanza kwa *document* kubwa sana aliyoifanyia kazi. Kwa sababu mtu kuvunja yake akenda mpaka akaangalia haInsard ya miaka ya nyuma kwa kweli nampongeza sana kafanya kazi. Lakini Mhe. Spika, kazi

yake kai-*dilute* kwa sababu vionjo vingi japo vidogo vidogo. Mhe. Spika, nitavitoa hapa kwa uchache tu.

Mhe. Spika, ukurasa wa kwanza anasema tuliwahi kusikia misamiati mingi iliyotutumainisha kwamba safari ya kuelekea nchi ya ahadi kiuchumi ipo karibu. Mhe. Spika, pili anatwambia ni vyema tukakubali kwamba MKUZA umefeli. Ni lini wataalam wa *cluster* hizo wamepewa mafunzo ya kufanya tathmini. Mhe. Spika, MKUZA haujafeli na unaendelea. Namshukuru Mhe. Ali Juma Shamuhuna amegusia kidogo na mimi nitazungumza.

Mhe. Spika, anasema haitoshi serikali kujisifu kwa malengo ya milenia, lakini kila mwaka habari za Wazanzibari kula mizizi na chochoni zinasikika. Mhe. Spika, Mhe. Said Ali Mbarouk anasema bajeti ina sura ya kutotekelezeka, mtu akisema hivyo atakuwa amekosea.

Halafu anasema uduni wa uchumi wa Zanzibar unachangiwa na mambo mawili, udhaifu wa sera zinazofuatwa na SMZ na usimamizi duni wa sera hizo, pia mfumo mbaya wa Muungano. Mhe. Spika, viongozi wa SMZ wanajaribu kujipapatua tu katika makucha hayo lakini ujasiri umekuwa dhaifu. Akanukuu hoja ya asilimia 4.5, mgao wa faida ya *BOT* na *GBS*.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba si jambo baya kwa sababu haya ni maoni yake Mhe. Waziri Kivuli na kama alivyosema yeye katoa *alternative budget* (bajeti mbadala). Lakini namshukuru sana Mhe. Ali Juma Shamuhuna, sasa hiyo bajeti mbadala itatumika wapi? Kwa sababu bajeti iliyopo sasa ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi.

Kwa hivyo, kwa sasa hivi kwanza namuomba hii bajeti mbadala aiweke pembeni tuisikilize hii na itolewe maoni hii, aichangie hii, atuoneshe *the way forward*. Lakini humu hakutuonesha katukosoa sana tunamshukuru. Hii bajeti mbadala aliyoiweka hapa nasema yake ndio haitekelezeki kabisa. Hii naweza kusema wazungu wanaita *utopian, It doesn't exist.*

Mhe. Spika, mawazo yake mengine ya uchambuzi mimi tumeyakubali, tumeyapokea na tutayafanyia kazi. Lakini naomba nimgusie kwenye MKUZA, amesema MKUZA tumefeli. Mhe. Spika, kuna kitabu hiki cha Mkakati wa Ukuzaji Uchumi Zanzibar (MKUZA) 2006 mpaka 2015 tulikisambaza nafikiri mwaka jana. Ningeomba ninukuu kidogo azma ya MKUZA na vipi tunavyouendeleza.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na program ya mageuzi ya kijamii na kiuchumi iliyoanzishwa mwaka 1964 ndio maana tunasema Mapinduzi Daima. Mageuzi ya kijamii na kiuchumi bado

yanaendelea tokea yalipoanzishwa na mwasisi wetu mwaka 1964. Msisitizo wa mageuzi haya ulikuwa kwenye uimarishaji wa huduma za kijamii kwa wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kupunguza umasikini uliokithiri.

Hatua kadhaa za kuimarisha usimamizi wa uchumi zilichukuliwa kwa lengo la kufikisha huduma bora kwa wananchi. Sera za kiuchumi zilielekezwa katika kutoa fursa pana zaidi kwa sekta binafsi kwenye shughuli mbali mbali za biashara na uwekezaji. Serikali ilibakia na wajibu wa kujenga mazingira mazuri yenye kutoa fursa zaidi kwa sekta binafsi na makundi mengine. Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilijihusisha na ujenzi wa miundo ya kiuchumi na kuweka mfuko wa kisheria na sera zinazoimarisha mazingira bora ya biashara, ukuaji wa uchumi, ongezeko la mapato na ubora wa huduma za kijamii.

Mhe. Spika, huu ndio MKUZA na utaona kwa kweli uko *up to date* na hotuba yetu mwaka huu. Yaani tunakwenda kwa kuongozwa kama walivyosema waheshimiwa na nilivyosoma hotuba yangu kwa kuongozwa na MKUZA, kwa kuongozwa na Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, kwa kuongozwa na Dira ya 2020. Sasa huu ndio MKUZA na hatujafeli, kwa kweli tunakwenda vizuri tunapanga na sasa hivi tunafanya tathmini. Hawa washiriki wenzetu wa maendeleo kwa kweli wanatuunga mkono vizuri, wao wanatwambia hasa bila ya MKUZA sijui mngekuwa wapi. Mhe. Spika, lazima tujisifu na tuwasifu wataalam wetu, wachumi wetu wanafanya kazi nzuri. Tusiseme kwamba wataalam Wazanzibari, hapana ni hao hao, *we should feel proud over our experts.* MKUZA ndio huu na tumeutayarisha wenyewe na huu ni *multi-sectoral* vyama vyote wameshiriki, wadau wote, *private sector* wote wameshiriki. Sasa nasema haujafeli bado uko *strong* na tunauendeleza vizuri.*(Makofi).*

Mhe. Spika, nimejitahidi kuuelezea MKUZA na sitaki nichukuwe muda mwingi zaidi lakini Mhe. Said alizungumzia suala la mfumko wa bei kutofikia asilimia kumi. Napenda nifahamike kwamba wastan wa mfumko wa bei kwa mwaka hapa Zanzibar haujawahi kufikia asilimia 20 yeye amesema umefikia asilimia 24. Mwenendo wa mfumko wa bei umeelezwa vizuri katika bajeti ya Serikali mwaka 2009/2010 ambapo kiwango kikubwa zaidi kimeripotiwa kwa mwaka 2008 kilifikia asilimia 20.6. Hii imesababishwa zaidi na ongezeko la bei ya mafuta ya nishati.

Hata hivyo katika miezi ya hivi karibuni mfumko wa bei uliendelea kushuka kwa kasi sana, kama hali itaendelea kama hivi basi sasa matarajio ya mfumko wa bei ni kushuka zaidi hata ya chini ya kile kiwango kilichokisiwa cha asilimia 10 kwa mwaka 2010. Na hii inajionesha wazi sokoni. Bei ya mchele ilivyo hivi sasa, bei ya saruji, juzi tulikuwa tukilalamika saruji bei yake leo *alhamdulillahi* 12,000 unapata mfuko wa saruji. Kwa kweli ni jambo zuri la

kupigiwa mfano na chakula nacho ushindani kwenye *market* leo *brand* za mchele aina tofauti, *brand* za saruji aina tofauti, ushindani uko kwenye soko letu. Leo hii inaonesha wazi kwamba soko letu imenawiri na *inflation* inashuka.

Utekelezaji wa malengo ya mileniam, Mhe. Said pia alizungumza suala la utekelezaji wa malengo ya mileniam. Nisema kwamba malengo ya utekelezaji wa malengo ya mileniam yanakwenda sambamba na utekelezaji wa MKUZA. Mwaka 2008 Serikali imefanya mapitio ya utekelezaji wa MKUZA na vile vile kujipima kwa mujibu wa malengo ya mileniam. Ripoti ya utekelezaji wa MKUZA imeshachapishwa na kusambazwa nchini kote, kama Mheshimiwa hajaipata basi naomba atujulishe tumpatie kwa kweli ni vizuri kuwa nayo hii ripoti.

Ripoti ya Utekelezaji kwa mujibu wa malengo ya mileniam karibu pia itachapishwa. Mhe. Spika, katika mwaka 2009 utafiti unafanywa kupima maendeleo ya binadamu yaani Zanzibar Human Develop Report. Ripoti inatarajiwa kuchapishwa mwisho wa mwaka. Kamati ya Mawasiliano ya Mkuza itafanya kazi ya kuitangaza ripoti hizi.
Pia Mhe. Spika, baada ya kukamilika kwa ripoti husika zitasambazwa nchi nzima kama zilivyosambazwa ripoti ya MKUZA. Azma ya Serikali kuona kwamba bajeti ya kawaida inakidhiwa na makusanyo ya ndani. Mhe. Spika, ninamshukuru tena Mhe. Shamhuna alizungumzia vipi tunavyoweza bajeti yetu ya ndani kukidhi mahitaji yetu na kuendesha Serikali vizuri.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado inaendelea na azma yake ya kuona kwamba bajeti ya kawaida inakidhiwa na makusanyo ya ndani. Hili linadhihirishwa na takwimu zilizopo ambazo zinaonesha kuwa nakisi kati ya mapato ya ndani na matumizi ya kawaida kuanzia mwaka 2006/2007 hadi mwaka 2009/2010 inaendelea kupungua kama ifuatavyo:-

Nakisi kati ya bajeti ya mapato ya ndani na matumizi ya kawaida kwa mwaka 2006/2007 mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 83,000,000,000 matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 110,000,000,000 nakisi ilikuwa kama 27. Na mwaka 2007/2008 tulikuwa na kama shilingi bilioni 114,000,000,000 matumizi 140 nakisi kama 25,000,000. 2008/2009 mapato ya ndani yalikuwa kama shilingi bilioni 134,000,000,000 matumizi ya kawaida shilingi bilioni 149,000,000,000 nakisi kama shilingi bilioni 14,000,000,000.

Mwaka 2009/2010 shilingi bilioni 159,000,000,000 matumizi ya kawaida 172, nakisi shilingi bilioni 12,000,000,000 utaona *trend* ilivyokuwa inashuka. Kwa mtiririko huo inaonesha dhahiri kwamba SMZ imefanikiwa na azma yake ya kuona kwamba bajeti ya kawaida inakidhiwa na mapato ya ndani. Na hivyo

ndivyo tunavyo bajeti, kwa kweli tunajitahidi sana kuhakikisha kwamba bajeti yetu haina *deficit* kubwa.

Mhe. Spika, washirika wa maendeleo wamechangia asilimia 35.3 ya makadirio kwa kipindi cha miezi 9 na yanatarajiwa kufikia asilimia 40 ya makadirio ya mwaka mzima ya shilingi bilioni 173,000,000,000 ambayo ni sawa na shilingi 69.5 bilioni. Kigezo gani kilichotumika cha kuweka makadirio ya shilingi bilioni 199,000,000,000 aliuliza Mhe. Said.

Niseme kwamba kabla ya kuingizwa mchango wa wahisani katika bajeti huwepo na mawasiliano ya kutosha kutoka kwa washirika wa maendeleo wakithibitisha kutoa michango yao kwa sekta husika. Mhe. Spika, kigezo kilichotumika kuweka makadirio ni ahadi za mchango zinazotolewa na washirika wa maendeleo husika.

Aidha naomba nimtoe wasiwasi Mhe. Waziri Kivuli na wananchi wote kwamba kwa ujumla wasiwe na hisia kuwa bajeti hii haitekelezeki. Bajeti hii imetayarishwa kitaalamu ninakuhakikishieni kwamba inatekelezeka.

Mhe. Spika, bajeti ina sura ya kutekelezeka ninafikiri nimeshasema kwa ufupi sina haja ya kufafanua zaidi. Naomba nitoe mifano iliyopo hai tu leo tunalipa mishahara kwa wakati, tunalipa viinua mgongo, Wizara za Serikali zinakwenda na hatujafikia watu kufa njaa hapa nchini mwetu tunashukuru. Kunakuwa na *shortage* za vyakula lakini Serikali ina-*intervene.*

Serikali kwa kweli inajitahidi inapunguza kodi kwa makusudi ili wananchi wetu wapate kununua bidhaa kwa bei ambayo wanaimudu ili hali isiwe ya kuweza kutomilikika. Kwa kweli tunashukuru niseme kwamba lazima tutoe pongezi kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jinsi tunavyokwenda na kuienesha Serikali na kutosheleza haja za wananchi kwa sera zetu. Na lazima tukiri kuwashukuru sekta binafsi mchango wao huu wa biashara.

Halafu Mhe. Waziri Kivuli aliulizia suala la ajira katika nchi kuinua kipato, kuongeza matumizi, kukuza biashara, kuongeza ulipaji wa kodi na huinua uchumi. Ni kweli katika ukurasa wa 4 kifungu cha pili cha hotuba ya Mhe. Waziri Kivuli, nikuu zote zilizofanywa na Mhe. Waziri Kivuli tukizichambua kwa kina basi utakuta zina malengo mawili makubwa.

Kwanza Serikali kukubali jukumu lake la kuandaa mazingira mazuri za kuongeza nafasi za ajira nchini kwamba linashughulikiwa kwa nguvu zote. Pili pamoja na kukubali jukumu hilo lakini Serikali pia imegundua kwamba bado kuna ongezeko la vijana wanaomaliza masomo ambao wanahitaji ajira.

Mhe. Spika, bado itaendelea kuwa changamoto kwa Serikali kwa vile kila mwaka kuna ongezeko la vijana wanaomaliza masomo yao.

Mhe. Spika, Serikali inaona umuhimu wa raslimali hii kutoa ajira na kuongeza tija nchini na ndio maana bado juhudi zinaendelezwa za kuandaa mipango mizuri na endelevu kushughulikia raslima hii.

Mhe. Spika, tafiti zinaonesha kwamba Serikali inaendelea kuwa Muajiri Mkuu katika ajira rasmi nchini. Aidha kuna waajiriwa wengi katika sekta isiyo rasmi ambapo zaidi ya asilimia sitini ya hao wameajiriwa katika kilimo.

Kwa upande wa taasisi binafsi sekta ya utalii na biashara zimechangia vizuri katika ajira kwa kuajiri zaidi ya asilimia 43 ya wafanyakazi waliorodheshwa na ZSSF kwa mwaka 2007.

Kutokana na mipango na Sera zilizopo za ajira inatarajiwa ajira katika sekta ya biashara na utalii kuongezeka katika kufikia wafanyakazi 40,000 ifikapo mwaka 2015.

Mhe.Spika, pamoja na hatua hizo kwa kuwa bado mahitaji ya ajira yapo na yataendelea kuwapo kama ilivyotokeza hapo kabla, Serikali bado itaendelea kufanya juhudi zaidi na kutoa kipa umbele katika uekezaji binafsi ili kupunguza ukosefu wa kazi.

Aidha mafunzo stadi na amali yatazidi kuendelezwa na taasisi husika ili vijana wetu waweze kujiajiri.

Mhe. Spika, tofauti nyengine Mhe. Waziri Kivuli alizungumzia masuala ya uhusiano baina ya kukua kwa sekta ya kilimo na mfumko wa bei. Ninafikiri hili Mhe. Ali Juma Shamuhuna kalieleza vizuri na tena kwa ufasaha kabisa na sitaki tena kulirejea.

Mhe. Spika, usahihi wa ukusanyaji wa takwimu na matumizi yake. Usahihi wa matumizi takwimu ni jambo muhimu na la msingi katika mipango ya maendeleo. Utayarishaji wa sera na kusimamia na kutathmini mipango mbali mbali ya kijamii na kiuchumi. Ili kufanikisha hili serikali ilitayarisha sheria mpya ya takwimu ya mwaka 2007 ambayo ilipitishwa na Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, si jambo sahihi ya kwamba takwimu zinazokusanywa kupitia mabuku ya Masheha ndizo zinazotumika kutoa viashiria vya kiuchumi. Katika ukusanyaji wa takwimu zipo njia za kitaalamu zinazotumika, njia hizo zinazotumiwa na wataalamu wetu. Mbali ya utafiti wa matumizi ya mapato ya

Kaya uliofanywa mwaka 2004/2005, serikali kupitia Afisi ya Mtakwimu Mkuu imeendelea kufanya tafiti mbali mbali.

Tafiti zinazofanywa ni mwendelezo wa utekelezaji wa kalenda ya utafiti ambayo inaishia mwaka 2012, wakati itakapofanyika sensa ya kitaifa ya watu na makaazi. Kwa kawaida tafiti hizi huwa zinafanywa kila baada ya miaka mitano. Katika kipindi cha miaka 2000, tafiti zilizofanyika ni kama hivi zifuatazo:-

- sensa ya viwanda ya mwaka 2001
- sensa ya watu na makaazi 2002
- sensa ya kilimo 2003
- sensa ya taasisi za biashara 2004
- utafiti wa hali za watu na afya 2004/2005
- utafiti wa mapato na matumizi ya Kaya 2004/2005
- utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi 2006
- utafiti wa hali ya viashiria ya ukimwi na malaria 2007/2008
- utafiti wa orodheshaji wa taasisi za biashara 2008
- utafiti wa kila mwaka *(Annual Economic Survey)*

Kwa mwaka huu Mhe. Spika, 2009 tafiti zinazohusiana na sensa ya kilimo na matumizi ya mapato na Kaya zinaendelea. Aidha utafiti wa hali za watu na afya kwa mwaka 2009/2010 maandalizi yake yapo katika hatua za mwisho na unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwaka huu 2009.

Mhe. Spika, takwimu pia zinazotokana na tafiti hizi na nyengine ndizo zinazotumika katika mipango yetu mbali mbali ikiwemo matayarisho ya bajeti. Mhe. Spika, alizungumzia hali ya utumishi serikali jambo linalohitaji mageuzi makubwa. Kuna haja ya serikali kufanya tathmini ya utumishi kwa umma. Niseme tu kwamba kwa hatua ya awali serikali inafanya mapitio ya muundo ya utumishi serikalini unaotarajiwa kukamilika mwezi Disemba mwaka huu.

Kwa uchache au kwa ufupi nimalizie hapa kwa Mhe. Waziri Kivuli lakini kama kuna mambo nimeyaacha basi namuomba kwamba asione kuwa nimeyadharau, lakini kwa sababu ya muda tu lakini tumejitahidi, na *issue*s nyengine kazungumza pamoja na Waheshimiwa wengine tutazigusa kwa pamoja.

Ujenzi wa barabara za Pemba ambazo Mhe. Mohamed Ali Salim kazungumza hili lakini kwa kweli nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. Machano Othman Said kwa ufafanuzi wake mzuri na ufasaha kuhusu suala zima la sekta ya mawasiliano hasa barabara.

Nafikiri kagusa sehemu zote kabisa na Mhe. Mkongwe Nassor naye ninaamini karidhika kwamba mambo yapo njiani, chungu kinapikwa na mule ambamo kidogo hamupitiki hivi sasa basi tutafanya mpango tumuwezeshe kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa.

Kwa kweli Mhe. Machano tunamshukuru na niseme kwamba ile azma yetu kwamba safari hii ni bajeti ya miundo mbinu ninafikiri tumeiona ni bajeti ya miundo mbinu, kwa sababu hata rafiki yangu Mhe. Said Ali Mbarouk safari hii hakuzungumzia kabisa ujenzi wa barabara ya Wete/Gando, anajua kwamba mambo yameshawiva sasa hivi.

Hata Mhe. Mulla na yeye ninafikiri barabara ya Wambaa hakuzungumza mwaka huu. Kwa hivyo kaona haya mambo yameshawiva na Mhe. Abass Juma Muhunzi na yeye pia barabara yake pia kila mwaka anaizungumza na yeye mwaka huu hakuizungumza, kaigusia kidogo lakini anajua kwamba mambo yameshawiva.

Sasa niseme tu kwamba tunapopanga basi tuwe na subra, mipango unajua ni hatua, inakuja kidogo kidogo mpaka inatekelezwa. Kwa hivyo, Mhe. Abubakar ninakumbuka alikuwa ananimbia unatuletea mpaka *press conference* hapa. Ndio ninajaribu ku-*convince* kwamba haya mambo hatudanganyi. Sasa hizi ahadi zetu Mhe. Abubakar kwamba zinatekelezwa na ninaomba tuwe pamoja tusaidiane tufanikishe haya mambo.

Mhe. Spika, watu wengi walizungumzia suala la kwamba tumepoteza udhibiti wa sera za fedha *(monetary policy)* ambazo ni muhimu katika udhibiti wa uchumi. Waheshimiwa waliona kwamba labda tumepoteza mwelekeo tunategemea sana Tanzania Bara kwa mambo haya.

Mimi niseme kwamba si kweli lakini lazima tufahamu sera ya fedha ni sera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Msimamizi mkuu wa sera hii ni Benki Kuu ya Tanzania ambayo ni mshauri wa serikali zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Sisi "*we are a part a parcel"*, benki ile ni '*part a parcel'* yetu na sisi tumo, japo wenzetu kidogo wengine hawataki lugha hii, lakini huo ndio ukweli na hili tunalolizungumza kuwathibitishia ukweli huu. Sasa wanaposhauri nchi hizi basi na sisi pia tunashauri. Juzi tu Gavana wa Benki Kuu tulimwita hapa, alikuja akatutolea semina nzuri kwenye *cabinet* na ninafikiri tunafanya mipango, unajua yupo *busy* sana aje tumuombe atoe ile *stimulus package* au hali kwa ujumla kwa waheshimiwa.

Tunafanya mipango kidogo sisi hiyo Baraza la Mapinduzi kumpata basi tumehangaika muda mrefu sana lakini ninaahidi kwamba tutajitahidi Mhe. Spika, tumpate na yeye aje kidogo atuzungumze au atupe hasa huu mtikisiko wa uchumi pamoja na hii *stimulus package.*

Mhe. Spika, katika maandalizi ya sera za fedha Zanzibar huwakilishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi Zanzibar. Viashiria vya sera ya fedha ni vya nchi nzima na sio Tanzania Bara kama inavyodaiwa. Hii ni kutokana na mzunguko wa fedha unaotumika unajumuisha fedha ziliopo katika mzunguko pamoja na fedha ziliopo katika mabenki ambayo yapo nchi nzima ikiwemo Zanzibar.

Vile vile sera ya fedha *(monetary policy)* haina athari ya moja kwa moja katika kuanguka kwa thamani ya shilingi, hii ni kutokana na mfumo wa kiwango cha ubadilishaji wa fedha za kigeni *(exchange rate)* uliopo, ni ule wa kuelekea yaani *floating exchange rate* ambao unategemea nguvu ya soko la fedha la kigeni *(market forces)*

Mhe. Spika, suala jengine kama nilivyosema Waheshimiwa walizungumza ni suala la ongezeko la idadi ya watu mbali ya wale wanaoingia nchini lakini ni ongezeko la idadi ya watu kwa ujumla. Kasi ya ongezeko ya idadi ya watu ni kubwa, tunakubali ongezeko hili linasababishwa zaidi ya ongezeko la uzazi ambalo ni 5.6.

Aidha, kuimarisha kwa huduma za afya hasa za mama na watoto kunachangia katika ongezeko hili. Yale maradhi madogo madogo ya akinamama sasa yamedhibitiwa. Kwa hivyo tunashukuru akinamama alhamdullahi afya ni nzuri, wanakula vizuri basi unajua tena utajiri wetu, tunasema utajiri wa maskini ni watoto. Lakini sasa tusiende huko, tupate watoto lakini tuweze kuwashughulikia ipasavyo.

Katika kulishughulikia hili serikali imeifanyia mapitio sera ya idadi ya watu ya mwaka 2003. Lengo ni kupunguza kasi ya ongezeko la watu kwa kutumia mbinu bora za mpango wa idadi ya watu na masuala ya maendeleo. Hivi sasa serikali inayaingiza masuala ya idadi ya watu katika mipango yote ya maendeleo pamoja na kusambaza huduma bora za uzazi wa mpango na salama.

Kushuka kwa kiwango cha ukuaji wa pato la taifa. Mhe. Spika, kiwango cha ukuaji wa pato la taifa hakijashuka kwa mwaka 2008. Kilichojitokeza ni kupungua kwa kasi ya ukuaji wa pato la taifa ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa mwaka 2007. Hali hii imetokana na athari za kukatika kwa umeme hapa Zanzibar, ujenzi wa bandari na mtikisiko wa fedha na uchumi duniani.

Mhe. Spika, suala jengine kama nilivyosema Waheshimiwa wengi waliuliza ni suala la kutosafirisha matunda hasa ya embe. Ninakumbuka Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Makame Mshimba wengi waliliulizia hili. Sababu kubwa ya kushindwa kutosafirisha zao la embe ni kutokana na kuathiriwa kwa zao hilo na nzi wa embe.

Mhe. Spika, nilisema kwamba tatizo hasa ni hawa nzi wa embe au wanaitwa *fruit fly*. Kiutaratibu nchi iliyoathiriwa haiwezi kusafirisha matunda yake katika nchi nyengine. Nzi wa matunda wameenea takriban katika sehemu zote za visiwa vyetu. Hata hivyo serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira inaendelea na jitiahda za kutokemeza wadudu hawa kwa kuweka mitego yenye dawa maalum katika sehemu tofauti mijini na vijijini. Hivi karibuni jumla ya shilingi milioni 200 zilitolewa na mradi wa *MACEMP* kusaidia juhudi za kuangamiza wadudu hawa. Vile vile wananchi hasa wakulima wa zao la embe wanashirikishwa kikamilifu katika jitihada za kuangamiza nzi hawa wa embe.

Kilimo cha mwani. Mhe. Spika, kama nilivyosema kilimo cha mwani nacho kimechagiwa takriban na Waheshimiwa wengi kwamba kidogo ni kilimo kigumu na hasa akinamama wetu wanapata shida lakini bei ni ndogo. Ninachoomba kusema Mhe. Spika, ni kwamba serikali kupitia Wizara yake ya Kilimo inaendelea na juhudi ya kutafuta fursa za uwekezaji wa viwanda vya usarifu wa mwani.

Katika mwaka 2007/2008 ujumbe wa Wizara ya Kilimo ulikwenda China kwa mazungumzo na serikali ya nchi hiyo. Makubaliano ya mwanzo ya kuanzisha viwanda vya usarifu wa mwani pamoja na kufanyika utafiti wa mwani wenye bei nzuri unaostawi hapa Zanzibar yamezingatiwa. Makubaliano ya mwanzo yamefikiwa na hatua za usoni zinazingatiwa.

Wasi wasi wa bajeti ndogo iliyoekwa kwa kuendeleza zao la karafuu. Hili nalo limechangiwa na Waheshimiwa wengi, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Zakiya Omar Juma.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba shilingi milioni 60 ni kidogo sana kwa kuhudumia zao la karafuu ambalo ni kuu la taifa. Hata hivyo kiasi hicho cha fedha kwa mwaka huu kimetengwa kugharimia kazi ya uzalishaji wa miche pamoja na kuandaa mkakati mpya wa utafiti na elimu *organic* kwa ajili ya kuliendeleza zao hilo. Siku hizi kuna *approach* hii mpya ya *organic farming* na ndio inayotakiwa hasa kwa baadhi ya nchi tunazosafirisha karafuu zetu.

Hivyo kuanzia mwaka 2010/2011 serikali itatanua shughuli za kuimarisha zao la karafuu. Lakini suala la msingi tunaloliomba Waheshimiwa tuzidi

kuwahamasisha wananchi wetu kwamba waichukue miche na waipande. Baadhi ya maeneo inafurahisha miche imepandwa au inaendelea kupandwa na inanawiri. Nitatoa mfano Kangani au Wambaa, Donge bado tunashukuru watu wanapanda, lakini ninaomba tuzidi kuwahamasisha. Kuna mikarafuu mingi mikongwe na bado kuna mapengo. Sasa miche inashangaa mpaka dakika ya mwisho.

Ningeliomba sana Waheshimiwa tusaidiane katika majimbo yetu haya kwa kilimo cha mikarafuu yakienemeka kujaza mkarafuu, hatujui keshokutwa bei inaweza ika-shoot ikenda juu tukaja kuzitafuta karafuu. Kwa hivyo si kama serikali imedharau kwa kutoa bajeti ndogo la! a! la! bado inathamini juhudi hizo. Kulikuwa kuna hoja na hii hasa aliuliza Mhe. Haji Faki Shaali kwamba Wizara ya Fedha na Uchumi huwa anaomba idhini ya kukusanya fedha za ndani na fedha za nje na kuomba idhini ya matumizi ya kazi za kawaida tu na maendeleo, Mawaziri wengine huwa hawasemi hivyo, sasa yupo sawa?

Mhe. Spika, kuhudu idhini kuomba idhini ya matumizi na kukusanya fedha za ndani na za nje, kwanza katika mchanganuo wa bajeti ambapo vifungu vya wizara zote vinaoneshwa, wizara huomba idhini kwa fedha za kawaida na matumizi ya maendeleo ambapo ndani ya matumizi ya maendeleo zimo hizo fedha za nje.
Pili Waziri anayeshughulikia fedha na uchumi kuomba idhini ya kukusanya fedha za nje ni sahihi, kwa sababu kwa mujibu wa taratibu yeye ndiye dhamana wa utafutaji wa raslimali kutoka nje ya nchi kwa niaba ya serikali. Kwa ufupi tu niseme hivyo.

Mhe. Spika, Mhe. Abubakar na Waheshimwa wengine wamezungumzia kuhusu sekta ya uvuvi. Ninakumbuka Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Ame Mati Wadi, Mhe. Ali Haji Ali na wengineo kwamba sekta ya uvuvi ni miongoni mwa sekta ambazo ukuaji wake ni wa kuridhisha kwa mwaka 2008. Ukuaji wa sekta ya uvuvi umekuwa kwa asilimia 5.2.

Hata hivyo, maelezo ya kina yatatolewa na Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira wakati atakapowasilisha bejeti yake. Kwenye hii ya serikali tugusie lakini tumuachie yeye mwenyewe uwanja Mhe. Waziri wa Kilimo kwa sababu hii ni sekta kubwa hapa kwetu, basi atakapokuja yeye basi atoe *elaboration* kubwa sana.

Mhe. Spika, jee serikali inaelewa ibara ya 115 ya Katiba ya Zanzibar. Mhe. Salmin Awadhi alituuliza hilo. Niseme tu kwamba ibara ya 115 inaweza masharti ya fedha yahusuyo mambo ya muungano, kuhusu uwezo wa kutumia kasma kwamba hakuna fedha itakayotumiwa katika sehemu hii hadi kwanza Tume ya Pamoja ya Fedha inayohusu mambo ya muungano kama

ilivyoanzishwa na Katiba ya muungano imechambua mapato na matumizi ya shughuli za muungano na kutoa mapendekezo yake kwa vyombo vinavyohusika juu ya mgawanyo wa matumizi hayo. Pili Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huyakubali mapendekezo hayo na mgawanyo wake. Kwa hivyo niseme tu kwamba tunayakubali.

Kupotea kwa mapato kupitia kwa misamaha Mhe. Ali Abdulla Ali aliuliza hili. Mhe. Spika, misamaha hutolewa kwa mujibu wa sheria na utaratibu uliopo ambapo kupitia kamati maalum ya kumshauri Mhe. Waziri iliopo *ZRB* juu ya mapendekezo juu ya kustahiki au kutostahiki kwa maombi ya misamaha iliyowasilishwa na hupelekwa kwa Mhe. Waziri, ndipo Waziri anapoweza kutoa misamaha hiyo.

Mhe. Spika, mingi ya misamaha inayojitokeza ni ile inayoambatana na uwezekezaji wa miradi ya kijamii, miradi ya serikali. Hii miradi mikubwa yote kwa mikataba kwamba kodi wasamehewe na ndio miradi hasa inayochukua sehemu kubwa sana. Sasa hii kwa kweli hatuwezi kuiepuka tunajifunga wenyewe. Miradi ya afya, barabara, ujenzi wa uwanja wa ndege, yote hii miradi mikubwa lazima wanasema kwamba hizi ni pesa za watoza kodi za nchi zao basi na sisi huwa tunasema huku musitoze kodi tena, lakini pia kurahisisha hiyo investment yenyewe inavyofanywa pia tuwasamehe kodi.
Pia kwa mujibu wa sera zetu za uwekezaji hawa wawekezaji wanasamehewa, wanapoekeza wanasamehewa mali ghafi. Ndio maana miradi hii mingi ya ZIPA utakuta tunaisamehe. Kwa hivyo, kwa kweli mambo yote haya yanafanywa ndani ya sheria.

Mhe. Haji Mkema Haji alitaka kujua suala la barabara zinazofanywa matengenezo madogo madogo ni zipi. Ninafikiri hili Mhe. Machano Othman Said kalieleza vizuri tu barabara zake za Koani, Jendele, Ungujaukuu, ninafikiri kalieleza na sina haja ya kulirejea.

Miradi midogo midogo. Mhe. Ali Abdulla Ali, Mhe. Makame Mshimba na Waheshimiwa wengi sana waliulizia suala hili. Utaratibu uliopo wa kutoa fedha za miradi midogo midogo ya wananchi unategemea na jitihada zao za kujiletea maendeleo katika maeneo yao. Serikali husaidia kumalizia miradi iliyoanzishwa, naomba kusisitiza hapa kwamba serikali husaidia kumalizia miradi iliyoanzishwa kutokana na maombi yaliyotumwa Wizara ya Fedha na Uchumi, hivyo serikali inawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wahamasishe wananchi waendelee na jitihada za kuibua miradi na serikali haitosita kusaidia jitihada hizo kama maombi hayo yatakavyotumwa.

Lakini lazima niwashukuru Waheshimiwa kwa ushauri walioutoa kwamba ile pesa iliyowekwa hivi sasa ya miradi basi igaiwe kwa majimbo yote.

Tumeupokea ushauri huo na tutaufanyia kazi. Lakini naomba tu kwamba sio kama hata kama jimbo halina mradi itapelekwa tu ile pesa, kuna utaratibu wetu maalum umeekwa wa kuli-*qualify* wa kupata hizo pesa. Utaratibu huo upo tu baadae ninafikiri nitatoa *photocopy* Mhe. Spika, ili Waheshimiwa waweze kuona zile taratibu za ku-*qualify* kupata. *Ceiling* au ukomo umeekwa ni shilingi milioni tano.

Pia serikali kama nilivyosema inasaidia sehemu ya fedha ya mradi huo na mradi utakaoombewa fedha uwe unatoa mwelekeo wa kukamilika na zisiwe za kuanzia. Miradi ya skuli, usambazaji umeme, usambazaji maji, ujenzi wa barabara za ndani, ujenzi wa vituo vya afya, hiyo yote inazingatiwa.

Niseme tu Mhe. Hijja Hassan kwamba sisi wizarani kule hatuna habari kama kuna watu wananyofoa zile pesa au ili upate basi wapate *percentage*. Sasa yeye kama mradi wake kafanyiwa hivyo au labda huko huko Mtangani kama alivyosema lakini kwa Wizara ya Fedha na Uchumi pale sisi hatujalipata hilo. Lakini kama lipo basi tuje tuzungumze kwamba tuje tuweke dawa lisitokee hilo. Kwa kweli sisi pale wizarani maana pesa yenyewe shilingi milioni tano ukizinyofoa mbili tu zimebaki ngapi.

Mhe. Spika, barabara ya Bumbwini Mhe. Said Khelef na Mhe. Mkongwe Nassor kwa kweli sina haja ya kulirejea, kama nilivyosema Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi ameshazungumzia kwa ufasaha kabisa.

Kushuka kwa idadi ya watalii kutaathiri vipi sekta ya utalii Zanzibar. Mhe. Spika, ni dhahiri kushuka kwa idadi ya watalii kutaathiri sekta ya utalii hapa Zanzibar kwa kiasi kikubwa. Utalii ni sekta yenye *multiply effect*, yaani athari zake zinatugusa sote au zinatapakaa. Hivi sasa inaonekana katika nyanja zote za uchumi. Kuanguka kwa idadi ya watalii kutakuwa na athari kubwa sio tu kwa pato la taifa tu lakini kunaweza kuathiri kwa sekta nyingi kama vile ajira, uwekezaji, hifadhi ya mazingira na utamaduni.

Lakini uingiaji wa watalii nchini vile vile unaweza ukasaidia sana uhusiano baina ya nchi, upatikanaji wa misaada, mitaji, masoko na kuifanya nchi inayotembelewa kuwa maarufu ulimwenguni. Athari ya misukosuko ya fedha ulimwenguni unaweza kubainika baada ya kufanywa utafiti.

Mhe. Spika, kwa kweli athari hii kwetu utalii utakapoathirika kama nilivyosema utakuwa na hiyo *multiply effect*, yaani utatugusa sote. Lakini bahati nzuri tulipata nafasi ya kuzungumza na Naibu Waziri wa Biashara wa Italy. Alipokuja alitupa faraja kidogo kwamba wao hasa Italy hawakugusika sana na ule mtikisiko wa kifedha, yaani zile *policy* zao walizirekebisha mapema

za kifedha. Kwa hivyo hawakufuata mfumo wa Kimarekani na wa Kijapan kama wengine.

Kwa hivyo ninasema kwa kweli wanatarajia hali ya *flow* ya watalii kwetu haitokuwa mbaya, lakini sasa hatujui mambo haya hayatabiriki. Lakini yeye alituhakikishia kwamba soko lenu la utalii tunatarajia kuwa zuri. Lakini tunamshukuru Mhe. Waziri wa Biashara, Utalii na Uwekezaji hivi majuzi tu alifanya *promotion tours* nchi za Ulaya na Urusi huko, kama alivyosema Mhe. Ali Juma Shamuhuna kwenda kufungua masoko mapya.

Kwa hivyo kwa kweli serikali inajitahidi sana haidhuru misukosuko ipo lakini tuhakikishe kwamba tusikae tukakaa tukafunga mikono, tukasema watakuja tu. Huko kidogo wengine wameathirika na wengine hawakuathirika na wanahitaji tutoke tukawahamasishe na kutafuta masoko mapya.

Mhe. Spika, msitu wa Kiwengwa ambao Mhe. Makame Mshimba aliuzungumzia. Niseme tu kwamba Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Mazao ya Biashara, Matunda na Misitu inaendelea na juhudi ya kusimamia na kuulinda msitu mkuu wa Kiwengwa. Hivi sasa karibuni wizara kupitia idara hiyo imeandaa mpango mkuu wa usimamizi wa msitu huo kwa mwaka 2009/2010.
Ningemuomba sana Mhe. Mshimba kwamba yeye kama Mwakilishi angekwenda akazungumza na Mhe. Waziri na Mkurugenzi wa Msitu wakaona hali ilivyo kule, kwa sababu hili suala ni nyeti na zito na linahitaji nguvu za pamoja, sio mwengine analinda na mwengine anaharibu. Ningemuomba yeye kama Mhe. Mwakilishi na mwenye wananchi basi atoke aende wizarani wakae pamoja.

Kuhusu kilimo cha mwani Mhe. Haji Mkema alitaja kujua tu kwamba kinaendelea kufanyiwa utafiti. Niseme tu kwamba yeye alisema kwamba hakina *focus.* Lakini niseme tu kwamba kilimo hiki kinafanyiwa utafiti ili kupata mazao na mbegu zitakazostawi katika maeneo haya. Utafiti unafanywa pia kwa mazao mengine ili kuweza kusaidia kupata au kunyanyua tija kwa wakulima wetu.

Mhe. Mkongwe Nassor Juma alionesha *concern* kubwa kwamba madawa yanauzwa kwa mlango wa nyuma, mengine yanakwenda Tanzania Bara na yanakuja kununuliwa hapa Zanzibar. Ninataka kusema tu kwamba hiyo taarifa tumeisikia na kwa kweli Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha na Uchumi hatujaipata, lakini tunaomba mashirikiano tusaidiane na wadau wote katika kulikabili tatizo hili.

Fedha za kilimo Tanzania Bara, kwa nini hazionekani Zanzibar. Mhe. Spika, kilimo sio suala la muungano. Misaada yote ya kilimo kwa upande wa Tanzania Bara inaingia katika mfuko mmoja unaoitwa *basket fund* ambao sisi Zanzibar hatuhusiki nao. Hata hivyo, Wizara ya Kilimo imo katika juhudi za mwisho za kukamilisha mpango wa mfuko maalum wa misaada ya fedha za kilimo kwa Zanzibar. Hilo na sisi tunajitayarisha tupate *a kind of basket fund* kwa Zanzibar.

Malipo ya fidia kupitishwa umeme Mhe. Ali Abdulla Ali aliuliza hili. Niseme tu kwamba serikali imejitayarisha kwa ajili ya kulipa fidia kwa wale wote watakaoathirika kwa mali zao wakati wa kupitishwa kwa waya wa umeme kutoka Fumba hadi Mtoni chini ya mradi wa MCC.

Mhe. Ali Abdulla pia alitaka kujua au alishauri suala la pencheni kulipwa kwa mkupuo. Utaratibu Mhe. Spika, wa sasa wa kulipa pencheni ni kwa kila mwezi hadi mstaafu atakapofariki kwa mujibu wa sheria ziliopo. Pendekezo la ulipaji wa pencheni kwa mkupuo serikali imelipokea na kulizingatia lakini kama ulivyo utaratibu huo utaonekana unafaa mapendekezo ya mabadiliko ya sheria husika yataandaliwa na kuwasilishwa katika Baraza hili.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Abdulla alizungumzia suala la mkakati wa kujinusuru na msukosuko wa kifedha kwa Zanzibar. Taarifa ya mapendekezo ya mikakati ya kuinusuru na msukosuko huo unatarajiwa kuwasilishwa katika serikali zote mbili; SMT na SMZ kwa mazingatio kwa sababu kuna timu inaongozwa na mwenyewe Gavana wa Benki Kuu, Pro. Ndulu na sisi Zanzibar tunao wataalamu watatu katika kamati hiyo. Kwa hivyo inaandaliwa mipango, ile juzi ilikuwa kama muhtasari tu kuweza kutushajiisha.

Aidha mapendekezo ya mgao wa fedha wa kujinusuru na athari za msukosuko huo nayo pia yatawasilishwa katika serikali zote mbili kwa mazingatio na maamuzi.

Mhe. Spika, Mhe. Abubakar Khamis Bakary alizungumzia suala la co-operate tax kwamba zilipwe hapa Zanzibar. Serikali imeliona suala hilo na hata Mhe. Salmin Awadh pia alilizungumzia sana suala hili pamoja na lile la mapato ya payee. Suala hili limeshapokelewa katika kamati ya kero za muungano kwa ajili ya kupatia ufumbuzi. Tunalizungumza hili suala.

Suala jengine ni kuruhusu suala la maji ya drop hayauziki Tanzania Bara, Mhe. Abubakar, Mhe. Mshimba walilizungumza hili. Ni kweli sisi tumepata hizo salamu na tutajaribu kukaa na hawa wawekezaji wenyewe, kuona vipi tunaweza kuwasaidia kurahisisha soko kwa maji ya drop kwenda Tanzania

Bara, isiwe kama ile stori ya sigara zetu huko nyuma tukapata hasara mpaka kiwanda kikafa.

Mhe. Abubakar pia alizungumza sana na kuonesha na mchanganuo juu ya vianzio mbali mbali vya mapato. Mimi ninataka kusema Mhe. Spika, ningemuomba sana Mhe. Abubakar Khamis Bakary asubiri kwenye ile *respective budget* za wizara zenyewe, kwa sababu tukianza humu kutoa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi imekusanya hivi, Wizara ya Kilimo imekusanya hivi, ninafikiri itakuwa kubwa sana.

Lakini ningemuomba sana hivi vitabu akivisoma na hivi ndio *working document*, Mhe. Said Ali Mbarouk amesema *working document* ni ile hotuba yake Waziri Kivuli sio. Mimi ningemuomba sana ajue kwamba hii ndio *working document*. Kwa kweli tupitie sana Waheshimiwa kwa sababu maelezo mengi, ile ilikuwa ni summary tu niliyoisoma lakini haya nimepeleleza kwamba maelezo mengi ya Waheshimiwa waliyouliza basi yamo humu na yameelezwa kwa ufasaha.

Mhe. Spika, wenzetu wa Tanzania Bara asubuhi wanasoma mipango na jioni ndio wanasoma bajeti. Sasa sisi tumechanganya kwa pamoja kwenye ile niliyoisoma, lakini hiyo ni mwelekeo wa hali ya uchumi na hii ni mapitio ya hali ya uchumi na utekelezaji wa mpango wa maendeleo. Hivi vitabu vya kwanza na cha pili ni muhimu sana na yote yamo humu.
Mhe. Spika, kumradhi inabidi nimguse sana rafiki yangu Mhe. Said Ali Mbarouk – Waziri Kivuli kwa sababu yeye ni rafiki yangu sana. Mhe. Spika, hoja ya *supplementary budget*. Ninafikiri Mhe. Machano Othman Said kalieleza hili kwamba kwa kweli zile kasma zinazopitishwa hapa na Baraza, wizara hazijapindukia kiasi cha kuomba *supplementary budget* isipokuwa wanahaulisha wenyewe ndani ya wizara kwa vifungu ambavyo havitumiki. Kwa hivyo tunahisi kuwa haijafikia haja hiyo lakini ikifika haja basi tunaweza tukaomba.

Mhe. Spika, …

Mhe. Spika: Mhe. Waziri weka alama tulipofikia ili tumalize jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)
(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Anayeshughulikia Mambo ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nikushukuru sana kwa

kunipa fursa hii ya kuendelea kukamilisha majumuisho ya bajeti yetu hii ya Serikali.

Mhe. Spika, kwa kuendelea naomba kuzungumzia hoja ya pencheni nayo iliulizwa na waheshimiwa wengi sana. Mhe. Spika, Serikali inawajali sana wastaafu kwa muda waliotumikia Serikali kwa moyo mmoja hadi kufikia umri wao wa kustaafu. Serikali kwa mwaka imejitayarisha kufanya marekebisho ya mishahara na imeboresha viinua mgongo kwa kujumuisha mishahara na maposho ambapo itapelekea mstaafu kupata kiinua mgongo kikubwa ikilinganishwa na kabla ya kufanyiwa jumuisho la mshahara na maposho yaani *consolidation*. Kimsingi Mhe. Spika, Serikali itaangalia uwezekano wa kuongeza kima cha pencheni kwa mwaka wa fedha ujao 2010/2011 kama ilivyopendekezwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo ilizungumzwa na waheshimiwa wengi, Mhe. Haji Mkema, Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Hamad Masoud ni suala la VAT. Suala la VAT kwamba ipunguzwe zaidi ya pale tulivyopendekeza Serikali.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Haji Mkema na wengine kwamba kushuka kwa asilimia mbili ya kodi ya *VAT* kutasaidia kushusha bei za bidhaa mbali mbali ambazo zimekuwa zikitozwa V*A*T. Kwa hivyo ni matumaini ya Serikali yetu kwamba punguzo hilo pia litajitokeza katika bei za bidhaa na huduma mbali mbali zinazotozwa *VAT* hapa nchini.

Kwa mujibu wa sheria ya *VAT No. 4* ya mwaka 1998, sheria hii imetoa msamaha wa kutozwa kodi ya *VAT* kwa bidhaa zote muhimu ambazo zinamgusa mwananchi wa kawaida. Hii imewekwa kwa makusudi ili kutompa mzigo mkubwa wa kodi mwananchi kwa vile ni bidhaa ambazo anazihitaji katika matumizi yake ya kila siku. Bidhaa hizo zilizosamehewa kodi ya *VAT* na kuorodheshwa katika jadueli ya pili ya sheria ya *VAT* ya mwaka 1998 pamoja na vyakula muhimu katika nchi hii ni mchele, unga wa ngano, pamoja na dawa za hospitalini, vifaa vya elimu, mbolea na dawa za kilimo pamoja na vitabu na magazeti, huduma za usafiri kwa abiria, huduma ya maji, bidhaa za mafuta petroli na kadhalika.

Mhe. Spika, Serikali imeamua kwa makusudi kusamehe kodi ya *VAT* katika huduma na bidhaa hizo kwa lengo la kupunguzi ukali wa maisha wananchi wake. Kwa kweli kulikuwa na ushauri kwamba *VAT* tuifute kabisa nahisi kwa kweli tusende huko kwa sababu katika vianzio vyetu muhimu hapa kwetu basi hii kodi ya *VAT* kwa kweli ni muhimu sana na kwa kweli imekuwa inachangia kwa kiwango kikubwa kabisa. Nitatoa mfano kwa mwezi huu wa Mei ambapo kidogo mapato yalikuwa madogo tulikusanya kwa upande wa *ZRB* mapato

kiasi cha shilingi bilioni 1,242,789,122 na *VAT* ilichukua shilingi 2,116,908,023 ambapo kodi nyengine iliyofuatia ni *petroleum levy* iliyokusanya shilingi bilioni 1,208,000. Kwa hivyo utakuta *VAT* ni makusanyo yanayotuongezea mapato zaidi. Ukichukua tena kwa mwezi wa Februari makusanyo yote ninachukua kwa *ZRB* tulikusanya shilingi bilioni 9,905,946,000 basi *VAT* peke yake tumekusanya shilingi bilioni 3,365,447,352 kwa mwezi wa Februari.

Ukenda mwezi wa Machi ambapo mapato yalikuwa makubwa zaidi tulikuwa jumla ya makusanyo yafikayo shilingi bilioni 8,259,257,268 ambapo *VAT* tulikusanya shilingi bilioni 3,208,302,581. Kwa hivyo utaona Mhe. Spika, mote humu kodi ya VAT ni kodi ambayo kwa kweli inatupatia makusanyo mengi sana. Hatuna budi sote kwa kweli kuizingatia na kuikubali kwamba ni kodi halali na itatusaidia.

Mhe. Spika, kulikuwa na hoja nyengine tuliulizwa hii ni suala la wafanyakazi wa Bodi ya Mapato wadhibitiwe ili kuepuka vitendo vya rushwa na kupoteza mapato ya Serikali. Napenda kumhakikishia hasa Mhe. Mkema na Washeshimiwa wengine waliochangia kwamba Serikali imekuwa ikilipigia vita sana suala la rushwa kwa jumla na sisi wenyewe Waheshimiwa Wawakilishi kwamba mara nyingi tumekuwa tukilizungumzia hili suala na sio kwenye taasisi zake peke yake, bali ikiwa ni pamoja na taasisi za ukusanyaji wa mapato kama vile *ZRB*.

Lakini hata *ZRB* ikiwa hata *ZRB* ikiwa ni taasisi ya Serikali ambayo inajitegemea imekuwa ikitayarisha taratibu zake mbali mbali katika utendaji wake wa kazi. Kwa hivyo, kwa kuelewa kwamba kazi ya ukusanyaji wa mapato inaambatana na vishawishi vingi vinavyoweza kumfanya mfanyakazi kushawishika kutaka kupokea rushwa, imeweka kanuni za maadili, yaani *code of conduct* ambazo ndio muongozo wa utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Kanuni hizo za maadili zinasimamiwa na kamati ya maadili ya Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mapato. Endapo mfanyakazi yoyote atashikwa kwa ushahidi kwamba amepokea au ametaka kupokea rushwa kanuni hizi zina adhabu kali ikiwemo ya kufukuzwa kazi moja kwa moja na hatimaye sheria nyengine za nchi kuchukua mkondo wake.

Mhe. Spika, ushauri wa kulisha viapo watendaji wa *ZRB* ni zuri, isipokuwa suala hili linahitaji utaratibu wa kikatiba. Suala la viapo ni kwa viongozi na watendaji wakuu ambao limeainishwa katika Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa wengi ni suala la kodi ya majengo na tumeulizwa kwamba inamlenga nani na inatozwa kwa malengo gani. Mhe. Spika, kodi ya majengo si kodi mpya kama

inavyofikiriwa na wengi. Tumewahi kulizungumza hapa tulipopitisha sheria ni kodi ambayo ilikuwa ikitozwa kabla Mapinduzi Matukufu ya Januari, 1964. Na hata baada ya Mapinduzi kodi hii imekuwa ikiendelea kutozwa, kwa miaka yote hiyo kodi ilikuwa ikitozwa na kukusanywa na Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji. Lakini kutokana na kwamba kodi hiyo kuwa haikusanywi kwa ufanisi, ndipo kodi hiyo ilipohamishiwa kukusanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar ikiwa ndio chombo kikuu cha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria ya ukusanyaji wa kodi ya majengo kodi hii inatozwa kwa nyumba zinazoanzia thamani ya shilingi 50,000,000 katika kiwango cha asilimia 0.01 cha thamani ya jengo kwa mwaka mara moja kwa nyumba za makaazi. Kwa nyumba za biashara zinazotozwa katika kiwango cha asilimia 0.02 bila kujali thamani.

Kodi hii kote kule duniani ina lengo la kuimarisha huduma mbali mbali katika mitaa, na ndio maana imekuwa ikitozwa Manispaa mbali mbali duniani, ikiwemo hapa kwetu Zanzibar,hivi sasa ambapo hivi karibuni tu ilihamishiwa kukusanywa na *ZRB*. Mbali ya kuhamishiwa kukusanywa na *ZRB*, bado lengo la kutoza kodi hii imebaki pale pale ambapo nia ni kutoa huduma mbali mbali za mitaani, ikiwemo kutengeneza barabara ndogo ndogo za mitaani, kuweka taa za mitaani, kutengeneza mitaro ya maji na huduma mbali mbali katika miji na mitaa ya hapa Zanzibar. Hiyo ndio msingi hasa wa kodi hii ya majengo.

Mhe. Spika, kulikuwa na hoja pia ya kigezo gani kilitumika katika kuandaa kukadiria mchango wa Shirika la Maendeleo. Hii aliuliza Mhe. Abubakar. Mhe. Spika, kigezo kilichotumika katika makadirio ya michango ya Shirika la Maendeleo, ni ahadi za michango wanayotoa hao washirika wa maendeleo wenyewe. Utaratibu huu ni mzuri na unatekelezeka, kwani unawashirikisha washiriki wa maendeleo wenyewe kwa kuthibitisha kiwango watakachochangia kwa mwaka fulani ndipo mchango huo huingizwa katika bajeti yetu.

Pia sisi kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunaonesha mchango wetu wa Serikali yaani *commitment* ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Na kwa kweli siku hizi wanatuangalia sisi tunatoa mchango wetu kiasi gani na wao wana-*calculate percentage* ndio wanatoa ule mchango wao. Lakini kwa kweli ni jambo la kufurahisha siku hizi miradi yetu yote ya maendeleo sisi tunajitahidi sana na ndio imekuwa changamoto pia kwa hawa wafadhili na wao kutoa kile kiwango wanachoahidi.

Mhe. Zakiya alitoa ushauri wa kuongeza thamani za bidhaa na kuwa na ubunifu na alikuja na mkoba wake ule mzuri ambao alituonesha. Mimi nimshukuru tu Mhe. Zakiya kwamba na Serikali imelipokea na italichukulia hatua. Ninafikiri

Mhe. Samia na Mhe. Asha ambao wanashughulika na ujasiri amali wamesikia na watalifanyia kazi ipasavyo.

Mhe. Hamad Masoud alitaka kujua misaada ya kibajeti ilipwe tangu 2003 pamoja na riba ile ambayo hatukupata. Ukweli ni kwamba hii tuliokuwa tukiikosa ni misaada ya mikopo sio *grant* ni *loan* hii, wenzetu walikuwa wakitunyima lakini ukweli tungeipata ingetusaidia lakini kwamba tungekopa. Sasa naomba tukumbuke kwamba fedha hizo ni za mikopo kama nilivyosema na Serikali kama ingechukua wakati wote huo iliwajibika kulipa wenyewe pamoja na riba. Kwa kuwa hivi sasa tumekubaliana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupata mikopo hiyo, nashauri tuanze na hapo tulipofikia. Imekuwa kama bahati nzuri kwamba hatukuwahi kukopa basi tena deni hilo halipo, lakini sasa madhali tumekubali tutakopa basi tutailipa.

Na uzuri wa mikopo hii kwamba inapowiva mara nyingi tunaanza kulipa kidogo na baadae wanatusamehe. Sasa wenzetu wamekuwa wanafaidika sana kwamba walikuwa wanaitumia vizuri na baadae wanasamehewa. Sasa fursa hiyo tuliikosa huko nyuma na sasa tunashukuru na sisi tumeanza kuipata.

Mhe. Spika, miradi ya barabara ya Pemba inayodhaminiwa na MCC ninafikiri Waziri wa Machano Waziri wa Mawasiliano hili alilieleza kwa ufasaha kabisa sina haja tena kulirejea.

Sasa nizungumze kwa kina kidogo kuhusu lile suala la wengi waliloliuza na hasa niligusia mmoja mmoja, Waziri Kivuli aliulizia kwa urefu na yeye lakini naona tumetayarisha jawabu kidogo lenye maelezo ya kina. Naomba niliwasilishe nitachukua muda wenu kidogo lakini ni muhimu sana tulifahamu vizuri.

Mhe. Spika, mkakati wa kuunusuru uchumi wa Tanzania tayari nimeuelezea katika hotuba yangu na naomba Waheshimiwa Wajumbe wapitie bajeti yetu katikia ukurasa wa 43 hadi 46, tumeeleza vizuri pale mikakati hiyo ambayo tunaichukua.

Napenda kuwaeleza waheshimiwa kwamba mkakati uliotolewa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nao pia utatumika Zanzibar. Na kwa Zanzibar sekta zinazoonesha kuathirika ni utalii na kilimo. Kwa upande wa kilimo zao la karafuu na mwani bei yake katika soko la dunia imeshuka.

Mhe. Spika, karafuu bei imeshuka kwa asilimia 14.3 kutoka dola za kimarekani 4,000 kwa tani kwa mwezi wa Agosti mwaka huu hadi dola za kimarekani 3,500 kwa tani mwezi Februari mwaka huu. Kutokana na hali hiyo Shirika la *ZSTC* lilishusha bei ya karafuu kutoka shilingi 3500 kwa kilo moja kwa

karafuu za daraja la kwanza hadi shilingi 2500 kwa kilo moja. Hivyo hasara iliyopatika ni shilingi bilioni 3.1.

Mahitaji ya mwani katika soko la dunia yapo chini kwa asilimia 25 ya uzalishaji. Wakati uzalishaji umezidi kwa asilimia 10. Hivyo hasara iliyopatikana ni shilingi milioni moja kwa wafanyabiashara.

Kwa upande wa utalii maelezo yanapatikana katika kitabu nilichokiwasilisha katika hotuba yangu hiyo kwenye Baraza letu. Mhe. Spika, hatua mbali mbali za kutekeleza mkakati huo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza kufidia hasara walizopata wanunuzi wa mazao yaliyohusika kwa msimu wa mwaka 2008/2009. Pili kutoa udhamini wa kuahirisha mikopo ya waathirika, tatu kutoa mitaji ya uendeshaji kwa riba nafuu. Na nne kuimarisha mifuko ya dhamana yaani *credit guarantee schemes.*

Mhe. Spika, hatua hizi za kisera pia zitachukuliwa nazo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza kupunguza gharama za utalii kwa kuangalia viwango vya ada ya viza na kuendelea kukusanya ada ya viwanja vya ndege kupitia mawakala.

Pili kuinusuru nchi kutokana na upungufu wa chakula duniani uliochochewa na msukosuko huu. Serikali Mhe. Spika, kwa kuchochea uzalishaji wa kilimo cha umwagiliaji Serikali itaendeleza miradi ya kilimo cha umwagiliaji maji kama kichocheo cha uzalishaji. Serikali kwa upande wake pia itaendelea kununua zana za pembejeo za kilimo, kuongeza idadi ya matrekta na zana za umwagiliaji. Na wakati huo huo Serikali itaendelea kufanya utafiti wa kuanzisha ile *strategic grain reserve* au akiba ya nafaka ya chakula.

Mhe. Spika, Serikali itaendelea kulinda programu muhimu za kijamii kama za ukimwi, malaria, kifua kikuu na programu za ustawi wa jamii. Kulinda utekelezaji muhimu hasa katika miundombinu ili kuendeleza ukuaji wa uchumi na malengo ya *millennium.* Suala la msingi kwamba tujitahidi kwamba haya mafanikio tuliyopata basi yasituanguke, ikawa kazi yote tuliyoifanya ile imeharibika kama baadhi ya nchi.

Mhe. Spika, Serikali imeweka zaidi ya asilimia 33 ya bajeti yake katika miundombinu muhimu ili kuendeleza kilimo na utalii. Pia Serikali itaendelea kutafuta fedha za kutosha za kuekeza katika miundombinu ya jengo la abiria la uwanja wa ndege wa kimataifa wa Zanzibar. Upatikanaji wa majenereta ya dharura kwa upande wa umeme na ujenzi wa bandari ya Mpigaduri. Kwa hivyo basi mkakati wa kuinusuru upo katika uendelezaji wa utalii, kilimo na

miundombinu na ndio ujumbe wa bajeti yetu ya mwaka 2009/2010 ambayo ni maendeleo ya miundombinu kwa kuimarisha kilimo na utalii.

Mhe. Spika, nilizungumzia sana na wenzangu walinisaidia kuhusu suala la bajeti tegemezi. Naomba tu niseme kwamba malengo haya ya milenia ambayo yamewekwa na umoja wa mataifa, basi na sisi tumeyainisha katika mpango wetu huu wa utekelezaji wa MKUZA. Na malengo yenyewe yanaitwa *Millennium Development Goal* yapo manane.

1. Kuondosha umaskini uliokithiri na njaa.
2. Kufikia elimu ya msingi au kwa kwetu hapa tunashukuru tumeshavuka.
3. Kukuza usawa, jinsia, na kuwawezesha wanawake.
4. Kupunguza vifo vya watoto.
5. Kuimarisha afya za uzazi.
6. Kupambana namaradhi ya ukimwi, malaria na maradhi mengine.
7. Kuhakikisha mazingira endelevu na
8. Kukuza mawasiliano ya kidunia.

Mhe. Spika, nchi zinazoendelea zikiwemo nchi zetu hizi za ulimwengu wa tatu zinatakiwa kutayarisha mikakati ya utekelezaji wa malengo, ndio tukatayarisha mkakati wa kupunguza umaskini ambayo itaingiza malengo hayo katika mikakati hiyo ambapo kwa Zanzibar tunao mpango wetu wa MKUZA.

Mhe. Spika, ili kugharamia mikakati hiyo Serikali zetu pia katika mwaka 2002 walikubaliana katika makubaliano yanayoitwa *monterey consensus* ya kukabiliana na changamoto ya kugharimu maendeleo. Hivyo makubaliano hayo yalizingatia kwamba patafutwe raslimali za ndani hasa kuongeza mapato ya ndani kwa maendeleo.

Pili kutafuta raslimali za nje hasa *FDI* na private flows
Tatu biashara ya kimataifa iwe ka injini ya maendeleo.
Nne kuongeza misaada ya fedha na kiutaalamu kwa maendeleo.
Tano mikopo ya nje.

Mhe. Spika, sasa tunapoendelea kupokea misaada kwa ajili ya utekelezaji wa *MDGs*. ili kufikia maendeleo endelevu sio tegemezi bali ni kuendelea na utekelezaji wa makubaliano ya kimataifa. Na haya Mhe. Shamuhuna alieleza vizuri sana tunamshukuru. Na hizi nchi zilizoendelea wao wametakiwa kwa kweli waongeze misaada wanayotuletea ifike asilimia 0.7 ya pato lao la taifa.

Mhe. Spika, maoni ya Waziri Kivuli wa asilimia mgao kwa sekta. Mhe. Spika, napenda kuendelea kutamka kwamba bajeti hii ni bajeti ya maendeleo ya

miundombinu kwa kuimarisha kilimo na utalii. Asilimia alizotoa Mhe. Waziri Kivuli ni kutokana niseme na kutaka kupotosha ukweli wa hali halisi ya bajeti hii. Na alitaka kama tuseme kujifurahisha zaidi.

Serikali haizitambui takwimu hizo kama nilivyoeleza hapo mwanzo, na zaidi kwamba jumla ya mapato yatakayokusanywa kwa mwaka 2009/2010 kwa upande wetu au kama alivyotoa ni shilingi bilioni 412 kutoka vyanzo mbali mbali na hivyo matumizi yatafikiwa shilingi hizo hizo shilingi bilioni 412.6.

Hivyo kutokana na kiwango hicho mgao kwa Wizara ambazo zimepewa upendeleo kutokana na bajeti yetu, Wizara zilipogaiwa hizi fedha kutokana na hii keki ndogo, kwa mwaka huu basi Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi imepata asilimia 16.69. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi imepata asilimia 16.56. Wizara ya Fedha na Uchumi imepata asilimia 15.16 na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wamepata asilimia 14.08, Wizara ya Kilimo imepata asilimia 6.41 na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imepata asilimia 5.99. Kwa kweli safari ni ndefu, ninajua kuna mapendekezo ya kimataifa tungependa tuyafikie kwa wakati huu lakini ninafikiri twende kidogo kidogo. Kutokana na mgao huu basi bado tunasema miundombinu imepata mgao mkubwa ambao mafanikio yake ndio tunatarajia kuimarisha kilimo na utalii.

Mhe. Spika, naomba sasa nimalizie malizie kwa kuzungumza hoja ndogo ndogo lakini ni muhimu zilizoguswa na waheshimiwa. Majengo ya kisasa yazingatie ulemavu. Mhe. Hamad Masoud tunamshukuru wazo lake ni zuri, ni kweli sote tuzingatie majengo yetu ya kisasa yazingatie utaratibu wa kupita walemavu.

Utozaji kodi kwenye jeti, Mhe. Nyonje yeye alizungumza suala hili ukweli ni kwamba madhumuni ya kutoza kodi kwenye jeti unalenga kwenye kupunguza ujenzi wa jeti au sasa kila mtu anataka kujenga jeti kwenye ufukwe katika maeneo ya bahari. Lengo letu ni kupunguza uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo basi utozaji hauna lengo hasa la kuongeza mapato ya Serikali. Lakini *primary aim* ni kupunguza zile jeti.

Mhe. Spika, Zanzibar inaagiza mazao ya chakula kama vile mchele lakini sasa inaagiza hata karoti, mabilingani na nyanya kama vile Zanzibar ni visiwa vya jangwa. Baadhi ya Waheshimiwa Mhe. Mshimba alizungumza hii na wengine. Ni ukweli kwamba mazao ya chakula pamoja na mboga mboga yanaagizwa kutoka Tanzania Bara, lakini uagiziaji huu unakuja kutokana na mahitaji makubwa ya bidhaa hizo hapa Zanzibar kwa ajili ya matumizi ya hoteli na majumbani.

Kwa baadhi ya bidhaa kama karoti na kebeji zinastawi katika kipindi kifupi cha kipupwe kama kipindi hiki tulichonacho. Sasa hivi mboga mboga zote hizi za baridi, karoti, kabeji, mabilingani makubwa, pilipili boga ndio kipindi chake. Sasa kwa kwetu hapa ni kipindi kidogo sana kama miezi mitatu, ikisha miezi mitatu hii basi vitu hivi hata ukiamua kupanda kabeji halitofunga, kitunguu hakitofunga. Lakini wenzetu wana baridi za Mbeya, Lushoto, Moshi kule kuna baridi kwa kipindi kirefu kabisa ndio maana zinaagizwa. Sio kwamba kila kitu tunakiagiza kwa makusudi tu lakini tayari kuna maendeleo mazuri, kuna wakulima wengi wazuri wazuri sasa imekuwa kama wakulima *commercial farmers* kwa kuzalisha vitu hivi.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Abuubakar, Mhe. Mulla na Mhe. Hija pia walielezea wasiwasi wao kuhusu bajeti ndogo iliyowekwa kwa kuendeleza zao la karafuu. Ninafikiri hili tumelizungumza kwa kina asubuhi sina haja tena ya kulirejea.

Mhe. Said Ali Mbarouk pia alizungumza mada ya demokrasia mapato ya uvuvi na bahari kuu. Napenda kumtoa wasiwasi Mhe. Mjumbe kwamba ni kweli Mamlaka ya Bahari Kuu itajengwa Zanzibar na iwapo Mwenyekiti wa Mamlaka hiyo atatoka Zanzibar, basi Msaidizi wa Mwenyekiti atatoka Tanzania Bara au kinyume chake. Kwa upande wa wajumbe wengine wa mamlaka hiyo kamati maalum inayoshirikisha Makatibu Wakuu sita, watatu kutoka Zanzibar na watatu kutoka Bara, wao ndio watakaokaa na kuamua mgawanyo wa wajumbe hao.

Mhe. Spika, Mhe. Mkema alizungumzia kwamba kilimo cha maweni hakishughulikiwi tumejikita kwenye mpunga tu. Niseme ni kweli kwa kiasi fulani, mimi niseme wakulima wenyewe wa maweni wamekuwa wachache, wengi ni watu wazima wa zamani sasa tusaidiane kuwashajiisha wakulima wa maweni warudie na vilimo vile vya zamani. Kama viazi vikuu, mitama kule maarufu lakini sasa tuseme Serikali, Serikali inashajiisha lakini jukumu letu sisi kama Wawakilishi na viongozi wengine tuwashajiishe kabisa warejeshe vilimo hivi vya viazi vikuu, mtama na kadhalika.

Bi. Mkongwe asubuhi nilisema habari ya kuuza dawa zile vichochoroni ninafikiri tumesikia tutafatilia tuone kwamba kwa kweli hili halifanyiki.

Mhe. Spika, ongezeko la mishahara kuwepo katika makisio ya bajeti. Mhe. Mshimba aliuliza kwamba mishahara mipya hii imo kwenye makisio ya bajeti ya mwaka huu. Ukweli ni kwamba naoma nimhakikishie Mheshimiwa kwamba mapendekezo ya mishahara iliyowasilishwa imefanyiwa makisio katika bajeti hii tunayoisoma ya 2009/2010. Malipo hayo yataanza rasmi mwezi Oktoba mwaka huu kwa utaratibu kama nilivyoeleza katika hotuba yangu. Sababu

kubwa yanayopelekea malipo hayo kuanza mwenzi wa Oktoba, ni kwa uzoefu umeeonyesha kwamba mapato ya Serikali katika miezi ya Julai hadi Septemba ukusanyaji wake huwa ni mdogo. Hivyo ili Serikali kuwa na uhakika wa kufanya malipo hayo ni vyema yakaanza kama ilivyopendekezwa ambapo tutakuwa tumeshajitayarisha vizuri.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba aliuliza tena suala la Halmashauri za Wilaya kuchukua au kuhamishiwa kodi ZRB. Napenda kuchukua fursa hii kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba hakuna kodi inayosimamiwa na halmashauri za Wilaya iliyohamishiwa ukusanyaji wake kwenda ZRB kwa sasa hakuna.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo kubwa na muhimu ambalo waheshimiwa wengi walitaka nilitolee kauli ni suala la mafuta. Takriban waheshimiwa wengi sana walitaka nigusie.

Mhe.. Spika, kwa kweli sisi upande wa serikali tulizungumza tukalijadili, tukatoa mapendekezo, mapendekezo yale yakaja Barazani hapa na tukayapitishha tukayarudisha serikalini na tumeyakubali. Sasa mapendekezo yale niseme kwamba yanafanyiwa kazi sisi tuwe na subira tu, kazi tumeshaifanya, tumeshatoa kauli, sasa twende kitaalamu kuifanya kazi hii, hii kazi inataka utaalamu lazima tutulie na muiamini serikali yetu kwamba sasa inafanya kazi, haiogopi wala haiumbishwi hii ni dola kamili. Tunatakiwa tustahamili kuna mikakati mziru inakuja.

Jina mlipendekeza wenyewe kwamba tusiige Bara kwamba kuna *TPDC* hasa tufanye *ZBDC* aa! Tutatoa jina litakuja. Ninachoshauri sana kwamba mapendekezo mliotoa waheshimiwa kama marekebisho madogo tu lakini serikali imeyapokea, imeyazingatia na inayafanyia kazi.

Mhe. Salmin Awadh na Mhe. Abubakar Khamis Bakary walitaka kujua zaidi kwenye matumizi ya fedha za kazi za maendeleo. Napenda kuwatoa wasi wasi kwamba madhumuni ya kupanga bajeti ni kutekelezwa kama ilivyopangwa. Kwa hivyo, makadirio ya matumizi ya fedha za maendeleo yatafanyika kadiri fedha zilizopangwa zitavyopatikana, ndio msingi hasa, tunapanga na tunakadiria sasa inategemea tunachopata. Kwa hivyo, kadiri tutachokipata tutatekeleza lakini tuombe mambo yetu yaende vizuri.

Mhe. Spika, udokozi wa Maafisa wa Mapato nimeshazungumzia sina haja ya kurejea. Mhe. Spika, nakaribia mwisho, Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu aliulizia suala la kuiva kwa deni la serikali tuna maana gani? Naomba kumjuilisha kwamba madeni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yamegawika katika sehemu mbili, yale ambayo yana udhamini wa Serikali ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yale ambayo yanalipwa moja kwa moja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Kama inavyoeleweka madeni yote yanapokopwa huwa na muda wake wa kulipwa, kwa msingi huo ndio unaitwa kuiva kwa deni, ni pale wakati ukifika wa kulipa lile deni, sasa hapo unatakiwa baada ya miaka kumi, mitano, kumi na tano au ishirini. Sasa wakati ule unapotakiwa ulipe ndio tunasema deni lishawiva. Utaratibu uliopo maana yake ni kwamba kama deni linalipwa kwa vipengele au pamoja na riba au lina muda wa kutolipa mpaka baada ya muda fulani, huo ndio utaratibu tunaosema deni kuiva.

Mhe. Spika, pia Mhe. Nyonje alikuwa na malalamiko yake ya muda mrefu kuhusu Jambiani Kikadini. Nataka kumuomba sana Mhe. Nyonje yeye kama Mwakilishi basi tuwaelekeze watu walioko chini yetu kufuata taratibu ni suala la taratibu tu basi. Nilichokigundua ni kwamba kama alivyosema mwenyewe kuwa kweli ruhusu ilitolewa na wale watu walijaza fomu sasa walitakiwa wajaze fomu nyengine tu basi, sasa wakishajaza fomu hiyo fedha zao watarudishiwa kwa sababu ule ni mradi wa wananchi hakuna sababu ya kuzuiliwa. Lakini labda kidogo hawakufahamu au waliona tabu ndio ikawa hivyo, kipengele ni hicho lazima taratibu zilizowekwa zifuatwe.

Mhe. Spika, kwa kweli hakuna tatizo sisi tunamuomba Mhe. Nyonje tukitoka hapa twende tukakae tujaze fomu tumalize na zile shilingi milioni mbili na ushei tutamrejeshea kwa kufuata taratibu.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala jengine ambalo limezungumzwa na waheshimiwa wengi wameliulizia sana suala la vitambulisho. Niseme tu kwamba si nia ya serikali kumdhalilisha mtu yeyote au kumnyima haki yake. Utaratibu uliopo kwamba vitambulisho vinapotolewa wilayani au vinapokataliwa kutolewa iwapo mwananchi anahisi hakufanyiwa haki katika kupatiwa kitambulisho hicho ana haki ya kukata rufaa kwa kujaza fomu maalum ambazo zinapatikana katika afisi za wilaya. Ikiwa pia hakuridhika na maamuzi ya wilayani mwananchi huyo ana haki ya kukata ruifaa kwa Mkurugenzi hadi kwa Waziri. Kwah ivyo, inashauriwa wale wanaohisi hawakufanyiwa haki wafuate utaratibu huo nilioulezа kisheria. Kwa kweli huo ndio utaratibu hakuna haja ya malimbano, kugombana wewe umenyimwa haki kajaze fomu panda Mkurugenzi mpaka ufike juu ndio utaratibu uliowekwa. Nafikiri hili ni suala la msingi.

Nimalizie kusema kwamba nashukuru kuwaa sote sasa tumeona umuhimu wa kuwa na hizi hati za vitambulisho. Kwa sababu wengine hapa tulipoleta sera ya vitambulisho tuliipinga kabisa labda tulikuwa na wasi wasi fulani hivi, lakini sasa naona tumeungana na *development* nzuri tu kwamba kweli kuna haja ya

kuwa na vitambulisho sote kwa usalama wa nchi yetu na shughuli zetu. Kwa sababu nchi yoyote unayokwenda siku hizi unaulizwa *ID*, sasa nafikiri na sisi kama inavyotumika kwengine kama benki, kusafiria kukata tiketi ni muhimu kwa usalama wan chi yetu.

Mhe. Spika, kama nimesahau mheshimiwa yoyote naomba radhi si lengo langu, lakini nimejitahidi kuzijibu hoja, maelekezo na maswali ya Waheshimiwa Wajumbe kama walivyoulizia. Ni imani yangu kwamba maelezo yetu yamekidhi haja na ninaomba sana tu- *encourage* mashauriano, *dialogue* kati yetu, kati ya Wizara ya Fedha na sisi Waheshimiwa, sisi tuko tayari tunao wataalamu wamebobea katika fani zao tutasaidiana kuelimisha, kuelekezana tufanikishe lengo letu la kuiongoza nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa haya machache ya jioni hii naomba kusema kwamba nakushukuruni sana na naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe baada ya majumuisho hayo ya Mhe. Waziri naomba sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja hii ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2009/2010 wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAULI ZA MAWAZIRI

Taarifa za Utekelezaji wa Haki za Watoto katika Kilele cha Siku ya Mtoto wa Afrika tareha 16 Juni, 2009

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyenzi Mungu Mtukufu kwa kutujalia uzima na afya na kutuwezesha kukutana hapa leo hii kwa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Watoto kwa mwaka 2008/2009.

Mhe. Spika, itakumbukwa kama ilivyo kawaida ya adhimisho siku maalum ya Mtoto wa Afrika ambayo kilele chake hufanyika tarehe 16 Juni ya kila mwaka. Siku hii maalum inaadhimishwa kuwakumbuka watoto wasio na hatia

waliouwawa na askari wa makaburu katika kitongoji cha Soweto nchini Afrika ya Kusini.

Mauaji hayo ya kinyama yalitokea wakati wanafunzi walipoandamana kupinga amri ya serikali ya Kikaburu ya kutaka lugha ya Kikaburu kuwa lugha rasmi ya Afrika ya Kusini kwa lengo la kuwatawala zaidi wazalendo wa nchi hiyo.

Kitendo hicho cha kupinga wakoloni na ukandamizaji wa Waafrika kilikuwa ni hatua ya kishupavu na kishujaa. Jambo hili ndilo lililoifanya siku hii kuwa ni ishara ya kuwakumbuka watoto hao wakombozi wa Afrika.

Mhe. Spika, maadhimisho haya huandamana na ujumbe maalum ambao unatoa msisitizo kwa utekelezaji wa haki za watoto. Ujumbe wa mwaka huu ni, "tuhimizane kuhakikisha watoto wanapata haki zao msingi" .Ujumbe huu unasisitiza umuhimu wa kuwapatia watoto haki zao za msingi za kuishi, makuzi, kulindwa, kushiriki na kushirikishwa katika masuala ya jamii.

Mhe. Spika, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ndio mratibu wa masuala ya watoto nchini. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka mazingira mazuri ya kusimamia haki za mtoto kwa kuanzisha sera ya uhai, hifadhi na maendeleo ya mtoto na kutekeleza mpango wa uhai, hifadhi na maendeleo ya mtoto unaoratibiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mashirikiano na Shirika la Kuhudumia la Watoto (*UNICEF*).

Sera na mpango huu umezingatia utekelezaji wa mkataba wa kimataifa wa haki za mtoto na mkataba wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake ambazo Tanzania imeridhia. Lengo la sera na mpango huu ni kuinua na kuimarisha hali za mama na mtoto kwa mtazamo wa maeneo manne makuu kama yalivyoainishwa ndani ya mkataba huo.

Maeneo hayo ni kama hivi:-

- haki ya kuishi
- haki ya makuzi ya mtoto
- haki ya kulindwa
- haki ya kushiriki na kushirikishwa katika masuala ya jamii.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa maeneo haya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto hushirikiana na Wizara ya Maji, Ujenzi na Nishati, Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na taasisi zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kimataifa.

Mhe. Spika, ninapenda kuchukua fursa hii kueleza kwa ufupi utekelezaji wa haki hizi kwa mwaka 2008/2009 ambao ufafanuzi wake unapatikana katika taarifa muliokwishakupatiwa.

Mhe. Spika, utekelezaji wa haki ya kuishi, kazi ya ufuatiliaji na ungalizi wa maendeleo ya ukuaji wa mtoto iliendelea kwa kushirikiana na timu za afya za Wilaya. Hata hivyo hali halisi inajionesha, mahudhurio ya watoto katika vituo vya huduma za mama na watoto hayaridhishi. Kati ya watoto walio chini ya umri wa miaka 5 ni watoto 39,603 sawa na asilimia 18.8 ndio waliohudhuria.

Mhe. Spika, zoezi la utoaji wa matone ya *vitamin A* na dawa za minyoo kwa watoto chini ya umri wa miaka 5 lilifanyika mwezi wa Agosti, 2008. Kwa upande wa dawa za minyoo jumla ya watoto 156,470 sawa na 92.7 na matone ya *vitamin A*. Watoto waliopatiwa ni 169,354 ambao ni sawa na asilimia 84.0. Kiwango hiki ni kizuri na kimeonesha mwamko wa akinamama na walezi kuona umuhimu wa kuwapatia watoto *vitamin A* vya nyongeza pamoja na kupunguza matatizo ya minyoo.

Mhe. Spika, mafanikio ya kuridhisha yameonekana kwa kuongezeka kwa kiwango cha chanjo za watoto kwa Unguja na Pemba. Mafanikio haya yanatokana kwa kuongezeka kwa huduma za mikoba katika maeneo ambayo hayana vituo vya afya. Kuongezeka kwa mafriji ya kuhifadhi ya dawa za chanjo katika Wilaya za Mkoani na Micheweni. Mafriji hayo mapya yanatumia gesi asilia *(LPG)* na kuongeza uwezo wa uhamasishaji na kuwapatia mafunzo madiwani na masheha wa Wilaya zote za Unguja na Pemba.

Katika kuhakikisha afya za watoto zinaimarika zaidi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Kitengo cha Chanjo za mama na mtoto, imeanzisha chanjo mpya ambayo inatumika kukinga magonjwa ya homa ya uti wa mgongo na homa ya mapafu.

Mhe. Spika, maji ni muhimu sana katika ukuaji, hifadhi na maendeleo ya mama na mtoto. Huduma ya maji safi na salama inapokuwa haina uhakika huathiri maendeleo ya mama na mtoto katika nyanja zote za maendeleo kama afya, elimu na uchumi.

Katika kuimarishaji upatikanaji wa maji, miradi ya maji imeendelea kutekelezwa ikiwemo miradi ya serikali, miradi inayosaidiwa na *UNICEF* na *TASAF*.

Mradi wa maji na afya Pemba kwa kushirikiana na *UNICEF*, wanavijiji 20,000 kati yao 8,000 ni watoto wamefaidika na mradi huu. Maradhi ya kuharisha na

mripuko yamepungua. Kuna ongezeko la nyumba zenye vyoo, kutoka asilimia 61 hadi 64.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo na Amali kwa miaka 5 mfululizo imewezesha watoto wote walioandikishwa darasa la kwanza kupatiwa nafasi ya kusoma. Mwaka 2008 idadi ya wanafunzi wa darasa la kwanza katika skuli za serikali ilifikia 33,216 kati yao watoto wa kike walikuwa 16,457.

Mhe. Spika, wanafunzi waliomaliza elimu ya msingi mwaka 2008 walikuwa ni 22,884, wanafunzi waliofanya mitihani ya darasa la saba mwaka 2008 walikuwa ni 22,884 kati yao hao wanafunzi 19,359 walifaulu mitihani yao, sawa na asilimia 85 na kuanza masomo ya sekondari katika skuli za Unguja na Pemba.

Aidha, wanafunzi 919 wamefaulu vizuri zaidi mitihani yao na kuchaguliwa kuingia skuli za michepuo. Wanafunzi 523 kwa Unguja na Pemba wanafunzi 396.

Mhe. Spika, juhudi zimefanyika kuhakikisha kwamba wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata haki yao ya elimu sawa na wanafunzi wengine. Idadi ya skuli zenye kusomesha kwa utaratibu wa elimu mjumuisho imeongezeka kutoka 46 mwaka 2006/2007 hadi 76 mwaka 2008/2009.

Wanafunzi wa elimu mjumuisho wameongezeka kutoka 1,523 hadi 2,795. Jumla ya walimu 603 walipatiwa mafunzo kuhusu elimu mjumuisho.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaendelea kuwapatia elimu mbadala wanafunzi wenye umri wa miaka 13 na kuendelea ambao hawajabahatika kupata elimu au kuacha masomo njiani. Katika mwaka 2007/2008 vimekuwepo vituo 20 vya elimu mbadala vyenye jumla ya wanafunzi 988.

Katika kipindi hiki cha mwaka 2008/2009, wanafunzi 152 walifikia kiwango kinachotakiwa na wamejiunga na madarasa ya kawaida. Wanafunzi 10 kutoka katika vituo vya elimu mbadala wamefanikiwa kuingia katika madarasa ya michepuo.

Aidha, wanafunzi 500 ambao waliacha skuli kutokana na umaskini wamekubali kurudi skuli na kupewa msaada wa sera za skuli pamoja na vifaa vya kujifunzia.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imewapatia walimu 27 wa skuli za sekondari mafunzo ya sayansi, 24 mafunzo ya kiingereza na 35 mafunzo ya hesabati ili kuongeza ujuzi wao wa kusomesha skuli za sekondari.

Jumla ya walimu 86 wamepatiwa mafunzo hayo kupitia programu ya uimarishaji ya elimu ya sekondari unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Mhe. Spika, Chuo cha Mafunzo kinaendelea kupokea watoto wanaofanya uhalifu na utukutu kwa kurekebisha tabia zao. Chuo kinahakikisha watoto hawa wanapewa kazi nyepesi kwa mujibu wa umri na hali zao za kiafya. Uhuru wa kuonana na jamii zao na haki ya kuabudu.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii ina wajibu wa kuhakikisha watoto wanaolelewa katika vituo vya Unguja na Pemba wanapatiwa malezi bora ili waweze kukuzwa katika hali ya usalama na kupatiwa haki zao zote za kimsingi kama watoto wengine.

Hivi sasa Zanzibar kuna vituo vinne vyenye watoto yatima na wale wanaotoka katika familia zisizojiweza kiuchumi.

Aidha, Idara ya Ustawi wa Jamii imepokea kesi 19, kesi 3 zimepata ufumbuzi na 16 zinaendelea kusikilizwa.

Mhe. Spika, mwaka 2008/2009 jumla ya malalamiko 202 yamepokelewa na wizara. Kati ya hayo malalamiko 105 ni ya kutelekezwa kwa watoto. Kati ya kesi hizo 96 zilifikiwa makubaliano ambayo yalizingatia mikataba na sheria ya kuwalinda wari, wajane na watoto wa nje ya ndoa ya mwaka 2005.

Malalamiko 9 yamepelekwa Mahakama ya Kazi na malalamiko 41 ya kubakwa na kufanyiwa vitendo vyengine vilivyo kinyume ya utaratibu na visivyokubalika na kutoroshwa yamepelekwa katika Mahakama ya Mwanakwerekwe, Mwera, Vuga, Wete na Chake-Chake Pemba.

Mhe. Spika, Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) inatetea haki za wananchi hususan wanawake na watoto kwa kutoa elimu, ushauri na huduma za sheria. Jumuiya hii imefanikiwa kutatua matatizo yanayowakabili watoto kwa kutoa ushauri wa kisheria na kupokea malalamiko ya unyanyasaji. Kwa kipindi cha mwaka 2008/2009 jumla ya malalamiko 23 yalipokelewa na jumuiya yamepatiwa ufumbuzi na 13 yanaendelewa kushughulikiwa katika vyombo vya sheria.

Mhe. Spika, hatua za kutayarisha sheria ya mtoto zinaendelea hivi sasa, kunafanyika utafiti wa matendo ya udhalilishaji wa watoto Zanzibar ambao

utasaidia katika kuona hali halisi ya udhalilishwaji wa watoto. Matokeo ya utafiti huu yatachangia katika kuunda sheria hii.

Ili kuhakikisha sheria hii inafuata mila, desturi na misingi ya Kiislamu, Wizara kwa kushirikiana na *UNICEF* imo katika hatua ya kutafuta mshauri mwelekezi wa kimataifa ambaye ana uzoefu wa nchi zinazofuata misingi ya sheria na desturi zinazofanana na zetu.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na vitendo vya udhalilishwaji vya wanawake na watoto, wizara imefanya utafiti kadhaa, ukiwemo utafiti wa kuangalia uwezo wa watendaji wa vyombo vya sheria na watoa huduma kushughulikia masuala ya unyanyasaji wa kijinsia zikiwemo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Polisi na Mahakama.

Matokeo ya utafiti huo yamebainisha kasoro za ufahamu mdogo wa kusimamia masuala ya udhalilishwaji wa kijinsia kwa watoaji wa huduma, uhaba wa nyenzo za kufanyia kazi, mfano usafiri na vifaa kikiwemo kipimo cha DNA pamoja na watendaji wenye sifa na ukosefu wa taalum ya ushauri nasaha kwa watoto waliodhalilishwa na ukosefu wa utaalamu wa kuendesha kesi zinazohusiana na udhalilishwaji.

Mhe. Spika, haki ya kushiriki na kushirikishwa inatoa fursa na uhuru wa watoto katika kutoa na kushiriki katika maamuzi yanayowahusu na kuathiri maisha yao. Haki hii inawapa nafasi ya kujiunga na kuunda vikundi vyao wenyewe vyenye maadili mema ili kutoa maoni na kupata taaluma zinazowahusu.

Katika kuhakikisha watoto wanapata nafasi ya kukusanyika na kujadili haki yao na wajibu wao kwa jamii, wizara kwa kushirikiana na *Save the Children* Tanzania na *ZACA* wamewashirikisha watoto kwa kuunda mabaraza. Jumla ya mabaraza 100 ya shehia yameundwa 60 kwa Unguja na 40 kwa Pemba. Kupitia mabaraza haya watoto wanapata fursa ya kushiriki na kujadili mambo yao yanayowahusu.

Mhe. Spika, utekelezaji wa haki za mtoto unagusa sekta zote, hivyo hatuna budi kuchukua jitihada za pamoja katika utekelezaji wa haki hizo. Licha ya jitihada zilizoelezwa bado utekelezaji wa haki za mtoto unakabiliwa na changamoto nyingi, zikiwemo ukosefu wa bajeti maalum ambayo itatumika katika kutekeleza shughuli za watoto katika kila sekta husika.

Kuporomoka kwa maadili katika jamii na kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto, ongezeko la kuvunjika kwa ndoa, kutokuwepo kwa tabia ya kuwasikiliza na kuwashirikisha watoto katika masuala yanayowahusu.

Mhe. Spika, wizara yangu imetayarisha ngao zilizochongwa kwa kutumia mbao za mnazi na kudariziwa kwa shaba kama alama ya kuwapongeza wadau wanaoshirikiana na wizara katika kuhakikisha wanawake na watoto wanapata haki zao za msingi kwa kutathmini michango yao.

Wizara imeamua kupongeza wizara hizo na taasisi kama zifuatazo:-

1. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii
2. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
3. Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo
4. Wizara ya Maji, Ujenzi na Nishati
5. Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora
6. Kamishna wa Polisi
7. Mkurugenzi wa Mashtaka
8. Mashrika yanayohudumia Watoto – *Save the Children* na *UNICEF*

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na wengine wakishirikiana zaidi na sisi tutawapa hizo ngao vile vile.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kutumia fursa hii adhimu tena kutoa shukurani za dhati kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Amani Abeid Karume kwa kupongeza jitihada zake za kuweka mazingira mazuri yanayoturahisisha utekelezaji wa haki za mtoto hapa Zanzibar.

Aidha, shukurani za dhati kwa mashirika ya maendeleo ya kimataifa, kikanda pamoja na taasisi zisizokuwa za kiserikali za ndani na nje ya nchi kwa michango mikubwa katika utekelezaji wa sera ya uhai, hifadhi na maendeleo ya mtoto, na hivyo kutuwezesha kuwasilisha taarifa hii katika Baraza lako tukufu.

Mashirika hayo ni *UNICEF, WHO, UNESCO, SIDA, ILO, ADB, UNDP, World Bank, Save the Children in Tanzania, SOS, African Muslim Agency Istiqama, AghaKhan Foundation, Clinton Foundation, ZACA, ZAIDESA, ZAMWASO, ZAFELA, ZAPAD, GAF* na wengineo.

Ni matarajio yangu washirika hao wataendelea kutuunga mkono katika kuhakikisha haki za watoto zinafikiwa. Baada ya maelezo haya, naomba kuwasilisha taarifa rasmi taarifa ya utekelezaji wa haki za mtoto kwa mwaka 2008/2009.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak (Waziri Kivuli Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto) Ahsante sana Mhe. Spika, natoa taarifa kutoka kambi ya upinzani ya taarifa ya utekelezaji wa haki za watoto katika kilele cha siku ya mtoto wa Afrika.

Mhe. Spika, ninatanguliza maelezo haya ya kambi ya upinzani katika Baraza hili tukufu kwa kumshukuru Allah ambaye ndiye aliyetuwezesha leo hii kukutana hapa katika kuzungumzia haya tunayoyasema hivi sasa. Mambo yote hayo yamo katika mipango yake ambayo hakushirikiana na yeyote kuipanga.

Mhe. Spika, namuomba Mwenyezi Mungu mtukufu aniwezeshe kuyatoa maelezo haya kwa salama na amani na utulivu moyoni. Baada ya hapo naomba nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuniruhusu nitoe maoni haya katika Baraza lako hili tukufu. Ni matumaini yangu kuwa Wajumbe wa Baraza lako hili watanisikiliza vizuri na hatimaye watanifahamu.

Mhe. Spika, tunakidhi kukumbuka Siku ya Mtoto wa Afrika kwani siku yake hasa ilikuwa tarehe 16 Juni. Katika hili tunatumia msemo tulioachiwa na wazee wetu kuwa "mwendaji si mkaazi". Tumeona bora twende haidhuru tumechelewa.

Mhe. Spika, kama tunavyoelezwa kila mwaka kuwa siku hii ya Mtoto wa Afrika ni kumbukumbu ya mateso na mauaji ya watoto wa Soweto huko Afrika Kusini tarehe 16 Juni, 1976. Watoto waliandamana kupinga azimio la kufuta lugha yao katika mitaala ya elimu na kuweka lugha ya kigeni badala yake waliuliwa na makaburu. Huo ulikuwa uvunjaji mkubwa wa haki za binadamu. Kutokana na dhulma hiyo kubwa kikao cha Umoja wa Nchi huru za Afrika cha Julai 3, 1990 kikaiweka rasmi siku ya tarehe 16 Juni kuwa ni Siku ya Mtoto wa Afrika, ikiwa na lengo la kuitumia siku hii kuhakiki maisha ya watoto wa Afrika na tupate kuimarisha ustawi wao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naona sasa ni wakati wa kumuangalia mtoto wa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Bara la Afrika. Hapa naanza kwa kujiuliza je, mtoto wa Zanzibar uhai wake na maendeleo yake yakoje? Anaishi wapi, anaishi vipi, ana raha gani na ana matatizo gani? Je, haki zake anazipata kwa kiasi gani?.

Mhe. Spika, mtoto ana haki ya kuishi, tena kuishi katika hali inayostahiki. Katika kuishi kwanza anahitaji kula, kuanzia tumboni mwa mama yake na mpaka akiwa nje ya tumbo mtoto anahitaji chakula tena chakula kinachostahiki. Lishe ya mama wajawazito hasa vijijini si ya kuridhisha na humuathiri mtoto kuanzia tumboni kwa mama yake.

Hali hiyo huendelea pale mtoto akishazaliwa na anapoendelea kuishi. Hilo linatokana na uwezo mdogo walionao wananchi wetu wa kuweza kujikimu na kuwakimu watoto wao ipasavyo. Kwani kinachohitajika sio kujaza matumbo tu bali ni kupata chakula timilifu *(balanced diet).* Katika hili uhaba wa madini joto nao unaathiri sana maisha ya watoto. Bado kuna haja ya kushughulikiwa hali ya lishe ya watoto.

Mhe. Spika, katika kuishi mtoto anahitaji kukingwa dhiki ya maradhi na kutibiwa pale anapoumwa. Serikali imejitahidi kupambana na maradhi thakili ya malaria lakini inashangaza kuona vita dhidi ya malaria viko vijijini tu lakini mjini hapa Unguja hapana. Je, watoto wa mjini wana kinga dhidi ya malaria hata dawa ikawa haitiwi mjini? Kuna haja ya kupambana na malaria Zanzibar nzima ili tusitie maji pakachani. Kwa upande wa matibabu kuna haja kubwa serikali kuondoa michango ya matibabu kwa watoto ili kutoa nafasi nzuri ya watoto kupelekwa hospitali bila ya woga kwa kudaiwa michango na badala yake wakapigwa nyungu na kumalizwa maisha yao.

Mhe. Spika, katika maisha ya mtoto maji safi na salama ni jambo la lazima. Bila ya maji safi na salama watoto watajaa maradhi yatokanayo au yanayosambazwa na maji. Pamoja na juhudi kubwa ya serikali bado kuna sehemu za vijijini zilizopuuzwa kupatiwa huduma hii. Mpaka hivi sasa kuna watoto ambao inawapasa waamke alfajiri wende wakatafute maji ya kuokota mabondeni. Kisha wapande nayo mlimani kuyapeleka nyumbani kwao. Kwa sehemu ambazo vimejengwa visima vya kutumia pampu sasa umefika wakati wakapatiwa maji ya mfereji, kwani usumbufu wa pampu hizo huwafanya watoto waumwe na vifua kwa kusukuma pampu hizo.

Mhe. Spika, waziri katuorodheshea changamoto nyingi za utekelezaji wa haki za kuishi. Sijui changamoto hizi kaziorodhesha kwa lengo gani. Kambi ya upinzani ilitarajia kuwa Mhe. Waziri angeorodhesha changamoto na kutoa mipango ya serikali ya kupambana na changamoto hizo ili mtoto wa Zanzibar aweze kupata kikamilifu haki yake ya kuishi.

Mhe. Spika, haki ya pili ya mtoto ni haki ya makaazi. Katika makaazi mtoto anastahiki apate elimu. Elimu ya mtoto inaanzia nyumbani kwa wazazi wake anapokuwa bado hajafikia umri wa kwenda skuli. Elimu hii kwa kiasi kikubwa inatolewa na wazee na walezi wa watoto hao. Lakini anapofikia umri wa kwenda skuli hapo anatakiwa apatiwe elimu kuanzia chekechea mpaka sekondari. Pamoja na maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri kuhusu upatikanaji wa elimu kwa watoto wetu bado kuna kasoro kadhaa zinazohitajika kurekebishwa.

Kwanza, pamoja na juhudi kubwa ya wananchi ya kujenga mabanda bado kuna uhaba wa vyumba unaosababisha kuwepo kwa madarasa makubwa

yasiyosomesheka. Aidha, watoto wengi wanakaa chini madarasani na kuwafanya wafanye vibyongo kwa kuinama wakati wa kuandika. Kuna uchache wa walimu na walimu wenye sifa maalumu. Kuna uhaba wa vifaa vya kusomea na kufundishia. Yote hayo yanahitaji kushughulikiwa ili mtoto wa Zanzibar aweze kukua vizuri.

Kwa upande wa elimu ya maandalizi Mhe. Waziri katuorodheshea idadi ya skuli na idadi ya wanafunzi lakini hakutwambia ni asilimia ngapi ya watoto waliofikia umri wa kupata elimu hiyo. Hivyo haieleweki tuko katika kiwango gani katika elimu hii ambayo ndio mwanzo wa elimu ya skuli. Miongoni mwa elimu muhimu ni ile ya roho, yaani elimu ya dini. Hatujui kuna madrasa ngapi zinazotoa elimu hiyo na ni asilimia ngapi ya watoto wanaopata elimu hiyo muhimu kwa tabia ya mtoto.

Mhe. Spika, watoto wanaohitaji uangalizi maalumu ni wale wanaoishi katika mazingira magumu na mayatima. Watoto wanaoishi, kwa mfano, Micheweni ambako kuna njaa iliyokithiri wanasaidiwa vipi? Aidha, mayatima katika nchi hii wamepewa nafasi gani katika jamii. Je, serikali inaelewa tuna mayatima wangapi? Wanaishi wapi na katika mazingira gani? Bado kuna mayatima wengi ambao hali zao za maisha sio nzuri. Kuna haja serikali kuwatafuta, kuwajua na kuwapatia msaada maalumu.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii adhimu kuyashukuru mashirika yanayowaenzi watoto wenye mazingira magumu, mashirika ambayo Mhe. Waziri kayataja, kijiji cha kulelea watoto *SOS, African Muslim Agency* na Jumuiya ya Istiqama.

Mhe. Spika, jambo la kusikitisha ni watoto kufungwa katika magereza ya watu wazima. Je, hili tunawatendea haki watoto hao? Jambo hili linaweza likatoa watoto manunda na wale walioathirika katika mwili na akili. Kama nilivyosema kwa changamoto za haki ya kuishi pia yanafaa yale yale kwa changamoto za makuzi ya mtoto na changamoto zinazofuata.

Mhe. Spika, kwa upande wa haki ya kulindwa mtoto bado hakujawa na hatua zinazofaa. Uundaji wa sheria ya mtoto umechelewa sana na sheria hiyo inahitaji ipelekwe mbio badala ya kutambaa, ingawa mambo muhimu lazima yazingatiwe. Mpango wa kungojwa malalamiko yapelekwe wizarani ndio yashughulikiwe hautoshi. Haki ya ulinzi wa watoto ni jambo muhimu sana. Hivyo matatizo yanahitaji kutafutwa na sio kungojewa wizarani au kwenye ofisi mbali mbali, kwani kuna wenye uwezo wa kuwasilisha matatizo wizarani na wako wale wasioweza kufanya hivyo.

Mhe. Spika, manyanyaso na matumizi ya nguvu isiyostahiki kwa watoto bado yanaendelea. Pamoja na kuwa na matukio machache yanayoeleweka lakini bado yapo mengine yanayofichwa kwa kuchelea aibu. Mhe. Waziri kaeleza matatizo kadhaa ya ukatili dhidi ya watoto lakini kamalizia kwenye maelezo tu hakutoa suluhisho la matatizo hayo. Kuna haja ya kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu matatizo haya. Kwanza kuna haja ya jamii kuelimishwa vya kutosha, lakini pia kwa wale wanaokamatwa kuwadhalilisha watoto adhabu kali inahitajika, tena itangazwe ili iwe ni funzo kwa wengine.

Mhe. Spika, ajira kwa watoto zote ni mbaya, hakuna mbaya na nzuri. Watoto hawastahiki kutumikishwa katika ajira zozote zile. Lakini kuangalia ajira tu bila ya kuangalia sababu ya ajira itakuwa bado hatujawafanyia haki wazee na watoto hao. Kuna familia zilizoko katika maisha magumu sana zinazoongozwa na mama bila ya baba wala wahusika wengine. Au dada ana ndugu zake bila ya mama wala baba. Wazee hawa huona hawana njia ila kuwatoa watoto walionao wafanye kazi hizo mbaya ili waweze kujikimu. Hapa kambi ya Upinzani inauliza. Je, serikali imeweka mpango gani kuwajua watu wa aina hii na ni hatua gani zinazochukuliwa kuwasaidia ili watoto wasalimike na ajira?

Mhe. Spika, katika hali ya kushiriki na kushirikishwa watoto katika masuala ya jamii bado haijaridhisha. Hapa napenda kutofautishia baina ya watoto kushiriki au kushirikishwa katika mambo yao wenyewe na kushiriki au kushirikishwa katika mambo ya jamii. Katika mambo yao wenyewe watoto wana nafasi kubwa ya kushiriki au kushirikishwa. Lakini katika mambo ya jamii hakuna utaratibu maalumu uliopangwa. Mabaraza ya watoto ya Shehia, kama yapo kama tulivyoambiwa basi yatajishughulisha na mambo yao wenyewe na sio ya jamii. Hata hivyo, ilikuwa tudokezwe angalau ni Shehia zipi zilizobahatika kuwa na mabaraza ya watoto.

Sisi tunavyoelewa watoto hushiriki katika shughuli za jamii ikiwa ni sehemu ya maisha ya kawaida ya jamii zetu. Kwa mfano, watoto wanashiriki kwenda mazikoni, hitimani, harusini na katika shughuli mbali mbali za jamii bila ya kupangiwa na mabaraza yao au kupangiwa na uongozi wowote ule. Tabia hii ni nzuri na inafaa iendelee. Hata bado watoto hawana nafasi ya kushiriki katika maamuzi ya shughuli za jamii. Kwa mfano, kunatafutwa mradi wa jamii wa *TASAF*, watoto hawapewi nafasi kutoa maoni yao na huonekana hawana mawazo ya kufaa. Hili linahitaji lifanyiwe kazi kwani ni haki yao kushirikishwa.

Mhe. Spika, kwa kuhitimisha maelezo haya ya Kambi ya Upinzani napenda kuchukua nafasi hii adhimu na adimu kuwashukuru wazazi na walezi wa watoto kwa juhudi kubwa wanazochukua katika kuwalea watoto wa nchi hii. Namuomba *Allah* awazidishie uwezo na awape subira katika kazi hiyo ya ulezi.

Aidha, nawashukuru walimu wa taasisi mbali mbali zikiwemo zilizo rasmi na zisizo rasmi kwa kazi nzito wanayoifanya. Malipo yao yako kwa Mwenyezi Mungu. Serikali nayo naipongeza kwa kazi yake, ila pia naiomba izidi kutimiza wajibu wake kwa yote yale tuliyoyaelekeza na mengine ambayo itajua yanafaa kutekelezwa kwa maslahi ya watoto wetu.

Mwisho Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunivumilia muda wote niliotoa maelezo haya. Papo hapo nawashukuru wajumbe wote wa Baraza lako hili tukufu kwa kunisikiliza. Namuomba *Allah* atuwezeshe kuwalea watoto wetu kama alivyotuagiza na anavyopenda yeye ili tupate taifa zuri hapo baadae. Amin.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak kwa maelezo haya ya Kambi ya Upinzani. Taratibu zinatutaka kama kuna maswali tuulize ili hatimae Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto atoe ufafanuzi zaidi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu naomba nichangie suala dogo tu ambalo linamgusa mtoto na haki yake ya kumlinda. Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa taarifa yake hii nzuri na naamini dhamira yake kama ujumbe unavyoelezea katika kipeperushi hiki kwamba ujumbe wa mwaka 2009 tuhimizane kuhakikisha watoto wetu wanapata haki zao za msingi.

Mhe. Spika, hivi karibuni kwenye Sauti ya Tanzania Zanzibar kwenye Mawio tulimsikia mzazi mmoja kutoka Jimbo la Magogoni, Shehia ya Kinuni analalamika kwamba kuna kitangi ambaye kila siku anaharibu watoto kwa njia anazozijua yeye. Malalamiko mengi yameshapelekwa katika Kituo cha Polisi Mwanakwerekwe lakini hadi kufikia hii leo kwa ushahidi niliokuwa nao bado mtu yule anatamba na hatua za kisheria hazijachukuliwa.

Kwa kuwa hili suala liko wazi na mlalamikaji kaipeleka kesi hiyo kituoni hatua hazijachukuliwa. Je, atachukua hatua gani ili kuisaidia jamii ambapo huyu kitangi imekuwa ni kero kwa watoto wengi kushindwa kwenda *tuition* na sehemu nyengine kwa kumuogopa yeye.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nitakuwa na maswali yafuatayo. Mhe. Spika, nakumbuka mwaka jana Mhe. Waziri wakati wa kutoa taarifa kama hii tulimuomba kwamba ni vyema siku kama hii basin a watoto wakashirikishwa ili kujisikia kwamba wazee wao wanatoa taarifa. Je, kwa nini leo hakuwaita tukawashuhudia.

La pili nimeona kwenye ukurasa wa 30 wa taarifa yake kuna watoto 50 ambao wako Chuo cha Mafunzo lakini bahati mbaya wote wanaume. Ukiangalia makosa yenyewe ni shambulio la mwili na lugha chafu. Je, wanawake tabia hiyo hawana.

Mhe. Spika, jengine kuna taarifa kwamba sasa wanaingia kutafuta mshauri mwelekezi. Je, watoto wangapi Wazanzibari watashirikishwa ili kutoa maoni yao au maoni haya yatatolewa na watu wazima.

Mhe. Spika, mwisho hivi karibuni Mkoa wa Mjini Magharibi umeshiriki katika zoezi la kuvunja nyumba za wakaazi ambazo zilijengwa isivyo halali kwa mujibu wa taarifa zao. Kwa nini wizara yako haikushiriki kuwatetea watoto wale ili kunusuru maisha yao.

Mhe. Zahra Ali Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi nina swali moja tu kwa Mhe. Waziri. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katueleza hapa kama bado vyuo vyetu vya mafunzo vinapokea watu wazima na watoto. Mhe. Spika, Mhe. Waziri haoni kwamba kuwachanganya watu wazima na watoto kutapelekea watoto hao kutorekebishika tabia bali kuwafanya kuwa masugu. Je, serikali ina mpango gani kupitia wizara yake ili kuhakikisha kuwa mchanganyiko huu thakili unaondoka.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, kipindi kilichopita mwaka jana na mpaka sasa hivi tuliambiwa kama Micheweni inaongoza kwa umasikini ni kweli kabisa. Pia tuliambiwa Micheweni inaongoza kwa ajira za watoto. Je, Mhe. Waziri amefanya mipango gani ya serikali ili kuwasaidia watoto wa Micheweni kuondokana na ajira za watoto.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nina maswali machache sana. Kwanza kwenye suala hili la madini joto *(iodine)* hivi karibuni tulikuwa na maonesho ya taasisi zisizokuwa za kiserikali na wenzetu wa Pemba kuna *NGO* nimeisahau jina lake lakini wao wanashughulika na mambo ya chumvi. Walipokuja hapa walithibitisha kwamba chumvi yote ambayo inatengenezwa Pemba hivi sasa inatiwa madini joto. Sasa nataka kushangaa kidogo kuona kwamba Micheweni wanasema kuna tatizo hilo. Upi ukweli uliokuwepo.

Mhe. Spika, la pili kuna suala hili la chanjo. Mhe. Spika, napenda tu Mhe. Waziri anambie kwa sababu hapa mjini ni *form VI* au chuo kikuu, mimi na Mhe. Ame Mati Wadi kule shamba sio *form VI*. Sasa katika suala la chanjo wameandika hapa, kiwango cha wanaoasi chanjo kimeendelea kuwa kizuri kwa

wilaya nyingi isipokuwa kwa Wilaya ya Mjini, Chake-Chake na Micheweni. Nini tatizo hapa Wilaya ya Mjini.

Mhe. Spika, halafu kwenye ukurasa wa 12 hii ya vyandarua hizi takwimu sijui kama ni sahihi. Waliopata vyandarua viwili 25,044, waliopata chandarua kimoja ni 1,756, jumla ni 31,000. Nafikiri hebu tuangalie hizi takwimu inaonekana kama si sahihi kwa sababu kwa *figure* hizi itaonekana kuna kasoro. Hebu tuangalie ipi ni ukweli.

Mhe. Spika, kiwango cha malaria hasa kwa watoto kimepungua kwa kiasi kikubwa na sasa hivi malaria kwa watoto iko kiwango cha chini sana. Lakini kiwango hiki kimepungua kwa sababu tunae mjomba anayetusaidia, kuna siku mjomba ataacha kutusaidia, kuna siku Mmarekani atatuacha mkono. Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuona siku mjomba atakapoondoka tutaweza kuendeleza vipi suala zima la kuwakinga watoto wetu na malaria.

Mhe. Spika, jengine kwenye *cover* hii kuna watoto watatu. Hawa watoto inavyoonekana kama ndivyo wanachezea maji. Kwa kujua kwangu watoto wanapokuwa katika hali hii hawana nguo ndio tunakaribisha *pneumonia* kwa watoto. Tunapoweka picha kama hii halafu tunazungumzia malezi bora na utunzaji wa watoto, nadhani picha kama hizi tusiziweke.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa kwenye upande wa elimu. Mhe. Spika, sijui Mhe Waziri atashirikiana vipi na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kuona suala la elimu ni suala la lazima kwa watoto wetu. Lakini sasa hivi maeneo mengi ambayo kuna utalii watoto ambao wanapaswa kwenda skuli wanakimbia na skuli yao ni kusuka kofia za makuti na kuuza hawendi skuli, wazee wao wapo lakini wamewaachia. Je, Mhe. Spika, wizara yako na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali mna mpango gani wa kuona tatizo hili linaondoka.

Mhe. Spika, zamani tatizo hili lilikuwa kubwa sana maeneo ya pwani watoto wakipara samaki. Kwa mfano, ukenda pale Kizimbani watoto hawaendi skuli. Mhe. Spika, ni hayo tu.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ndogo ya kuuliza yangu machache niliyokuwa nayo ili nipate ufafanuzi kutoka kwa Mhe. Waziri. Mhe. Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru Mhe. Waziri na Waziri Kivuli kwa kutuletea maelezo yao kuhusu Mtoto wa Afrika. Sasa katika mambo yote haya yaliyozungumzwa mimi nilikuwa nataka nipate ufafanuzi wa mambo mawili matatu.

La kwanza kutokana na maelezo ambayo Mhe. Waziri ameyatoa ametwambia katika mambo ambayo anapigania moja ni haki ya kuishi na hapana anayebisha juu ya hili. Mhe. Spika, kwa sababu haki ya kuishi ni haki yake mtoto. Je, Mhe. Waziri na wizara yake wamechukua juhudi gani kuona kwamba ili mtoto azaliwe ndio aje aishi kupigania ile haki ya kwamba liondoshwe suala zima la kulipia kwenye uzazi. Mhe. Spika, tulipiga kelele sana hapa kwamba iondoshwe ile ada ambayo mama mzazi anatakiwa alipe. Sasa yeye kama anaipigania haki hii kafikia wapi katika hilo.

Mhe. Spika, la pili mtoto anakuwa ameshazaliwa na wakati mwengine amezaliwa katika njia ambazo si halali. Wakati mwengine wanafikishana watu Polisi, Mahakamani, mpaka wengine wanafungwa jela. Sasa mtoto anakuwa hana uhakika baba yake ni nani. Kwa hivyo, ili yule mtoto kupata haki yake ya kujua mzazi wake ni nani, kuna kifaa kinachocheki *DNA* ambacho kinathibitisha kama huyo baba ndie au sie.

Je, Mhe. Waziri amefanya juhudi gani ya kukipata kifaa hiki ili watoto wetu wawe na haki na wao wajisikie kama mimi huyu baba yangu, huyu mama yangu na vitu kama hivyo. Kwa sababu wakati mwengine inawezekana si suala la kuwa baba hajulikani lakini inaweza kuwa mtoto huyo kaokotwa, mtu kafanya shughuli zake kamtia kwenye mfuko au kamuweka chini ya mlango wa jirani yake kenda mbio.

Mhe. Spika, la mwisho kama nimemsikia vizuri Mhe. Waziri alitaja suala la mshauri elekezi. Mhe. Spika, nilitaka kujua huyu mshauri elekezi nae ni mtoto? Kama si mtoto ni mtu anatoka au wa humu ndani. Kama anatoka nje mimi nilikuwa nashauri kwamba kwa sababu watoto ni wa Kiafrika na zaidi wa Kizanzibari, basi ni vyema hawa washauri elekezi wakapatikana miongoni mwa wazee wa Kizanzibari. Lakini pia nitataka ufafanuzi wa haya maswali yangu yaliyotangulia kama huyu Mshauri Mwelekezi na yeye ni mtoto au vipi na anatokea wapi.

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kuhusu Taarifa hii ya Siku ya Mtoto wa Afrika. Kutokana na taarifa hiyo ninayo maswali machache madogo madogo.

Swali la kwanza Mhe. Spika, kuna familia nyingi zinakuwa na watoto na wazee wasiojiweza, lakini wakati huo huo wapo watu wanaopenda kulea watoto. Je, Mhe. Waziri amefanya jitihada gani za kuorodhesha watu wa aina hii ambao wanataka kulea watoto, wakati inapotokezea familia ambayo haina uwezo na kuweza kupelekewa yule mtoto na kumlea ?

Jengine ni kuhusu mambo ya taaluma. Tunapiga kelele jinsi wanafunzi wetu wa skuli wanavyonyanyaswa kwenye gari za daladala. Kwa hivyo, jitihada gani wizara hii imechukua kuona kwamba wanafunzi hawanyanyaswi kwenye gari za daladala wakati wanapokwenda na wanaporudi skuli ?

Vile vile swali jengine dogo kuna baadhi ya skuli zimekuwa hazifuati maelekezo ya kutoa huduma vilivyo hasa zile skuli za *private*. Kwa mfano, Skuli ya Laureate watoto wadogo hutiwa kwenye gari kubwa aina ya bus kiasi 100, yaani watoto wa umri tofauti kama vile wenye umri wa miaka mitano, saba, kumi na hata kumi na sita? Kutokana na hali hiyo wale wenye umri mdogo wasiwe kwenye hali nzuri wakati wanapokwenda na kurudi skuli. Je, wizara hili inalijua na imechukua hatua gani kwa maafisa wetu kuonana na uongozi wa skuli zile, kwa ajili ya kuwapa muongozo uliosahihi wa kuwapakia wanafunzi kwenye gari ?

Mhe. Spika, jengine kwa kweli amenifilisi Mhe. Zakiya Omar Juma kuhusu ada za wazazi hasa kwenye hospitali hilo namuunga mkono tutajibiwa pamoja.

Lakini bado kunakuwa na msongamano kwenye Wodi ya Watoto. Kwa kushirikiana kati ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na *UNICEF* hili wameliona na wamelichukulia hatua gani. Kwa sababu hata kwenye Baraza hapa tulipendekeza kwamba kuwe na Wodi ama Hospitali ya Watoto. Kwa hiyo, serikali mpaka hivi sasa inazingatia vipi juu ya suala zima la Watoto kuwa na Hospitali yao, ili wapate huduma za afya vizuri.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi naomba nimuulize Mhe. Waziri maswali matatu. Kwanza naomba anieleze mtoto kuanzia umri gani ambaye anahitaji haki hizo, kwa sababu hata mimi kwetu naitwa mtoto. Kwa hivyo, napenda nifahamishe kuhusiana na hili *(Kicheko/Makofi).*

Pili hivi karibuni kulitokezea tatizo la mtoto kuingiliwa kule sehemu ya Fuoni. Kwa bahati nzuri yule mtuhumiwa wa suala lile tunasikia yuko nje, lakini kutokana na hali ya yule mtoto alivyoingiliwa, yaani ameharibika ametoka hali ya utoto na ukuwa mtu mzima. Sasa mtu kama yule Mhe. Waziri ambaye hali yake imeharibika, yaani utaratibu wa kimaumbile umepanguka. Kwa hivyo, wizara yako Mhe. Waziri inamsaidia vipi ?

Tatu Mhe. Spika, kuna mama mmoja ambaye ametokea Bububu alikuwa amemuokota mtoto. Kwa bahati nzuri alijieleza kwenye vyombo kwa lengo la

kujitambulisha kwamba yeye ameokota mtoto wa kike. Lakini mtoto yule akawa nunda, yaani akikerwa anavunja vitu ndani ya nyumba.

Sasa mama yule alipoona ile hali imekuwa mbaya sana, basi alikuja kwenye wizara yako Mhe. Waziri kwa ajili ya kupata ufumbuzi pamoja na kuweza kusaidiwa mtoto yule. Sasa anataka kumrejesha katika vyombo vinavyohusika, ili aweze kulindwa pamoja na kupewa haki zake za mtoto.

Kwa bahati mbaya wizara yako kuna maafisa ambao walikuwa wakimsumbua huku na kule na hatimaye mama yule alirudi. Baada ya kurudi siku ya pili yake ndipo alipovunja *television*. Kutokana na hali ile yule mama ikabidi afanye jambo bila ya kukaa, basi yule mtoto alimfukuza. Je, Mhe. Waziri katika suala hili wizara yako itakuwa imehusika na kufukuzwa kwa yule mtoto ?

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Spika, nakushukuru swali langu ni moja ambalo ni dogo tu. Hivi sasa katika nchi yetu zinaingia baskeli za mitumba nyingi sana na kuna wazazi ambao wanawapenda watoto wao huwanunulia baskeli hizi watoto kuanzia umri wa miaka 8 mpaka 15 na kabla hawajajua vizuri baskeli hizo, watoto huingia barabarani. Je, huku ni kuwapenda au ni kuwahatarishia maisha yao. Wizara inatoa wito gani kwa wazazi wa watoto hao ambao kwa mapenzi yao wanahatarisha haki ya mtoto ya kuishi ?

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana naomba kuuliza maswali mawili madogo. Wapo watoto ambao hawana baba wala mama, yaani wazee wao wameshafariki, lakini watoto hawa wanalelewa na ndugu wa baba na mama na wala hawana uwezo wa kihuduma kimaisha. Je, Mhe. Waziri utawasaidi vipi watoto hawa, ili waweze kujimudu kimaisha.

Pili wapo watoto ambao wazee wao wanao uwezo wa kuwasomesha, mavazi pamoja na chakula, lakini watoto hawa hawasikii la muadhini wala mtekamaji msikitini. Je, Mhe. Waziri utawasaidia vipi watoto hawa, ili wawe pamoja na wazee wao ?

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali machache yanayohusu haki za watoto. Masuala ya malezi pamoja na ukuwaji wa watoto wetu kwa kweli ni mambo yanayohusu wizara nyingi kwa hivyo naomba niulize maswali yafuatayo.

Kwanza tunalo tatizo kwenye jamii yetu kuhusu watu walioathirika na virusi vya UKIMWI, hutokezea wakazaa watoto na wao wakawa ni waathirika. Sasa serikali ina mpango gani wa kuwahudumia watoto kama wale ?

Pili Mhe. Spika, enzi za zamani kati ya miaka ya 70 watoto wa siku hizo ambao ndio viongozi wetu wa leo. Kwa kweli walikuwa wakipata maarifa makubwa sana kutokana na ile tabia kwamba ikifika saa 2 za usiku watoto wasitoke ndani, yaani ile ilisaidia sana enzi ya Valantia Sakabona, basi suala lile lilisaidia malezi. Watu wazima wa leo ambao ndio waliokuwa watoto wa miaka hiyo wamekuwa na heshma nzuri.

Lakini leo utaona watoto saa 2 mpaka 5 za usiku wanaranda mitaani na suala hili tunaambiwa mara nyingi na wazazi hushiriki. Kwa sababu tunayo serikali nini kauli ya serikali katika kuhakikisha kwamba wanaoitwa watoto na wala sio kama Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, wanabakia nyumbani na kuendelea kufanya shughuli zinazowahusu kama vile kupitia vitabu vyao pamoja na mambo mengine *(Kicheko/Makofi)*.

Tatu Mhe. Spika, zamani vile vile serikali ilikuwa na utaratibu maalum hususan Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupita maskulini na kukagua afya za watoto, kitu ambacho kwa kweli kilisaidia sana ukuwaji mzuri wa watoto katika kipindi kile. Leo suala lile limekufa maskulini na watoto afya zao si nzuri, kwani mtoto anaweza kwenda skuli bila ya kuangaliwa afya zao, yaani anakwenda na kurudi ni suala la wazazi hiari ya nyumbani.

Lakini serikali kipindi kile ilikuwa na dhamana hasa ya kupita na kuangalia afya za watoto. Je, serikali haioni umuhimu wa kulirejesha tena suala lile.

Mhe. Spika, sambamba na hili hivi karibuni tulishuhudia na huwa tunashuhudia kila mwaka, wenzetu kule Bara wanao utaratibu wa kuchangisha chakula kwa ajili ya wanafunzi wa skuli, yaani watoto. Sasa hilo kwa upande wa Zanzibar liko vipi? Mhe. Spika, nakushukuru na ahsante sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nilikuwa na mengi lakini mengine yameshaulizwa, isipokuwa nitauliza kwa njia nyengine.

Kwanza kuhusu suala la wanafunzi kuzurura wakati wa usiku ambalo hili tunaliona linasababisha athari kubwa kwa watoto na wanachukua muda mrefu sana kwa usiku mpaka saa 6.

Kwa mfano, wanakwenda kwenye Video, wanazurura na wengine kuwaona wale watu ambao wanatumia dawa za kulevya na watoto kuiga. Suala hili kwa upande wa wizara yako Mhe. Waziri umelioni na utalichukulia hatua gani, kwa ajili ya kushirikiana na wazazi ?

Pili ni kuhusu suala zima la wanawake wanaoachwa wakiwa na watoto wengi kama vile watano au sita, yaani mume amemuacha mke na kumtupa, yaani

hatoi huduma yoyote kwa watoto wake, hali ile ni mzigo wa mtu mwengine. Je, katika suala hili wizara itachukua hatua gani ?

Tatu ni kuhusu watoto ambao takriban tukiangalia Unguja pamoja na Pemba yetu, hivi visiwa vimezungukwa na bahari na watoto wetu wengi sana wanazurura sehemu za pwani katika kufanya shughuli za kupara samaki, yaani ajira za utotoni. Kwa kweli suala hili linaendelea na bado hakuna hatua zilizochukuliwa. Je, hili Mhe. Waziri ameliona na hatua gani zinaweza kuchukuliwa ?

Nne ni kuhusiana na ulinganisho baina ya watoto na watoto katika kivazi. Kwa sababu tunaona sehemu nyengine za Pemba na Unguja kwamba kuna watoto ambao wana hali duni katika kivazi. Je, katika hali kama hii watoto hawa tutawasaidia vipi ?

Mwisho ambalo ni swali muhimu ambalo takriban Unguja na Pemba siku hizi kuna Mashindano ya *Tahfidh ll-Quraan*, ambapo watoto wanawekwa sehemu nzuri kwa ajili ya kuendeleza suala hili. Je, katika wizara yake Mhe. Waziri anatoa mashirikiano gani, ili kuwasaidia wanafunzi hawa kuhusiana na suala hili.

Mhe. Spika, nakushukuru na ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza nataka kupata maelezo kuhusiana na jaduweli ilioko kwenye ukurasa wa 33 wa kitabu hiki cha Taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Watoto, yanayohusiana na malalamiko yaliyopokelewa Idara ya Wanawaka na Watoto kwa Mwaka 2008/2009, yenye *items* tofauti yakiwemo masuala ya kubakwa, mimba, kutoroshwa, kutekelezwa, mvutano wa malezi, kufukuzwa, kudhalilishwa.

Kwenye jaduweli hili Wilaya ya Kaskazini ‘A’ Unguja kuna mtoto mmoja tu kuhusiana na masuala ya kubakwa, Wilaya ya Kusini hakuna hata *column* moja iliyojazwa kama vile hakuna matokeo haya na Wilaya ya Kaskazini ‘B’ ni sehemu moja tu.

Kwa hivyo, nataka kujua hizi takwimu ni zile zilizopokewa tu au ufuatiliaji ulikuwa si mzuri na kwa sababu wengine hawakupeleka ndio maana hatukupata, wakati kukusanya takwimu ni kitu muhimu sana. Hilo ni moja.

Pili Mhe. Spika, tumesikia kesi nyingi za watoto kubakwa na watoto wenzao na kesi hizi kupelekwa mahakamani, kwa sababu ya ushahidi umekamilika basi hata Kipindi cha Mawio hutangaza kwenye Redio ya Sauti ya Tanzania Zanzibar. Lakini wakati kesi inapoendelea kwa muda mrefu basi inakuwa

kimya na kitendo kinakuwa kimetokea kweli. Hali hii ni sawa na kusema kwamba huyu mtoto hakutendewa haki.

Kwa hivyo, nataka kufahamu wizara inajihusisha vipi kwa wale watoto waliofikwa na maafa kama haya. Lakini kutokana na mazingira yalivyo, uwezo na ufahamu wa wazee wao huwa hawana sehemu nyengine ya kwenda baada ya hukumu kutolewa na wakati wamefanyiwa mambo kama haya.

Tatu Mhe. Spika, kuna skuli pale Mabaoni Chake-Chake ambayo inachukuwa watoto yatima na wasiojiweza, kwa ajili ya kuwapatia haki zao zikiwemo elimu, mavazi, chakula pamoja na malazi pale pale. Lakini kwa bahati mbaya mabweni mawili juzi yaliungua moto na kuwaka kabisa. Kwa kweli kazi ya kuwadhitibi watoto wale masikini ni lazima imetetereka.

Kwa hivyo, ninaiomba wizara izuchukue hatua angalau za kufuatilia hali hii pamoja na kuzungumza na waohusika, ili kutafuta njia ya kuweza kusaidia na kuona ile hali imerudi haraka iwezekanavyo kwa manufaa ya watoto hawa.

Mhe. Amina Iddi Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante mimi swali langu ni dogo sana. Kuna baadhi ya wazazi wanawalazimisha kuwapa waume watoto wa kike wakiwa na umri mdogo na kuwakatisha masomo. Je, Mhe.Waziri suala hili wizara yako inalishughulikia vipi ?

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, ahsante sana mimi swali langu ni dogo ambalo liko kwenye ukurasa wa 22 na 26. Tunafahamu kwamba wizara hii ni *cross cutting issue*, lakini zaidi mzigo mkubwa unabebwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwa kweli tukiangalia kwenye kitabu hiki kila mwaka wanahitaji waandikishwe watoto 22,773, pamoja na kwamba serikali inajitahidi maana imesambaza jumla ya madeski 1,980. Lakini kinachopoteza ili wizara zisipange mipango yao afya na elimu ni kutokuwa na takwimu nzuri ya watoto wanaozaliwa, ili kukidhi mahitaji halisi. Hivyo, Mhe. Waziri mmeshauriana vipi na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ili kusimamia Uzazi wa Mpango.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama alivyosema Mhe. Ame Mati Wadi kwamba mambo haya yanakwenda kwa mashirikiano kati ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kusaidia majibu, ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameuliza maswali kwa lengo la kumsaidia Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Watoto.

Kwa hivyo, nitajitahidi kwa yale ambayo nitakuwa na uwezo wa kuyajibu. Mhe. Spika, ninafanya hivi kwa kuwa ni Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii pia Mhe. Waziri ni mwenzangu sana na lazima nimsaidie *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, nianzie na hoja inayoeleze kuhusu chanjo za watoto ambao na kwa upande wa Wilaya ya Mjini, Chake Chake pamoja na Micheweni inaonekana hali haikuwa nzuri. Tatizo hasa la msingi wazazi wenye watoto hawakujitokeza kwa ajili ya kuwapelekwa watoto kuchanja chanjo hii.

Hali halisi ilivyokuwa ni kwamba siku moja kabla ya chanjo ile ilitolewa chanjo nyengine na ukatokezea mtihani kidogo kule, basi na hapa wakapata kama mshtuko. Hata hivyo, Mhe. Waziri alitoa maelezo pamoja na kushajiisha kiasi cha kutosha, lakini bado wengine hawakujitokeza. Kwa ujumla maeneo mengine yote wamefanya vizuri hasa Wilaya ya Magharibi pamoja na maeneo mengine.

Kwa upande wa Wilaya ya Mjini Chake-Chake pamoja na Micheweni ndizo ambazo hazikufanya vizuri, pengine kwa sababu ya kuangalia *television* sana pamoja na mambo mengine ya mjini. Hiyo ndio hali halisi ilivyokuwa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo naomba nilizungumzie ni kuhusu maradhi ya malaria kwamba hivi sasa mjomba yupo anatusaidia na malaria imeshuka. Je, mjomba akiondoka tutafanya nini ? Kwa kweli maswali haya tayari yameshajibiwa sana na hata Mhe. Waziri Kiongozi ameshalitolea ufafanuzi.

Kwa kawaida miradi mingi inayoletwa hapa na wafadhili au wahisani ama washirika wa maendeleo wanapoondoka, serikali yenyewe ndiyo inayochukua nafasi. Kwa hivyo, suala hili serikali itajitahidi pamoja na hatua tuliyofikia hivi sasa kuona kwamba tunafanikiwa vizuri baada ya kuondoka hawa washirika wetu wa maendeleo. Vile vile nizungumzie kuhusu swali lilioulizwa la kuwafanyia uchunguzi watoto wetu katika skuli. Mhe. Spika, hivi juzi tu nilijibu swali hili ambalo lilikuwa limeulizwa kwa swali Nam. 30 linalohusu utaratibu mzima ambao wizara yangu imepanga kutembelea skuli.

Nilisema kwamba mwaka uliopita tayari skuli 48 zimepitiwa na huu tunaumaliza mwaka 2008/2009, pia kuna utaratibu ambao umeshapangwa wa kutembelea skuli nyengine mwaka 2009/2010. Mradi huu umewachunguza wanafunzi 58,957 na kati ya hao wanafunzi 2,147 ndio waliogundulikana na matatizo.

Kwa hivyo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa hili inalishughulikia ipasavyo. Matatizo yaliyogunduliwa ni pamoja na masikio kutoka usaha, macho hayaini vizuri, maradhi ya ngozi, kichocho, meno pamoja na maradhi mengine.

Mhe. Spika, kuhusu takwimu za vyandarua ninadhani hii ndio hali halisi ilivyo, yaani ndivyo vilivyotolewa. Kwa hivyo, hivi sasa tuchukulie takwimu hii ilivyo na baadaye kama kutakuwa na masahihisho zaidi huko usoni tunaweza tukaangalia, vyandarua vinaendelea kutolewa. Kwa sababu vimeshatolewa maeneo ya vijijini na hivi sasa kwa sehemu za mjini.

Suala jengine ni kuhusu msongomano wa Wodi ya Watoto. Mhe. Spika, pamoja na hali tuliyona, lakini kwa sasa asilimia kubwa ile tuliyokuwa nayo na msongomano wa watoto kidogo imepungua. Kwa sababu tatizo kubwa lililokuwa likisababisha msongomano ni malaria, hivi sasa maradhi haya yamepungua kwa kiasi kikubwa.

Kutokana na hali hiyo msongomano umepungua, isipokuwa yaliopo ni matatizo ya kawaida na wala siwezi kusema umeondoka kabisa. Lakini umepungua si sawa na hali iliyokuwepo hapo nyuma, ambapo maradhi haya kasi yake ilikuwa kubwa tukilinanisha na hivi sasa.

Mhe. Spika, suala jengine ni la kuondoa ada ya mzazi wakati anapojifungua kwa njia *operation*. Kwa hivyo, hili tutalichukua na tunalifanyiakazi. Lakini ninadhani tulikubaliana sote hapa kwamba tulipitisha Sera ya Kuchangia Hudama hii. Mara nyingi tunasema pamoja na hali tuliyonayo hivi sasa, lakini kwa kweli suala la kuchangia kwa kiwango ambacho tumekiweka bado ni nafuu. Isipokuwa niseme kwa kuwa hili ameombwa Mhe. Waziri wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto tukaa pamoja na tutangalie tufanya vipi. Kwa maana hiyo, tutakaa pamoja na kuangalia namna gani tunaweza kulishughulikia suala hili na kufikia hatua muafaka.

Kwa hiyo, nadhani tuendi kidogo kidogo, kuna msemo unaosema hivi "bora ghali tunachokipata kuliko rahisi ambacho hatukipati". Mhe. Spika, lazima tujue kwamba wazazi wapo wengi na tunajitahidi pamoja na Uzazi wa Mpango tunaoupanga, bado hatujafikia hatua hiyo na matatizo tunayo. Kwa mfano, mimba za utotoni au za umri mkubwa zaidi, yaani matatizo yake yanayosababisha watu kufanyiwa *operation* yako mengi.

Mhe. Spika, hili tunalichukua na tutakaa kwa pamoja, kwa ajili ya kulifanyiakazi na kuona hatua gani muafaka tuchukue, zikiwemo za kupunguza kidogo kidogo. Lakini kwa sasa ni vyema tuende hivyo hivyo.

Kwa hayo machache nafikiri nimemsaidia kidogo Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, kwa yale mengine nadhani ataendelea mwenyewe kwa utaratibu.

Mhe. Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu juu ya masuala mawili matatu. Nakubaliana na Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa maelezo yake fasaha, kuhusiana na azma ya serikali kuendelea kuushughulikia Mradi huu wa Kupambana na Malaria.

Ni kweli katika mikutano mbali mbali ya Baraza lako tukufu hili, nimewahi kusema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejidhatiti vizuri kuendelea na Kampeni ya Kupambana na Malaria. Pamoja na hayo hata pale itakapofika wakati, wafadhili wanaotusaidia wamechoka kuendelea kutusaidia. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejidhatiti na itafanya kila lililo kwenye uwezo wake, kuhakikisha kwamba Mradi huu wa Kupambana na Malaria unaendelea.

Kwa sababu tumefikia mahala kila mmoja wetu anakubali, kwamba kiwango cha malaria Zanzibar kimepungua sana. Ingawa kuna wakati ninadhani wapo baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe katika Baraza lako tukufu walikuwa wanatilia shaka juu ya dhamira hiyo.

Mhe. Spika, kama nakumbuka vizuri kuna Mhe. Mjumbe mmoja aliwahi kusema ah! Serikali kwa takwimu hizi za kwamba kiwango cha malaria imezipata wapi, lakini leo kama waswahili wasemavyo kweli ikidhihiri uongo hujitenga, kila mmoja anabaini kwamba kiwango cha malaria Zanzibar kimepungua sana, kwa maana hiyo basi mafanikio haya ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumeyapata hapa tulipofika hatutorudi nyuma tutafanya kila linalowezekana na kutumia uwezo wetu tuliokuwa nao hata kama ni mdogo kuhakikisha kwamba program hii inaendelea, ili wananchi wetu wazidi kuishi maisha ya raha. Kwa sababu afya bora ina mchango mkubwa sana katika maendeleo ya nchi takriban kama kwa asilimia sitini mpaka sabiini ni wagonjwa wengi hapa Zanzibar, ambao wanafika katika vituo vyetu vya Afya, wengi wanabainika wanasumbuliwa na ugonjwa huu wa malaria.

Sasa kwa mafanikio haya tuliyopata basi kwa kiwango hicho cha asilimia sitini mpaka sabiini tutakuwa tunaimarisha afya za wananchi wetu, kwa mnasaba huo basi kadri tunavyoendelea kupambana na malaria ndivyo tunavyowasaidia wananchi kuwa na afya bora na wakiishi na afya bora basi na maendeleo yetu nayo yataimarika zaidi.

Suala la pili Omar Ali Shehe pale alisema umefika wakati labda angepatikana Sakabona mwengine, halafu akaendelea kupendekeza akasema pengine valantia wangeweza kufanya kazi hiyo. Mimi huwa napata matatizo mara nyingi ninaposikiliza mijadala yetu, jana kulikuwa na wajumbe wanasema kwamba valantia na JKU vifutwe havina maana, leo tunawapa kazi nyengine ya kulea, sasa mimi huwa najiuliza ni lipi.

Lakini sio neno, maana kazi ya mdomo ni kusema na kazi yetu sisi wanasiasa ni kusema sasa pengine hilo sio neno, pengine tuchukue tu ile falsafa iliyomo kwenye jambo hilo ambalo Mhe. Mjumbe kalizungumzia, mimi kwa mawazo yangu wakati huu tuliofika wakati ambapo nchi yetu inajenga misingi ya utawala bora na haki za binaadam sina hakika sana kama wakati huu ni muafaka kurudi nyuma tulikotoka.

Kwa sababu wakati ule Sakabona na wenziwe walivyokuwa wanapita kwenye majumba yetu, wapo watu wana harakati walikuwa wanasema mbona serikali inaingilia haki za binaadamu huu sio utaratibu mzuri, serikali ikaanza pole pole kuanza utaratibu huo mpaka utaratibu huu ukaondoka. Sasa leo tunarudia tena na tunapendekeza pengine Valantia na wengine watumike kwa kazi hii, mimi nasema jambo hili tulifikirie kwa makini sana. Nafikiri dhama na wakati umebadilika sana, kazi ya kulea sisi wazazi na walezi kazi hii tumepewa na Mwenyezi Mungu kwa hivyo ni jukumu letu kuendelea kulea, sasa tukitaka kuiachia kazi hiyo ya kulea tuiachie serikali sidhani kama inaweza kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi zaidi, nafikiri Sakabona mzuri zaidi mimi nafikiri ni baba na mama.

Suala la watoto wakorofi waheshimiwa wajumbe mtakumbuka kulikuwa na wakati serikali ilianzisha utaratibu wa skuli ya Manunda Tunguu pale, lakini nayo baadhi ya walezi na wana harakati wa harakati wa masuala ya haki za binaadam jambo lile hawakulipenda sana, walihisi kwamba serikali inatumia nguvu kuwaweka vijana wale na kuwatenganisha na jamaa zao na ndugu zao, utaratibu ule tukaondoka nao sasa mimi nafikiri kama nilivyosema mwanzo kuna baadhi ya mambo wakati wake umeshapita sana na mimi nakubaliana na wale wanaosema kwamba kazi ya ulezi ingefanyika vizuri zaidi katika familia zetu, badala ya shughuli hiyo kufanywa na serikali. Serikali tuiachie tu iwe na kazi za jumla jumla hivi, kutoa ushauri na maelekezo kama kazi ambayo wizara hii inashughulikia maendeleo ya wanawake na watoto kazi ambayo wanaifanya, kazi yao ni kutoa ushauri na maelekezo, lakini kazi hii ya kuendelea kutumia nguvu mimi nafikiri wakati wake umeshapitwa sana.

Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa maelezo machache kuhusu mambo yaliyojitokeza katika ripoti hii ya mtoto.

Mhe. Spika, nadhani Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeguswa zaidi na mambo mawili makubwa. Kwanza kuhusu watoto ambao wanatembea bila ya kwenda skuli, lakini la pili nadhani ni madawati ambayo vijana wengi sasa hivi wanakaa chini kama ilivyoelezwa hapa.

Mhe. Spika, napenda niseme kwamba suala zima la malezi ya watoto kama alivyosema Mhe. Waziri Kiongozi ni suala la jamii na kwa maana hiyo sote tunahusika. Wizara yangu imekuwa ikishirikiana na jamii wakipitia kamati za skuli, Wabunge, Wawakilishi na hivi karibuni Mhe. Waziri nadhani alizungumza na wawakilishi pamoja na wabunge kuhusiana na suala zima la maendeleo ya elimu na jinsi ya kulea watoto wetu.

Kwa maana hiyo basi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inashirikiana na jamii kuona kwamba vijana hao wanapata fursa ya kwenda skuli. Lakini vile vile pamoja na kwamba baadhi yao wako mitaani lakini Wizara bado inachukua jitihada ya kuwaelimisha wananchi na kuzungumza na wazazi kuona kwamba wazazi waelewe umuhimu wa vijana hawa kwenda skuli.

Mhe. Spika, kuhusu madawati nadhani ukiangalia ukurasa wa 22 kuna takwimu zinazoonyesha idadi ya wanafunzi ambao wanaandikishwa kila mwaka na inaonyesha kwamba idadi inaongezeka kila mwaka na haipungui laki mbili kwa kila mwaka, hii inaashiria kama alivyosema Mhe. Ame Mati Wadi kwamba kuna haja ya kuangalia suala zima la uzazi na suala zima la maendeleo.

Kwa maana hiyo kama alivyozungumzia Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwamba kuna umuhimu wa kushirikiana na kuona kwamba suala zima la uzazi linatiliwa mkazo hasa ukilinganisha na matokeo au athari zake katika maendeleo.

Lakini Mhe. Spika, mbali ya hilo wizara yangu imekuwa ikichukua jitihada mbali mbali kuona kwamba tatizo hili linaondoka na mara nyingi nimekuwa nikijibu kwamba wizara ina mpango wa kuongeza madawati kwa ajili ya kupunguza tatizo hili, tuna mradi au msaada wa USD ambao hivi sasa unatarajiwa kuleta madawati yasiyopungua elfu tatu na hili nadhani nimelizungumza mara nyingi hapa Barazani kwa ajili ya kupunguza tatizo hilo. Lakini pia tuna mradi wa World Bank amao utajenga shule pamoja na vifaa walimu pamoja na vitabu kwa ajili ya kupunguza matatizo haya ya masuala ya elimu katika skuli zetu.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka mimi nadhani nichangie hayo tu na nadhani waheshimiwa wajumbe wamepata uelewa. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwanza naomba nianze na kuwashukuru wote waliochangia kwa kuuliza maswali na kutoa mapendekezo kwa kuwa lengo ni kuhakikisha kwamba hii haki ya mtoto inapatikana na inaendeleza ahsanteni sana waheshimiwa wajumbe.

Namshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Waziri Kiongozi kwa maelezo yake na ufafanuzi wa kutosha sana aliosaidia katika hoja au masuala ambayo yameulizwa, namshukuru sana Mhe. Shawana Bukheti Hassan kwa ufafanuzi wake kwa masuala yote, namshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Khamis Jabir kwa maelezo yake aliyotoa kuhusu masuala ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni moja tu ambalo nahisi lilinipita kulitolea maelezo hili la kadhia ya kuungua majengo kule Mabaoni. Kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Elimu walipopata habari hiyo haraka sana walikwenda na kuangalia hali halisi na kwa hivyo hatua muafaka zinachukuliwa, hongera sana Mhe. Waziri.

Sasa niendelee kwenye masuala madogo madogo ambayo pia ni makubwa ambayo natakiwa mimi mwenyewe niyatolee maelezo, kwanza naomba sana nitilie mkazo kwamba masuala yote yanayohusu watoto mama yanatuhusu sote, kwa hivyo suala la kuangalia haki ni letu sote kwa hivyo sote tunawajibika, lakini pia naomba tuzingatie huu ujumbe maalum, naomba kwa ruhusa yako Mhe. Spika, turudie tena tuhimizane kuhakikisha watoto wanapata haki zao za kimsingi. Nasema hivi ili kusisitiza jukumu hili ni letu sote na kila mmoja wetu aliyekuwemo kwenye Baraza hili, aliyekuweko kwengine kokote wote wananchi wa nchi hii jukumu letu kuhakikisha kama watoto wetu wote wanapata haki na wanapata maadili na malezi yaliyokuwa bora na wanakuwa raia wema.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarouk aliuliza kwamba ni shehia zipi zinazoshirikisha watoto katika mabaraza yao Mheshimiwa ni shehia zote.

Mhe. Ali Suleiman Ali yeye anasema kuhusu huyu kitangi anayetamba narudia tena kwamba hiyo ni kazi yetu sote tuhakikishe kila mmoja anachukua hatua pale anapoweza, kama wewe unamjua na una ushahidi basi uende kwenye vyombo vinavyohusika na usimame imara kutoa ushahidi ili kitangi huyu adhibitiwe, sasa wewe mwenyewe Mwakilishi ndio uko kwenye jimbo mimi niko sehemu nyengine kabisa. Lakini nitakapopata madaraka hayo ya kuweza kuwa na mikono ya kuweza kushughulikia kote basi nakuhakikishia kitangi huyu nitambaka mara moja.

Mhe. Hijja Hassan Hijja umeuliza kwamba hakuna wanawake wasio tabia mbaya wanawake wote ndio wana tabia njema hilo ni jambo ambalo liko wazi, hata kama wako wanawake watukutu, lakini ni wachache sana mara nyingi sisi kama unavyotuona hatuna matatizo sana tabia zetu ni nzuri. *(Makofi)* ndio maana umeona katika kesi ambazo tunazo hakuna ya msichana kwa hivyo sisi tuendelee kuendeleza haya malezi mema na sisi tuzidi kung'ara kwa kuwa na tabia njema na hivyo vizazi vyetu vitaendelea kuwa na tabia njema, kwa sababu kama unavyojua mwana mama yeye ndio mhimili wa kila kitu yeye akiwa na tabia njema kwa mfano kama mimi mambo yote yanakuwa mazuri.

Mhe. Spika, kuna mtu aliuliza mshauri mwelekezi anatafutwa vipi suala ambalo limeulizwa pia na Mhe. Zakiya Omar Juma huyu anakuwa ni mtaalam na hapa anatafutwa kusaidia kuunda ile sheria ya watoto, tayari ameshapatikana na ameshafanya kazi sehemu mbali mbali kama Msumbiji na kwengine huyu ni mwanamke ambae anaandaa utaratibu na kutizama zile sheria hasa zitakazoweza kufaa kwa ajili ya watoto wetu.

Katika kufanikisha shughuli hiyo wadau mbali mbali wataulizwa maoni yao kwa hivyo yataunganishwa na hayo ya Mshauri mwelekezi wenyewe tunaidea mwelekezi anafanya nini sote tunakumbuka, kwa hivyo tutaweza kuchangia na kuona tunapata sheria ambazo zinatufaa zaidi sisi hatutosikiliza sana mwelekezi kwa sababu tunayo idea yake mwelekezi, lakini tutafuata utaalam wake na idea zake. Hiyo rasimu itakapokuwa tayari itatufikia sisi waheshimiwa tukaonyesha wapi pa kufanya yaliyokuwa bora katika ile sheria ili ikidhi kwa wakati huo ambao watoto watakuwa tayari kutumia sheria hiyo.

Mhe. Spika, mwengine nimeulizwa hapa ya uvunjaji wa nyumba nasema tena vilevile kama alivyosema kiongozi wangu kwamba nchi hii inaongozwa kwa utawala wa sheria na katiba, kwa hivyo naamini mambo yote yanayofanywa yanazingatia misingi hiyo, lakini mimi sijaja kuripotiwa kama kuna mtu anayelala nje sijapata hiyo taarifa kwenye Wizara yangu na hata kama ningepata basi ningeipeleka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wakapata mahala pa kujistiri kama ingekuwa imetokezea hivyo, lakini naamini hakuna aliyelala nje, kwa hivyo hakuna mtoto aliyepata baridi siku hiyo.

Nakubaliana na Mhe Zahra Ali Hamad kwamba si vyema kuwachanganya hao watu katika magereza kwa sababu sisi tuna maadili, silka na taratibu zetu sasa kuwachanganya watu wenye sifa mbaya na wale ambao watoto wadogo ambao wanaweza kukopi si jambo zuri sasa nafikiri suala hilo litafuata mikondo yake na litashughulikiwa.

Mhe. Subeit Khamis Faki kama alivyoeleza kiongozi wangu Waziri Kiongozi kwamba suala la malezi ni la wazazi wenyewe sio la Sakabona, kwa hivyo

suala hili la kuhakikisha kule Micheweni wanakwenda skuli kwa sababu skuli zipo ni suala la wazazi wenyewe, huko Micheweni wao wasimamie kwa kina kabisa na kuhakikisha kwamba hii tabia ya utoro utoro inakoma kabisa.

Mhe. Tafana Kassim Mzee yeye aliuliza mambo ya chumvi kule Pemba kama inatiwa katika madini joto, lakini mambo ya nishati na chunvi ni masuala ya wizara yake nafikiri atapata ufumbuzi yeye mwenyewe.

Lakini alisema kuna picha ambayo inaonekana kwamba watoto watapata baridi, hawa ni watoto wanaoonekana wana afya bora na hapa wameanza kufundishwa namna ya kupiga msuaki sasa wapo katika kulinda afya ya meno, kwa hivyo hakuna tatizo lolote kwa sababu unapokwenda kukoga hukogi na nguo zako unavua nguo na watoto wanajiandaa katika kujiweka vizuri.

Mhe. Zakiya Omar Juma masuala yako ya ada yameshajibiwa vizuri sana na Mhe. Shawana kwa hivyo huku sitogusa na naamini marekebisho kama alivyosema yatafanyika kidogo kidogo kwa mujibu wa hali na mfuko utakavyoruhusu. Kifaa cha *DNA* pia ndio hali ya mfuko, mfuko utakaporuhusu kitapatikana kwa sababu sasa hivi mimi ninayo habari kile kifaa cha *CT scan* kimeshapelekwa pale na mambo ni mazuri pale Wizara ya Afya, mambo ni mazuri kama mlivyoona wenyewe tarehe 22 walizindua jengo lao ambalo la kileo na wameonyesha mambo mengi ya maendeleo sana. Hongera Wizara ya afya ni kazi kubwa mnaifanya.

Mhe. Haji Mkema Haji anasema watu wanapenda kulea watoto, lakini sasa utaratibu gani, mtu kama anataka kulea mtoto utaratibu upo pale kwenye kituo cha watoto yatima kama unataka unaweza kwenda kule sisi hatuna hiyo orodha ya watoto kwa sababu sio tatizo, watoto wakiletwa wanapelekwa kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii ambako iko chini ya Wizara ya Afya sasa kule nafikiri wanaweza kuwa na idadi ya watoto wangapi ambao wapo, sisi kwetu kama alivyosema kiongozi wangu kusimamia tu sheria zinakwendaje na kupokea malalamiko yao kuyapeleka kunakohusika. Sasa mtu kama anataka mtoto aende kule au afanye utaratibu wa kuoa atapata mtoto. *(Kicheko)*

Suala lake jengine alisema mrundiko wa watoto katika madala dala hili pia ni shauri ambalo haipendezi, lakini ni kosa la kunyanyaswa watoto na kurundikwa katika daladala zinazokwenda kwenye maskuli, raia mwema anatakiwa anapoona tatizo, basi aliripoti asingojee mtoto wa Afrika akaja kusema hapa kwa sababu itakuwa imeshachelewa sana, hatua kama hizi pale pale unapiga namba ya simu au unasema mimi nimeona kitu fulani ambacho nafikiri kitaleta madhara baadae kwa vyombo husika vipo na wapo watu wa traffic, lakini kama utangojea mwaka mzima uje kunambia mimi hapa kidogo itakuwa sio sawa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk yeye alitaka mimi nimwambie mtoto ni mtu gani, yeye mwenyewe anasema bado ni mtoto. Mtoto ni mtu kuanzia dakika moja au saa moja anapozaliwa mpaka miaka kumi na saba na ndio maana mtu anapofikia miaka kumi na nane anaweza kuwa na haki ya kupiga kura, kuendesha gari na kupata zile akili ambazo sasa hivi ameshatoka utoto yuko kwenye ujana. Sasa Mhe. Mshimba ikiwa yeye ni mwakilishi anawakilisha kuanzia watoto mpaka watu wazima nafikiri yeye alikuwa anatakiwa ajue wale watu wake anaowakilisha ni kuanzia nani mpaka nani, lakini nimeshamfahamisha hivyo.

Kuhusu huyu kijana ambae anasema ni mtoto mtukutu huyu nafikiri labda pengine ana tatizo kwenye akili yake labda apelekwe akapimwe na mimi sijaona ushahidi wa kutosha kwamba ilikuja hiyo ripoti na haikufanyiwa kazi, lakini kwa yeye na mimi tulivyo kwa sababu anakuja kwa mambo mengine, lakini hili la mtoto kwa nini akachelewa au kwa kuwa walikuwa hawamjui mtoto kuanzia mwaka gani hakuja kunambia nikachukua hatua, kwa hivyo Mhe. Mshimba nakushauri siku nyengine hasa hii tabia ya watoto kwa sababu mimi ndio dhamana ya watoto serikali ya Mapinduzi imenipa dhamana niripotie haraka sana.

Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim yeye amezungumza habari ya baskeli za mitumba, mimi ningeshauri kwamba watoto waelezwe wapi pa kwenda kuchezea na hizo baskeli zao na wasiende kule barabarani kwa sababu hawajajua sheria za kuendesha baskeli katika barabara, kwa sababu wanaweza kupataajali wakaumia wakawapa wazee wao mashaka ya kuwauguza na gharama za kuwahudumia kwa matibabu, sasa kwa kweli lazima watoto hao wanapopewa hizo baskeli wawapeleke sehemu maalum kama Mnazi Mmoja pale ndio sisi tulipojifundisha baskeli tulichezea pale mpaka mpaka tukawa watalam, halafu baadae wataingia barabarani. Kuna hatari pia kwamba hizi baskeli za mitumba pengine hata breki hazina, kwa hivyo tutizame kama hizi baskeli ni nzima tunajua tunawapenda watoto wetu, lakini lazima tuwape vifaa vya kuchezea, lakini pia tueleze na taratibu za watu wakache, kwa sababu kuchezea chezea vitu ovyo ni hatari.

Mhe. Mtumwa Mbarak Kheir alisema wasiosikia tutawasaidia vipi ndio maana nilisema hili jambo ni letu sote tushirikiane katika kuwaeleza na kuwazungumza kwa njia zozote zile, kwa ushauri, taratibu kwa kukemea siku moja wanaweza kufahamu na kujirekebisha kwa sababu mtu sio mbwa. Mtu anaweza kufahamu na akaweza kubadilika kwa hivyo ulezi ni wetu sote.

Mhe. Omar Ali Shehe yeye anafahamu kabisa kwamba masuala haya MTAMBUKA na sio tu yanawagusa Wizara, lakini yanatugusa sote hasa sisi viongozi wawakilishi ndio wenye jukumu la kweli kweli kabisa kuhakikisha

kwamba tunaweka watoto wetu katika njia zinazofaa na wawe na tabia na raia wema.

Suala la kuwahami watoto wanaozaliwa taratibu hizi zimeshafanyika na siku hizi watoto wanaozaliwa hata kama wazazi wao wamekuwa na bahati mbaya wameambukizwa wao wanakuwa hawafuati taratibu hizo na huduma za afya zinafanyika hakuna matatizo tena sasa hivi.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis yeye analalamika sana wazururaji wa usiku hayo yote tunayajua, mambo yaliyokuwa hayafai ya kula unga na vileo, lakini narudia pale pale hii sio kazi ya Wizara peke yake pengine ni kazi yetu sote, kwa sababu hawa watoto tuko nao sisi huko majumbani kwetu hawako Wizarani kule wizarani ikifika saa kumi na mbili hakuna mtu.

Kwa hivyo, lazima tuelewe kama jukumu hili ni letu, kwa hivyo yote haya pamoja na kivazi na hii hifadhi ya Qur-ani najua liko somo la dini pengine Wizara ya elimu itazidisha kwa kushirikiana na Mufti ili kuona kwamba hili jambo linafanyika na watu wanaendelea. Kwa sababu unapoleta Qur-ani unamleta Mungu karibu yako zaidi kwa hivyo hata ile tabia ya kufanya maasi maasi kidogo unakuwa unaogopa yanapokuja yale mambo ya mungu, kwa hivyo jambo hili pia ni zuri na naliunga mkono moja kwa moja.

Mhe. Salum Abdalla Hamad anasema kule Pemba kwa nini takwimu haionekani sasa kama anavyosema suala la takwimu ni suala zito na gumu na linahitaji hali ya ziada, sasa kama takwimu haikuletwa na pengine pia kulingana na hali yetu sisi inakuwa vigumu sana kupata ile hakiki, kwa hivyo hiyo iliyoripotiwa ndio tuliyoweza kuipata inawezekana yapo mengine, lakini kama hayakufutikia sisi na hali yetu kupitia kila pahala. Lakini kwa vile tunakwenda kwenye mtandao wa mambo ya *information system* utaratibu tunaweza kuwa na takwimu zote, kwa sababu sio ya mambo haya tu, lakini hata figa ya kawaida tu au hisabu ndogo tu ukitaka kujua kuku wangapi wapo pahali fulani pia huwezi kupata, kwa hivyo taratibu tutaweza kufikia huko na tutazungumza na wenzetu kila takwimu tuwe nayo.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk yeye anasema atafanya nini kuhusu wale watu wanaokwenda kuoa watoto wadogo na kuwakatisha elimu yao, kwa kweli hao watu ni wabaya sana kwa sababu elimu tunajua sote ni msingi wa maendeleo na ndio mhimili mkuu. Anayepata elimu bora anakuwa na maisha bora na hata anayepata elimu bora hata ikitokezea bahati mbaya akiwa hana mume kama mimi lakini maisha yake yanakuwa hayateteruki, kwa sababu anakuwa na mshahara wake mzuri na anendeleza familia yake.

Lakini utakuwa huna elimu, huna kazi na una watoto kumi utafanya nini ndio unabomoka kila pahala kutokana na ugumu wa maisha. Lakini elimu ni muhimu sana na tutahakikisha kwamba tunaweka sheria za kuwabana zaidi watu hawa wakorofi wachache ambao wanaona watoto wazuri na wanawaoa mapema na kuwaharibia maisha yao. Naamini vita hivi tutashinda sisi hasa nikiwa jemedari mimi mwenyewe.

Mhe. Spika, Mhe. Ame Mati Wadi yeye nimeshasema kutokana uwezekano wa kupatikana takwimu, hata hizo za kuzaliwa kwa sababu si watu wote wanaokwenda kiripoti. Wengine wanaona hakuna haja madhali kazaliwa salama ndio basi imekwisha. Lakini wakati tunawafahamisha wananchi wetu umuhimu wa kuripoti sio kwa uzaliwaji tu, lakini mpaka kifo lazima kiripotiwe ndio mambo yetu yatakaa sawa.

Kwa hivyo tutaendelea kushirikiana ili kuhakikisha tunawahimiza wananchi wetu kwamba mtoto yeyote anayezaliwa basi lazima akaandikishwe ijulikane. Na mtu yeyote anayekufa pia akaandikishwe ili kumbukumbu zetu zikae vizuri, kwa kutusaidia kupanga mipango yetu ya maendeleo, kwa sababu tutakuwa tunajua tuna watu wangapi na wangapi wamekufa. Tutajua nini tufanye, lakini vyenginevyo mipango itakuwa migumu kama tutakuwa hatuna takwimu zilizokuwa sahihi.

Namalizia kwa kusema kwamba nawashukuru sana waheshimiwa na naomba tuwe pamoja katika kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata haki hizi. Wanapata afya njema na sisi tunakuwa salama, tunaepukana na mambo yote ya uzalilishaji ambao ni kinyume cha haki. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Haikuwa hoja lakini lakini niwahoji wale wanaokubali na kupokea taarifa ya utekelezaji wa mtoto wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, naomba uliahirishe Baraza lako tukufu kabla ya muda wake mpaka kesho tarehe 25//6/2009 Saa. 3.00 asubuhi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 1.32 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 25/6/2009 Saa. 3.00 asubuhi)